NAFSI ZILIZO KIFUNGONI SASA

Asante. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

Baba wa Mbinguni, tunatoa shukurani Kwako, leo, kwa majaliwa haya ya kukusanyika wakati mwingine tena, tukijua ya kwamba siku moja tutakusanyika kwa mara yetu ya mwisho, kama wanadamu, kisha tutakusanyika katika hali ilyotukuzwa pamoja Nawe, nao wote waliokombolewa wa nyakati zote watakusanyika huko.

2 Loo, mioyo yetu inadunda sana, juu ya . . . na kwa matumaini makubwa, tukingojea ile saa ifike! Tukiwa na jambo hilo, hofu zote hutuacha. Hatuna cha kuhofu, hatuna cha kuhofia sana. Tunaitazamia ile ahadi ambayo Mungu wa Milele ametupa, nasi tunajua ya kwamba ni Kweli. Hiyo ndiyo sababu tunaishi. Tunaishi kwa ajili ya jambo hilo, saa hiyo, wakati huo, wakati huu uharibikao utakapobadilishwa, nasi tutafanywa kama Yeye, wala hakutakuwako na maradhi tena, hakuna huzuni tena, hakuna majonzi tena. Loo, yote yatakuwa yameisha wakati huo. Na kwa furaha ya moyo, sisi, katika imani na ujasiri, tunaitazamia Siku hiyo.

3 Hiyo ndiyo sababu tumekusanyika hapa leo, Bwana, kuungama makosa yetu na kuomba rehema. Hiyo ndiyo sababu tuko mbele ya madhabahu hii asubuhi hii, kwa kuwa tunajua ya kwamba sisi tunapatikana na mauti, na kuna makosa mengi ndani yetu, nasi tumejaa makosa. Bali tunakuja kukiri makosa yetu, kisha tumwangalie Baba yetu wa Mbinguni kwa mioyo mikunjufu, kwa ajili ya baraka na kufanywa upya nguvu na imani, ambayo angetupa katika saa hii, kwa kuwa tumekusanyika hapa kulingana na ile ahadi, "katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu." Kwa kuwa tunadai ya kwamba tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, kwa ahadi Yake, nasi tumeshikwa katika hali ya Kimbinguni, tukiketi pamoja Naye sasa. Yeye na atufundishe asubuhi ya leo mambo ambayo Yeye angetaka tujue, kisha atupe Mkate wa Uzima, ili kwamba tupate kutiwa nguvu kwa ajili ya siku za usoni zilizo mbele yetu. Tujalie, Bwana. Hii ndiyo dua yetu tunayoomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mnaweza kuketi.

4 Habari za asubuhi, kwa kila mtu. Na ni vizuri sana kukusanyika hapa pamoja nanyi tena asubuhi ya leo, katika hali hii ya Kimbinguni ya kuabudu.

5 Tumechelewa kidogo tu, tulipata si- . . . simu mbaya, mbaya sana dakika chache zilizopita; mvulana amelala pale, anakufa. Na kwa uhakika kama ninavyosimama hapa, Bwana aliugusa mwili wake na kumwachilia aenda zake. Kwa hiyo . . .

6 Na m—m—mvulana akisimama hapa, ambaye ni mwana wa binamu yangu. Wao walikuwa Wakatoliki kweli, kwanza, lakini walienda misa asubuhi ya leo halafu kitu fulani kikawaambia waje huku. Na kwa hiyo wao. . .Kuna badiliko. Kwa hiyo basi wao—wao wanakuja nyumbani sasa, wapate kujiandaa kwa ajili ya ubatizo wa maji. Kwa hiyo wao ni—wao ni. . .mambo tu ya ajabu ambayo Bwana wetu anafanya wakati wote. Yeye hufanya tu mambo wakati wote. Wao walikuja kuingia, nao hawakuweza kuingia. Walisema hakukuwa na njia kamwe ya kuingia.

7 Nikasema, "Vema, kama mnataka kuzungumza nami," nikasema, "vema, njoni tu nyumbani, nasi tutazungumzia jambo hilo, huko."

8 Kwa hiyo nikafikiri, nikienda zangu New York sasa, kwenye mkutano huu unaokuja, ya kwamba lingekuwa ni jambo zuri sana. . .Najua ningeburudika nikija na—na kusaidia kuwasha moto wangu kutokana na moto mliokuwa nao ninyi nyote, nasi tukasimama kwa siku moja, asubuhi ya leo. Basi tulifika jana, juzi, adhuhuri.

9 Halafu inatubidi kuondoka. Nilikuwa niondoke, alasiri ya leo, bali nafikiri nitaenda. . .Nasi tunaanza asubuhi, mapema, mapema sana. . .Huenda tukawa na theluji barabarani, na kadhalika, kati ya hapa na New York. Hatuna budi kupitia Virginia, kupitia milimani, na pia kupitia kwenye ile ya Allegheny, halafu basi sehemu tu ya chini ya—ya Adirondack.

10 Kwa hiyo tutaanza, nasahau, ni kwenye uwanja wa michezo kule, mpya. Waliuvunja ule uwanja wa kale wa Mt. Nicholas, nasikia. Wakajenga huu mpya. Basi kadiri nijuavyo mimi, tunapata kama baadhi ya siku za kwanza usiku ambazo ziko. . . ambazo zilikodishwa. Kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo, kwa ajili ya watu wa Kipentekoste wa New York kuu. Nami nafikiri tuna makanisa kadha yanayoshirikiana, nasi tunatarajia wakati mkuu.

11 Nasi tutarudi, Bwana akipenda, mnamo juma lijalo. Na—na kama ni mapenzi ya Mungu, mbona, tunatumaini kupazuru mahali hapa Jumapili, juma lijalo, kwa—kwa ajili ya ibada ya Jumapili asubuhi.

12 Halafu nilimvamia mchungaji wetu tena, kama ninavyofanya daima, mnaona, nami—nami nikafikiri labda kama ningeingia, na hata bila kuomba. Na halafu kwa kuwa kuna kundi zuri hapa, na watu ninaowaona kutoka nje ya mji, wako hapa; nilifikiri labda, usiku wa leo, kama mchungaji hana kitu maalumu, kwamba tungekuwa na ibada ndogo usiku huu, fupi tu, na, vema, labda tuwaombee wagonjwa. [Ndugu Neville na kusanyiko wanafurahi—Mh.] Asanteni.

13 Tunatumaini kuwaombea wagonjwa usiku wa leo, kuzungumza juu ya kuponya Kiungu na—na kuwaombea wagonjwa. Tuanze mapema ili kwamba tuweze kutoka mapema.

Na kama mchungaji akipenda, kile... Kwa kawaida mnaanza saa moja na nusu. Sivyo? Vipi kuhusu kuanza saa moja usiku, moja? [Ndugu Neville, "Amina."—Mh.] Halafu hebu nianze kwenye saa moja na nusu, na hiyo itaniwezesha kutoka kwenye saa mbili ama mbili na nusu, halafu inawapa watu wakati basi wa—wa kutoka, kama jambo hilo ni—hilo ni—ni sawa. Kila mtu alicheka ni—niliposema mbili, ama mbili na nusu. Ni—ni—ninatumaini kutoka kwenye wakati huo. Kuwaombea wagonjwa, mwajua, hatujui kamwe.

14 Kwa hiyo tumekuwa na—na wakati mzuri sana tangu tulipowaacha kwenye msimu huu uliopita wa Mwakani, mapema, naye Bwana ametubariki katika mambo mengi makuu. Kwamba... Na usiku wa leo, kama Bwana akipenda, ninataka kuwaambia juu ya kuzuriwa kwa mwisho nilikozuriwa, kutoka kwa Mungu, huko Colorado, majuma machache yaliyopita. Na hilo ndilo nililofikiria ningaliwaleteeni sasa, labda kuchochea imani kwa ajili ya ibada nzuri ya kuponya usiku wa leo, kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka.

15 Naam, asubuhi ya leo, kuingia moja kwa moja katika ibada, mimi... Jambo fulani liliugusa moyo wangu yapata mwezi mmoja uliopita. Na huenda likawa, sasa, nafikiri wao wana-... Wao wanaunasa huu? Wao wanaunasa huu? Naam. Vema. Ili kwamba niweze kujua ni mahali gani, kama kanda hii ikiwafikia wengine. Siwezi kusema hayo ambayo nitazungumza habari zake asubuhi ya leo... Siwezi kusema ya kwamba ndi—ndi—ndicho... Ninajua ni kweli, mnaona, sehemu ya Ujumbe itakuwa sahihi. Lakini jambo lenyewe, ninalotaka kufanya, ni swali moyoni mwangu. Linaonekana dhahiri sana. Na hata hivyo tangu niliporudi, na tangu mimi... lilipofunuliwa kwangu, nimekuwa nikiogopa sana kwamba ningetamka jambo lisilo sahihi na huenda nikaacha mawazo mabaya kwa watu. Na ni... Nami...

16 Yale niliyokuwa nimeandika muhitasari, juu ya yale niliyokuwa niseme, niliondoa sehemu yake, ili kwamba nisilifanye zito sana. Kwa maana, mnaona, kama—kama mtu fulani... ni—ninampenda Bwana Mungu, na, jinsi tu ninavyojua ninampenda, ni kwa sababu ninawapenda ninyi. Mnaona? Hivyo ndivyo jinsi ninavyojua tu. Na hata hivyo mimi—mimi sitaki nifunuliwe jambo lo lote halafu nisiwaambie, kama ni la kuwaambia. Halafu ninahofu ya kwamba kama nikisema jambo ambalo ni zito sana, huenda likamuudhi mtu fulani. Kisha, mnajua, ni... Karibu inakubidi kufika tu jukwaani halafu usikie ukiongozwa kusema unalotaka kusema. Ni hayo tu. Na halafu wakati mwingine unaweza kusema kitu fulani, ndipo mtu fulani angepata... mwelekeo mwingine kwenye kitu hicho, nao wangeenda upande *ule*; na halafu mtu fulani angesema, "Loo, hii ni *hili*, mnaona."

17 Lakini nawatakeni mjue ya kwamba ninachotaka kusema ni kuthubutu tu, nalo neno *kuthubutu* maana yake ni "kufanya bila mamlaka." Kwa hiyo mimi . . . Si—sisemi kwamba jambo hili ni kweli, bali ni wazo dogo tu ambalo huenda nikawaachia, ili kwamba mpate kulipima na kuona mnalowazia juu yake. Kisha lita-, bila shaka, lita-—litakuwa la Kimaandiko, maana nisingehubiri kitu cho chote . . .

18 Lakini hivi sasa hiyo ndiyo ile saa? Je! jambo hili limefikia kwenye saa hii, na hivi mambo haya yamemaanisha jambo hilo? Ninaomba, kwa yote yaliyo ndani yangu, ya kwamba siyo. Mnaona? Ninaomba kwamba si kweli, ya kwamba siyo ile saa. Itakuwa, bali hivi imefikia wakati huo sasa? Mnaona, hilo ndilo sijui. Naam, kila mtu anafahamu, kabisa, ya kwamba mimi sijui? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Mimi tu . . . Je! huu ndio ule wakati? Kama ndio, Mungu na aturehemu. Lakini, kama sio huo wakati, hebu . . . utakuja.

19 Naam, mara tuwezapo, tuna mpango mkuu wa kusafiri mbele yetu, Bwana akipenda. Nami sina budi kwenda nchi za ng'ambo, mara baada ya Krismasi, huko Ulaya na Asia; Ulaya, hasa. Kisha ninarudi hapa Marekani, kwa ajili ya ibada chache, halafu ninarudi Afrika Kusini. Nitaanza tarehe mbili Se—Septemba, huko Durban, kisha niondoke kwenye tarehe mbili, nadhani, mpaka mnamo yapata tarehe kumi, halafu nina siku mbili kutoka huko kwenda Johannesburg na kuanza tena. Lakini nadhani ni mwezi wa Aprili, tutaanzia kwenye nchi za Scandinavia, huko Norway na Sweden na—na Finland, na—na Uholanzi na Uswisi na Ujerumani, na—na kupitia Ulaya kule. Kwa hiyo iweni katika maombi kwa ajili yetu.

20 Tuna mikutano michache hapa, majira ya Krismasi sasa, mara baada ya Krismasi. Jambo jingine, tunataka kuwa hapa kwenye Krismasi, mnaona, nyumbani. Watoto wanataka kuja nyumbani, kwenye Krismasi. Nasi—nasi tunapenda Arizona, lakini mnajua ja—jambo tunalokosa, wala hutuwezi kuliepa, ni kanisa hili pamoja na ninyi watu. Haidhuru twende wapi, tufanye nini, ni tu . . . Watoto, mimi, mke na kadhalika. Kamwe hakuna mahali kama hapa. Hiyo ni kweli. Hakuna kamwe.

21 Nimeabiri bahari saba, nami ni—nimezuru kila mahali, bali hakuna mahali panapoonekana wakfu kwangu kama mahali hapa padogo papa hapa. Hapa ndipo. Wewe ondoka tu mahali hapa siku moja, kama unataka kujua. Kuna kitu fulani tu juu ya mahali hapa. Nimehubiri kila mahali ulimwenguni, karibu kila mahali, nami kamwe sijawahi, wakati wo wote, mahali po pote, kumsikia Roho wa Mungu, kwa uhuru na kadhalika, kama ninavyomsikia nikisimama papa hapa. Hapa ndipo penyewe.

22 "Mungu, pajalie . . ." Kama ile siku niliyoweka jiwe la pembeni kule, nilisema, "Bwana Mungu, usipaache paanguke."

Watu walisema, "Katika miezi miwili, patakuwa gereji."

23 Nikasema, "Usipaache paanguke, Bwana. Hebu pasimamishe, na watu humu ndani wawe wanakusifu wakati atakaporudi Yesu." Ninatumaini patakuwa hivyo.

24 Sasa hebu tufungue Biblia sasa, na—na kumtarajia Bwana kutupa baraka Zake. Nasi tunataka kusoma Maandiko fulani. Nina Maandiko yaliyoandikwa hapa ambayo ninataka kuyarejea, na mihitasari fulani. Nami ninataka kusoma kutoka sehemu tatu kutoka kwenye Biblia, nami nitawapa hayo, kwanza. Ninataka kusoma katika Yuda 5 na 6. Yuda ni Kitabu kimoja tu, mnajua. Kisha ninataka kusoma Petro wa Pili sura ya 2, 4 na 5. Kisha ninataka kusoma Petro wa Kwanza, 3:18 hadi 20.

25 Nalo somo langu asubuhi ya leo, Bwana akipenda, ni: *Nafsi Zilizo Kifungoni Sasa*. A-ha. *Nafsi Zilizo Kifungoni Sasa*, zimefungwa, zimehukumiwa milele. Kamwe, hazina njia ya kuokolewa, mnaona, nafsi zilizowekwa kifungoni sasa.

26 Sasa hebu tusome katika Kitabu cha Yuda, kwanza. Ninaamini nimepaandika hapa kama mahali pa kwanza, katika Yuda; kisha tufungue Petro wa Pili, kisha—kisha kwenye Petro wa Kwanza. Sasa, Yuda, ningetaka kuisoma yote; bali ili kuokoa wakati, kwa maana tayari ni saa nne u nusu, nitaanzia na aya ya 5. Naam, Yuda alikuwa ni ndugu, ndugu wa kambo, wa Yesu Kristo, kama tujuavyo sote. Mnaona? Yeye alikuwa mwana wa Yusufu.

> *Tena napenda kuwakumbusha, ijapokuwa* ninyi *mmekwisha kujua haya yote, ya kwamba Bwana, akiisha kuwaokoa watu katika nchi ya Misri, aliwaangamiza baadaye wale wasioamini.*

27 Akawaokoa, kwanza, akawapandisha kutoka Misri, kisha ikambidi kuwaangamiza kwa maana hawakuendelea na ujumbe wao, mnaona.

> *Na malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yao yaliyowahusu,* tayari *amewaweka katika* vifuli. . .*vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu.*

28 Malaika ambao siku moja walikaa Mbinguni, wala hawakuilinda enzi yao na hali waliyokuwa, wakaanguka, na sasa wamo katika vifungo vya Milele na Milele vya giza, vifungo vya milele vya giza, wamewekwa katika hali hii mpaka kwenye ile Hukumu ya ile Siku kuu wakati watakapohukumiwa pamoja na wasioamini wengine.

29 Sasa katika Petro wa Pili, sura ya 2, kuanzia kwenye aya ya 4, ambayo itakuwa kitabu kimoja ama viwili nyuma yake, mnaona.

> *Kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni, akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu;*

Wala hakuuachilia ulimwengu wa kale, bali alimhifadhi Nuhu, na watu wanane, *mjumbe wa haki*, *hapo alipoleta Gharika juu ya ulimwengu wa wasiomcha Mungu*;

30 Hakuwaachilia Malaika; akawaweka katika vifungo vya giza, kisha akauhukumu ulimwengu wote kwa maangamizi, ya—ya Nuhu.

31 Sasa katika Petro wa Kwanza, sura ya 1 na. . .Petro wa Kwanza, sura ya 3, kuanzia na aya ya 18, tunasoma tena. Naam, sikilizeni kwa makini sasa.

Kwa maana Kristo naye aliteswa m*ara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasi*o *haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali Roho yake akahuishwa, . . .mwili wake ukauawa, bali Roho yake akahuishwa,*

Ambayo kwa hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri watu hawa waliokuwa kifungoni;

Watu wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji.

Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unatuokoa sisi *pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo.*

Naye yupo mkono wa kuume wa Mungu, amekwenda zake mbinguni, malaika na enzi na nguvu zikiisha kutiishwa chini yake.

Na tuombe tena.

32 Sasa, Baba wa Mbinguni, mstari kama huo wa Maandiko hapa, mashahidi watatu, sehemu tatu katika Maandiko zikitoa ushuhuda. Nawe umesema katika Neno Lako, ya kwamba, "Katika kinywa cha mashahidi wawili ama watatu, kila neno lithibitike." Sasa nakuomba Wewe, Ee Mungu, ya kwamba utakuja kwa watu kisha utalifasiri Neno hili, Ujumbe huu, katika nuru inayopaswa kuwa, ili kila mwanamume, mwanamke, mvulana, ama msichana, apate kufahamu katika kiwango kile ulichowakusudia kufahamu, na sasa tukijua ya kwamba mashahidi watatu hawa wanashuhudia Kweli.

33 Nami ninaomba ya kwamba utamtuma Roho Mtakatifu juu yetu sasa. Nasi tutamwangalia Yeye aliye Mfalme wetu, kati yetu asubuhi ya leo, Bwana Yesu Kristo; ambapo tumeinuka sasa kwa imani, tukiketi katika sehemu hizi za ulimwengu wa Roho katika Yeye. Tunaungojea Ujumbe Wake. Uzungumze kupitia kwetu, Bwana, uusikilize kupitia kwetu, tunapokuomba Wewe uitahiri

midomo inayonena na maskio yanayosikia, ili kwamba iwe kwa ajili ya heshima na utukufu wa Yeye aliye Maandiko. Kwa maana tunaomba hayo katika Jina Lake. Amina.

34 Naam, kumbukeni ibada usiku wa leo, ibada ya kuponya. Sidhani ingekuwa muhimu kutoa kadi za maombi, kwa hiyo tunawaombea tu wagonjwa. Nina jambo ninalotaka kuwaambia, nami—nami ninaomba ya kwamba litalileta tu kusanyiko katika mahali ambapo kutakuweko na kila namna ya kuponya. Ninajua litatukia kama tukiliamini tu namna hiyo.

35 Sasa hili, nafsi zilizo kifungoni sasa, nafsi zilizo kifungoni sasa!

36 Sasa, nafsi ya mtu si mwili wa mtu, ni nafsi. Mnaona? Nayo nafsi ni kitu ambacho ni—ni tabia ya roho. Halafu basi wakati tabia ya mtu. . . Wakati aliposema, "Sisi tumekufa," Maandiko yanatwambia dhahiri ya kwamba, "tumekufa, na maisha yetu yamefichwa katika Mungu kwa Kristo, yakatiwa muhuri mle kwa Roho Mtakatifu." Naam, si kwamba mwili wako ulikufa; si roho yako iliyokufa. Tabia ya roho yako ndiyo iliyokufa; mnaona, tabia, ambayo ni nafsi. Tabia ya nafsi yako ni—ni Mungu, kama umezaliwa mara ya pili. Kama hujazaliwa, ni ya ulimwengu. Kila kitu kinachoanza hakina budi kukoma, kwa hiyo basi, njia pekee wewe unayoweza kuwa na Uzima wa Milele ni kuwa na Uzima ambao haujapata kuanza. Basi uhai wako ulianza ulipozaliwa, wakati Mungu alipopulizia pumzi ya uhai katika pua zako nawe ukawa nafsi iliyo hai, ndipo ukaanza basi. Lakini wakati ulipo- . . .

37 Tabia ile iliyokuwa ndani yako, kwa tabia ulikuwa wa ulimwengu, umetengwa na Mungu, kwa kweli ulikuwa ni mnyama. Hiyo ni kweli kabisa. Kila mtu anajua ya kwamba sisi ni jamii ya wanyama wanaonyonyesha watoto. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Sisi, sisi ni wanyama wanaowanyonyesha watoto, sisi ni jamii ya wanyama wenye damu moto, hivyo ndivyo tulivyo kwa maumbile yetu ya duniani. Lakini, mnaona, kile kilichotufanya tofauti na wanyama wengine wanaowanyonyesha watoto, kwa—kwamba Mungu aliweka nafsi ndani yetu. Mnaona? Naam, wanyama wengine wanyonyeshao haiwabidi kuvaa nguo. Hakuna mnyama mwingine inayembidi kuvaaa nguo kufunika aibu yake, isipokuwa sisi. Sisi ndio tu tunaofanya jambo hilo, kwa maana tuna nafsi. Lakini, angalia, Mungu, hapo mwanzo, alijua jinsi ambavyo mwanadamu angekuwa. Naye akaumba nchi, kisha akaleta kila namna ya wanyama, tangu walio wa hali ya chini sana hata walio wa hali ya juu sana; mnyama wa hali ya juu kuliko wote akatokea, alikuwa ni mwanadamu.

38 Halafu basi, kwanza, mwanadamu aliumbwa, alikuwa mtu wa roho, katika mfano wa Mungu.

39 Ambapo, “Mungu ni Roho,” Yohana Mtakatifu 4. Naam, “Yeye ni Ro—Roho. Nao wamwabuduo Yeye, wanamwabudu katika Roho na katika Kweli. Na Neno Lako ndiyo Kweli.” Sasa, tunamwabudu Yeye katika Roho na Kweli. Yeye ni—ni Roho aliye Hai.

40 Basi hapakuwepo na mtu wa kuilima nchi, basi Mungu akamfanya mtu kutoka katika mavumbi ya nchi.

41 Ndipo akatoa ubavuni mwake, kitu kilichotokana na kingine, ubavu; na, kutokana na huo, akamtenganisha mtu huyu aliyekuwa na asili mbili, ambazo zilikuwa ni ya kike na ya kiume. Basi Yeye akatoa ile ya kike, maana ilikuwa ni upendo, ndipo akaiweka katika mtu aliyeitwa Hawa, ambaye Adamu alimwita Hawa, ambaye alikuwa mkewe. Hapo ndipo upendo wake, wa kawaida, upendo wa kibinadamu, ulishikilia mkewe. Hivyo ndivyo mtu anapaswa kuwa leo, naye mwanamke amrudie mumewe. Mwanamume, ya kiume; mwanamke, ya kike.

42 Halafu basi, mnaona, baada ya kumfanya mtu katika Mfano Wake Mwenyewe, “akawaumba, mwanamume na mwanamke,” hapakuweko na mtu wa kuilima nchi. Ndipo Yeye akamweka katika mavumbi ya nchi, na kwa hiyo akawa . . . yeye alikuwa ndiye mtu yule. Mtu huyu wa kibinadamu alikuwa jamii ya wanyama wanyonyeshao watoto, mnaona, alikuwa mnyama; lakini Yeye akaiweka roho hii ya Mungu, uhai, ndani yake, ndipo akamfanya katika msingi kwamba yeye angeweza kujichagulia. Halafu wakati huyu mtu . . .

43 Sasa tunafikiri sisi ni kitu cha maana. Kumbukeni tu, sisi ni kitu gani? Donge la mavumbi. Hivyo tu. “Na kwa kuwa wewe ni mavumbi, utarudi mavumbini.” Kwa hiyo mnapomwona mtu huyu akitembea barabarani, anafikiri yeye ni mtu wa maana sana, mnajua, na ana elimu kidogo na kadhalika; kumbukeni, ni donge la mavumbi ya Indiana. Hiyo tu. Basi mwanamke huyo aliyevalia kaptura, huku anavuta sigara na kukosa adabu barabarani, akikatika-katika kama kwamba nchi nzima ni mali yake, ni donge la mavumbi ya Indiana, na hivyo ndivyo linavyorudia. Kwa hiyo wewe si kitu kikubwa sana kwanza, unaona. Kwa hiyo, hiyo ni kweli, hivyo ndivyo ulivyo.

44 Lakini, nafsi hiyo iliyo mle ndani, mnaona, nafsi hiyo ndiyo Mungu anayotenda kazi nayo, mnaona. Kama tu anaweza kuifanya tabia hiyo, roho hiyo, ikubaliane Naye, basi tabia hiyo inakufa, hiyo tabia pamoja na kuipenda dunia vinakufa, tena mambo yaliyomo katika dunia yamekufa. Mnaona? Kwa sababu, “Ukiipenda dunia, ama mambo yaliyomo katika dunia, kumpenda Mungu hakumo ndani yako.” Mnaona? Na mtu hana budi kuzaliwa mara ya pili. Kwa hiyo, tabia hii haina budi kufa, na tabia ya Mungu inakuja na kuishi ndani yako. Naye Mungu ndiye kitu tu kilichopo ambacho hakikuanza wala hakiwezi kukoma.

45 Basi, kwa hiyo, Yeye ameshirikisha, mnaona, na kumchukua mtu huyu, wa duniani, na Roho hii ya Milele, na kuviweka pamoja. Kwa sababu, Mungu alijionyesha Mwenyewe katika jambo hilo, kwamba alifanyika mwanadamu wakati alipofanyika Yesu Kristo, Naye alikuwa Mungu, mnaona. Mungu alikuwa ndani ya Kristo; ambaye, mnaona, aliishi ndani Yake, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Na, kupitia kwa Mtu huyo mkamilifu, kila mmoja wetu asiyekamilika anayemwamini Mungu na amelikubali Hilo, anakuwa ukamilifu Wake.

46 Wala hakuuacha mwili Wake kamwe kuona uharibifu, wala hakuiacha nafsi yake kuzimu, bali alimfufua katika siku ya tatu, Naye yu hai milele. Nasi tutakuwa na mwili kama mwili Wake wa utukufu.

47 Hiyo ndiyo sababu tunabatizwa katika Jina Lake, ili tupate kufufuka katika Jina Lake, katika mauti Yake, katika kufufuka Kwake, ili kwamba tupate kufufuka tena, tukishuhudia kwa ulimwengu ya kwamba tuna Uzima mpya, ya kwamba yule mtu wa kale amekufa. Tuliizika tabia ile ya kwanza. Mnaona? Tabia hiyo ya kwanza imeondoka, na sasa sisi ni tabia Yake. Yeye anaishi ndani yetu, nasi hatufanyi mapenzi yetu wenyewe. Tunafanya mapenzi Yake. Hutuwazii mawazo yetu wenyewe. Ile nia, nia ndiyo inayowaza. Ile nia iliyokuwamo katika Kristo Yesu imo katika kila mwamini. Mnaona, hiyo—hiyo hapo ile nafsi, na hiyo ndiyo tunayonena habari zake. Basi, hiyo ndiyo ile sehemu ninayowazia sasa, ya kwamba hiyo imo ndani yetu, ile nafsi.

48 Sasa, kama tukiangalia, katika hili, kuna mambo mengi yanayotukia wakati mwingine, nasi hatujui kwa nini yatukie, nasi tunajiuliza wenyewe, na tunawauliza wengine. Lakini hatimaye, baada ya kitambo kidogo, tunaona kwamba, kama sisi ni Wakristo, yote yanatendeka vema kabisa, kwa namna fulani. Mmeona jambo hilo. Wakristo wote wanaona jambo hilo. Hatujui kwa nini tulifanya jambo hilo.

49 Nilishangaa wakati mmoja, wakati nilipoisoma Biblia kwa mara ya kwanza, "Kwa nini Mungu akamwacha Ibrahimu, huyo mtu mkuu, kupata kusimama pale na kusema ya kwamba Sara hakuwa mkewe?" Na jinsi alivyomfanya asimame pale na kusema uongo juu ya jambo hilo, na mambo yale aliyofanya, na halafu jinsi ambavyo alipata kumwacha Ibrahimu aondoke kwenye nchi ya ahadi ambayo alimwambia asiiache. Myahudi ye yote anayeondoka kwenye nchi ya ahadi amerudi nyuma, kwa maana Mungu aliwapa hiyo wao na kuwaahidi kukaa humo, mnaona, nao wakaiacha. Kwa hiyo akashuka akaenda Gerari. Lakini kama isingalikuwa kwa sababu ya jambo hilo . . .

50 Halafu Abimaleki, mfalme huyo kule chini kwenye nchi ya Wafilisti, alimpenda Sara naye alikuwa anataka kumwoa, naye alikuwa ni mtu mzuri, mtu mwenye haki. Na baada ya yeye labda . . .Jambo hili linasikika la kuchekesha, bali

kulifanya dhahiri sana kwenu. Baada ya kuoga jioni na kuvaa pajama yake, na kusema sala zake kisha akaenda kulala, Bwana alimtokea akasema, "Wewe ni kama tu mtu aliyekufa," na yule mtu hakuwa ametenda jambo lo lote. Mnaona? Yeye alikuwa amedanganywa kabisa, na Ibrahimu pamoja na Sara. Hayo ni kweli. Akasema, "Una mke wa mtu mwingine, unaona. Na si—sitayasikia maombi yako, hata uombe namna gani. Wewe ni kama mtu aliyekufa. Lakini mtu huyo ni nabii Wangu." Mnaona?

51 Mnaona, ni vigumu kuelewa jambo hilo, mnaona. Bali kama isingalikuwa ni kwa ajili ya jambo hilo, tusingelijua neema ni nini.

52 Kwa nini akatoka akaenda akamwoa Hajiri, baada ya kuwa na mke mzuri kama Sara? Wala yeye hakutaka kufanya jambo hilo, mnaona, bali Sara alimwambia. Kisha Bwana akamwambia, "Sikiliza alilokwambia Sara." Kwa nini? Ilibidi kuwe na Ishmaeli, "ili kwamba mjakazi huyo na mwanawe wasingerithi pamoja na mwanamke huru pamoja na mwanawe." Mnaona ninalomaanisha?

53 Mambo haya yote ni mifano. Kwa nini ilimbidi nabii yule kuoa malaya na kupata . . . pamoja na watoto hawa, kupata watoto wawili kwake? Kama ishara. Kwa nini mmoja akalala kwa mkono wake wa kulia kwa siku mia tatu na arobaini, kisha akalalia upande ule mwingine kwa siku kama hizo namna hiyo? Kama ishara. Mmoja alivua nguo zake akatembea mbele ya Israeli. Na, sasa, mambo hayo yote, ilikuwa ni mifano na vivuli, mnaona; nasi hatuna budi kuwa na mambo hayo, kujaza.

54 Na, mara nyingi, mambo hutukia kwetu hata tunashangaa kwa nini yatukie. Ni Mungu akitangulia kutuonyesha kitu fulani.

55 Naam, kama mvulana mdogo, nanyi mnajua hadithi ya maisha yangu, daima ni—niliamini, tangu ninapoweza kukumbuka . . . Moja ya mambo ya kwanza ninayokumbuka . . . kwanza Sasa hili, sasa, huenda uliniambia jambo fulani jana, nami ningelisahau ifikapo leo. Bali kuna mambo fulani, kule nyuma, yaliyotukia katika siku za ujana wetu, wengi wetu tuko namna hiyo, ambayo daima tunayakumbuka. Na jambo hili linasikika karibu ni la kuchekesha kusema hivi, bali ninakumbuka nilipokuwa nikitambaa, nikiwa na nguo ndefu. Watoto wachanga, sasa baadhi yenu watu wa rika yangu mngekumbuka jambo hilo, watoto wachanga walikuwa wanavaa kanzu. Nami ninakumbuka nikitambaa, na kutoa theluji kwenye miguu ya mjomba wangu na kuila, wakati alipoingia na alikuwa amesimama mekoni.

56 Halafu jambo jingine ninalokumbuka likitukia maishani mwangu, lilikuwa ni ono, la kwanza nililopata kuona, na likaniambia ningeishi sehemu kubwa ya maisha yangu karibu na mji unaoitwa New Albany. Nami nilikuwa mtoto mchanga wa

milimani kule juu, hata hapakuwepo na daktari nilipozaliwa. Na—nami ni—ni...Mwajua, wao...Nimeishi hapa yapata miaka hamsini, papa hapa; ono.

57 Halafu jinsi daima nilivyojua kulikuwa na Mungu mahali fulani, na nilipokuwa mvulana mdogo akazungumza nami, "usivute sigara, wala kunywa pombe, wala kuchafua" mwili wangu, hiyo ni kuzurura kizinifu na wanawake na kadhalika. Daima nilihofu sana jambo hilo, nami nilikuwa kijana mwanamume.

58 Ndipo nilikuwa nimetoka kuwinda wakati mmoja, jambo ambalo linaonekana ni asili ya pili kwangu, kupenda kuwinda. Nami nilikuwa huko nje nikiwinda na kijana fulani, Jim Poole, mtoto mzuri. Nafikiri mtoto wake huja hapa kanisani, maskini Jim, na jamaa nzuri ya watu. Ninaijua jamaa ya Poole. Mimi na Jimmy tulilala pamoja na kuishi pamoja tangu tulipokuwa wavulana wadogo shuleni. Tumeachana kwa yapata miezi sita, kwa umri. Basi Jimmy aliachilia bunduki yake ikafyatuka, nayo ikanipiga risasi katika miguu yote miwili, akiwa karibu sana nami, kwa bunduki. Nilipelekwa hospitalini, na, kule, nikilala kule nikifa, hakukuwa na penicilini wala cho chote katika siku hizo. Naam, sasa, wao waliniwekea kitambaa cha mpira chini, nami najua usiku huo...Walikuwa wanifanyie upasuaji asubuhi yake.

59 Walichukua tu na kulisafisha lile jeraha, huku vipande vikubwa vya nyama vimelipuliwa, nao wangechukua makasi na kuvikata, nami ilinibidi kushikilia mikono ya mwanamume fulani. Nao walikuwa na Frankie Eich, alijiuwa tu hivi majuzi, nao iliwabidi kushikilia, kukwatua mikono yangu kutoka kwenye viwiko vyake, walipo—walipomaliza. Nilipaza sauti na kulia, huku nimeshikilia namna hiyo, nao wakikatilia mbali sehemu hiyo ya mguu. Nilikuwa na umri wa miaka kumi na minne, mvulana tu.

60 Basi usiku huo nilijaribu kulala, nao...Niliamka, kitu fulani kama maji kilianguka. Basi damu ikatoka, karibu nusu galani, nakisia, ilitoka kwenye hizo vena. Nao walikuwa na... walipiga X-ray, nao wakasema ile risasi ilikuwa imekaa karibu sana na mshipa wa damu, pande zote mbili, hata mkwaruzo mdogo tu ungeukata moja kwa moja sehemu mbili, nami ningeanza kutokwa na damu. "Vema," nikawaza, "huu ndio mwisho wangu." Ndipo nikaweka mikono yangu chini namna *hii* na kuuinua, huku damu inatiririkia mikononi mwangu, nilikuwa nimelalia damu yangu mwenyewe. Nikaita, nikapiga kengele. Nesi akaja, naye akaipanguza tu kwa taulo kwa maana wasingeweza kufanya kitu.

61 Basi asubuhi yake, katika hizo hali za kudhoofisha, hawakuwekea damu siku hizo, mwajua, kwa hiyo wao—wao wakanifanyia upasuaji. Ndipo wakanipa nusukaputi. Nami

nilipo-...Ile nusukaputi ya kale, nadhani mnakumbuka, ilikuwa nusukaputi ya kale. Basi nilikuwa kwenye nusukaputi hiyo, nilipopata fahamu, nilikuwa ninatoka kwenye nusukaputi hiyo baada ya masaa manane. Iliwabidi kunipa nyingi sana, walifikiri nisingeweza—nisingeweza kuamka. Wasingeweza kuniamsha.

62 Ninakumbuka Bibi Roeder alisimama karibu nami, huko hospitalini. Sitamsahau mwanamke huyo kamwe. Hata kutukie nini, nisingeweza kamwe kumsahau. Yeye alikuwa tu ni mwanamke kijana wakati huo. Mumewe alikuwa msimamizi kule chini kwenye kiwanda cha motokaa. Nami na— namkumbuka akisimama karibu nami, yeye na Bibi Stewart. Nao ndio ambao kwa kweli walilipia gharama yangu ya hospitali. Mimi...Hatukuwa hata na chakula cha kula, nyumbani, kwa hiyo tungeliwezaje kugharimia gharama ya hospitali, mamia ya dolla? Lakini yeye, kupitia shirika la kanisa lake na Ku Klux Klan, wakalinilipia gharama ya hospitali, la Mason. Siwezi kamwe kuwasahau. Mnaona? Hata wafanye nini, ama cho chote kile, ningali...kuna kitu fulani, na jambo hilo nalikumbuka daima, mnaona, walichonifanyia. Nao wakalipa ile gharama kwa Daktari Reeder. Yeye angali anaishi, anaishi hapa katika Port Fulton, angeweza kuwasimulia hadithi hiyo.

63 Nilipotoka kwenye nusukaputi hiyo, kuna jambo fulani lililonipata pale. Daima nimeamini lilikuwa ni ono. Maana, nilikuwa nimedhoofika sana, nami...Wao walifikiri ninakufa. Bibi huyo alikuwa analia. Nilipoyafungua macho yangu kuangalia, niliweza kumsikia akizungumza, ndipo nikarudi usingizini, kisha nikaamka, mara mbili tatu. Halafu basi nikapata ono wakati huo. Na baadaye nilikuwa...

64 Yapata miezi saba baadaye, ilinibidi kwenda na kutolewa pamba kwenye jeraha za risasi na nguo za kuwindia zenye gilisi miguuni mwangu; yule daktari hakuzitoa. Na kwa hiyo damu ikapata sumu, miguu yote miwili ilikuwa imevimba na kukunjamana chini yangu, nao walitaka kuikata miguu yote miwili kwenye viweo vyangu. Nami tu...Nikasema, "La, sogeeni juu zaidi mkaikatie *hapa* juu." Hata nisingeweza kuvumilia jambo hilo, mnaona. Na kwa hiyo hatimaye, Daktari Reeder na Daktari Pirtle, kutoka Louisville, walinifanyia upasuaji, wakaikata mle ndani wakaitoa; na siku hizi nina miguu mizuri sana, kwa neema ya Mungu.

Lakini kwenye lile—lile ono la mwisho nililokuwa nalo...

65 Ono la kwanza, nilipojirudia, halafu nikaingia katika njozi hii. Nami nilifikiri nilikuwa kuzimuni, dhahiri tu...

66 [Ndugu fulani kwenye kusanyiko anasema, "Samahani, bwana."—Mh.] A-ha. ["Kuna mwanamke hapa ambaye amezirai, papo hapo."] Vema, mtu fulani na amwekee mikono, naye...

labda ampeleke kwenye hewa. Sasa ye yote anayesimama pale, weka mikono yako juu yake.

Na tuombe.

67 Mpendwa Bwana Yesu, naomba kwamba dada yetu ambaye ni mgonjwa asubuhi ya leo, na amezirai chumbani, neema Yako na nguvu na mamlaka . . . kuna mkono uliowekwa juu yake sasa, ukikuwakilisha Wewe. Nayo Maandiko yamesema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Na sasa naomba kwamba dada yetu atoke kwenye maradhi haya, na apate afya kwa utukufu wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba, na kumweka Kwako. Amina.

68 Sasa mtoeni kwenye hewa. Kuna—kuna msongamano sana. Ninaweza kuhisi hilo hapa, mbaya kweli, kweli. Unasikia tu kama kuzirai, hapa jukwaani. Nilikuhisi, mara nne ama tano hapa. Kama kuna . . . mara atakapojisikia vizuri zaidi, mbona, mpeleke mahali anapoweza kupata hewa. Hilo ni jema. A-ha. Mnaona, kuna msongamano sana, mwajua. Binadamu hutoa, kila mmoja wetu, futi nyingi za miraba za ugonjwa tu. Kama mna, mtu fulani ana maji pale, ama kitu fulani kummwagia huyo dada. Yeye—yeye atakuwa, ni mzima sasa. Mnaona? Vema. [Ndugu fulani katika kusanyiko anasema, "Tafadhali tufungue milango, Ndugu Branham."—Mh.] Naam, labda kama mngefungua milango, labda, ama kutoa hewa kidogo tu, nyingi tuwezayo, kwa njia fulani, mnaona.

69 Sasa katika wakati huu, kama nilivyokuwa na ono hili, na nikifikiri ya kwamba ni—nilikuwa nimepita kutoka maisha haya nikaingia katika mateso.

70 Basi miezi saba baadaye, hapa kwenye Hospitali ya Ukumbusho ya Clark County, nilifanyiwa upasuaji wa pili. Na wakati huo, nilipopata fahamu, nilidhani nilikuwa nimesimama Magharibi. Nikapata ono jingine. Basi kulikuwa na msalaba mkubwa wa dhahabu mbinguni, na Utukufu wa Bwana ukitiririka kutoka kwenye msalaba huo. Ndipo nikasimama huku nimetoa mikono yangu namna *hii*, nao Utukufu huo ulikuwa ukiangukia kwenye kifua changu. Nami . . . Lile ono likaniacha. Baba yangu alikuwa ameketi pale akinitazama, wakati hili ono lilipokuja.

71 Daima nimejisikia, ninyi . . . Watu wote ambao wamenijua miaka hii yote, wanajua daima nimetaka kwenda Magharibi. Mnajua jinsi jambo hilo lilivyo. Daima imekuwa kitu fulani kuelekea Magharibi. Lakini kwa sababu mamajusi mmoja aliniambia wakati mmoja, jambo lile lile, ya kwamba inanipasa kwenda magharibi . . . Nyota, wakati zinapovuka duara zao na kadhalika, nilizaliwa chini ya ishara hiyo, wala sitafanikiwa kamwe Mashariki; sina budi kwenda Magharibi. Basi mwaka uliopita nikaondoka nikaenda, Magharibi, kutimiza kile

kimekuwa hamu yangu maishani, mnaona, ku— kufanya jambo hilo.

72 Mbona mimi niko kule? Ni jambo la kuchekesha sana. Kuketi kule jangwani, nikilipa dolla mia moja na kumi kwa mwezi, malipo ya nyumba, na hii hapa nyumba imekaa hapa, nyumba ya mchungaji, nimepewa mimi, mnaona. Lakini ni kumfuata Bwana, mnaona, hilo—hilo ndilo lote nijualo kufanya. Nanyi mnajua yale maono na yale yaliyotendeka huko. Sasa—sasa katika jambo hili nataka kuwaambia . . .

73 Sasa kama dada yetu anasikia mdhaifu kidogo, Ndugu Roy, naye ange-. . . ukitaka kumtoa nje mahali fulani na kumweka chumbani huku, mahali anapoweza kupata hewa zaidi ama cho chote kile, basi hilo ni sawa kabisa, kwa sababu, naona kwamba atakuwa mzima sasa, mnaona. Ni sawa. Ana hali ya kuzirai tu, mgonjwa. Na kwa hiyo na—nawaambia, kama yeye . . . kama unataka kumleta hapa ambapo hewa . . . fungua madirisha haya, Ndugu Roy, na iwapo huyo dada anataka kupitia hapa, hilo—hilo litakuwa jema. Mnaona, kama yeye anataka ku—kuja hapa, vema, usiogope jambo hilo kamwe.

74 Ninataka kumwekelea mikono anapopita hapa. Nyote mniwie radhi kwa dakika moja tu. Na Mungu anisamehe kwa . . . Hilo, hilo ni sawa, ndugu.

75 Baba wa Mbinguni, huyu binti Wako hapa ameketi hapa asubuhi ya leo, naye amekuja kusikiliza Ujumbe, naye ana . . . Shetani anajaribu kukataza, lakini hawezi kufanya jambo hilo. Yeye hawezi kufanya jambo hilo. “Shetani hawezi, katika Jina la Yesu Kristo.”

Vema. Sawa, mlango ule, ninafikiri katika chache . . . ? . . . ndugu, halafu hewa inaweza kupitia hapa, kwenu.

76 Loo, mnazungumza juu kusongamana, mnapaswa kuingia katika baadhi ya nchi hizi za ng’ambo ambapo wao wanalundikana tu mmoja juu ya mwingine, wakiwa na ukoma na kansa. Na, loo, jamani, ni vigumu kupata hewa, wajua, katika vitu kama hivyo. Wanalala kwenye hayo majengo makubwa mno, wameambukizwa tu na—na magonjwa. Nanyi mnajua jinsi ukoma ungekuwa. Pale, wamelala pale bila maskio, na nusu ya uso wao umeliwa, hawana mikono, na vigingi vidogo badala ya miguu, na vitu kama hivyo, wamelala, wamelundikana mmoja juu ya mwingine. Na wengi wao wakifa wakati uo huo, wamelala kule nje, kutokana na kulundikana mmoja juu ya mwingine, wakijaribu kuingia ndani mahali fulani, mwajua, kusikia Ujumbe.

77 Basi sasa—sasa katika jambo hili, nawaambia kilichotukia. Katika lile ono nililopata, nitarudi nyuma, maana niliingiza hayo, hayo maono mawili, kuwaonyesha juu ya moja ya hayo. Ilikuwa niende huko Magharibi. Daima nimekuwa na shauku ya jambo hilo.

78 Basi sasa, kusudi la huu Ujumbe asubuhi ya leo ni kulijulisha kanisa, katika kila kitu ambacho ataniruhusu nilijulishe kanisa, kadiri nijuavyo mimi, mpaka ile... ninapoendelea. Basi hili lilinijia, kwa hiyo nilitaka kulijulisha kanisa. Naam, hii ni kwa ajili ya Maskani haya peke yake, mnaona, mahali hapa. Naam, basi katika ono hili, la kwanza, haya ndiyo yaliyotukia.

79 Basi baada ya hilo ono kunijia, nami nilikuwa mdhaifu sana, na nilikuwa nimepoteza damu hiyo yote, kisha nikaenda... nilifikiri ninatumbukia katika Umilele usio na mwisho. Wengi wenu mmenisikia nikisimulia jambo hili hapo kabla, huku—huku ninatumbukia katika Umilele usio na mwisho. Kwanza, nilikuwa nikipitia kwenye kitu kama mawingu, kisha katika giza, halafu nikazama chini, chini, chini. Basi muda si muda, nikafikia kwenye nchi ya waliopotea, ndipo mle ndani ni—nikalia kwa sauti kuu. Ndipo nikaangalia, na kule, kila kitu tu, hapakuwepo na msingi juu yake. Nisingeacha kuanguka. Ilivyoonekana, ningeendelea kuanguka Milele. Hapakuwepo na kikomo, mahali po pote.

80 Halafu basi ilikuwa ni tofauti jinsi gani na lile ono nililokuwa nimeona hapa, si muda mrefu uliopita, la kuwa Utukufuni pamoja na wale watu, ile tofauti! Lakini katika jambo hili, nilipokuwa ninaanguka, hatimaye, ni—nikamlilia baba yangu. Bila shaka, nikiwa mtoto tu, hilo ndilo ningefanya. Nikamwita baba yangu kwa nguvu, naye baba yangu hakuwa kule. Ndipo nikamlilia mama kwa nguvu, "Jamani mtu anishike!" Wala hakukuweko na mama kule. Nilikuwa ninaenda tu. Ndipo nikamlilia Mungu basi kwa sauti kuu. Hakukuweko na Mungu kule. Hakukuweko na kitu kule.

81 Ndipo baada ya kitambo kidogo nikasikia sauti ya maombolezi sana niliyopata kusikia, nako kulikuwa ni kujisikia kubaya sana. Hakuna njia...Hata moto wenyewe unaowaka ungekuwa ni faraja ukilinganisha na jinsi hali hii ilivyokuwa. Sasa maono hayo hayajakosea kamwe. Nako kulikuwa kumoja kwa kujisikia kubaya sana nilikowahi kujisikia, na kile...

82 Nikasikia kelele fulani, ilisikika kama namna fulani ya hali ya—ya—ya kuzuriwa na pepo. Basi wakati iliposikika, nikatazama, wakija, na ilikuwa ni wanawake. Nao walikuwa wamejipaka rangi ya kijani kibichi, ningeweza tu kuona nyuso zao, nao walikuwa na vitu vyenye rangi ya kijani kibichi chini ya macho yao. Na macho yao yalionekana kana kwamba yamerudi nyuma, kama vile wa—wanawake siku hizi wanavyoyapodoa macho yao, yakarudi nyuma namna *hiyo*, na ni macho yao tu na uso. Nao walikuwa wakisema "Uui, uui, uui, uui!" Loo, jamani!

83 Nililia tu kwa sauti kuu, "Ee Mungu, unirehemu. Unirehemu, Ee Mungu! Uko wapi? Kama tu utaniruhusu nirudi nikaishi, ninakuahidi, nitakuwa mvulana mzuri." Naam, hilo ndilo jambo pekee tu ningaliweza kusema. Naam, Mungu

anajua, na kwenye ile Siku ya Hukumu, Yeye atanihukumu kwa ajili ya tamshi hilo. Hivyo ndivyo nilivyosema, "Bwana Mungu, niruhusu nirudi, nami nitakuahidi Wewe nitakuwa mvulana mzuri."

84 Basi nilipopigwa risasi, nilikuwa nimesema uongo, nilikuwa nimefanya karibu kila kitu kinachoweza kufanywa, ni jambo moja tu ninalosema . . . Afadhali niliseme wazi wakati niko papa hapa sasa. Basi nilipoangalia kule chini na kuona nilikuwa nimelipuliwa nusu vipande viwili, karibu vipande viwili, nilisema, "Mungu, nirehemu. Unajua mimi kamwe sijatenda uzinzi." Hilo ndilo jambo moja ningaliweza kumwambia Mungu. Sikuwa nimekubali msamaha Wake kamwe, na mambo haya yote. Ninasema tu, ningeweza kusema, "Mimi sijatenda uzinzi kamwe."

85 Ndipo wao wakanitoa wakanipeleka kule nje. Halafu, katika jambo hilo, nikalia, "Mungu, nirehemu. Nitakuwa mvulana mzuri, iwapo tu utaniruhusu kurudi," kwa kuwa nilijua kulikuweko na Mungu mahali fulani. Na kwa hiyo nisaidie, hao viumbe wa kutaabisha walikuwa kila mahali, mimi nilikuwa mgeni aliyewasili hivi punde tu. Basi kujisikia kwenye kuchukiza kupindukia, kuogofya kupindukia, uovu mbaya kupindukia ambao . . . Ilionekana kama macho makubwa mno, kope kubwa zimetokeza namna *hiyo,* na zimerudi nyuma kama za paka, nyuma namna *hii*; na vitu vya rangi ya kijani kibichi, kama kwamba vilikuwa vimeoza ama cho chote kile. Nao walikuwa—walikuwa wanasema, "Uui, uui, uui!" Loo, ni kujisikia kulikoje! Basi wakati ni . . .

86 Basi katika dakika moja, nilikuwa nimerudi kwenye maisha ya kawaida. Jambo hilo limenisumbua mimi. Niliwaza, "Loo, hebu iwe kwamba sitaenda mahali kama hapo tena; pasitokee mwanadamu mwingine atakayelazimika kwenda mahali kama hapo."

87 Miezi saba baadaye, nilipata ono la kusimama kule Magharibi, na kuona msalaba ule wa dhahabu ukinishukia. Nami ni—nikajua ya kwamba kulikuwa na nchi ya waliolaaniwa mahali fulani.

88 Naam, sikuona jambo hilo sana mpaka yapata majuma manne yaliyopita. Mke wangu . . . Sikuliwazia jambo hilo kwa jinsi hii. Yapata majuma manne yaliyopita, mimi na mke wangu tulishuka kwenda Tucson, kununua bidhaa. Basi wakati tulipokuwa tumeketi . . . Mke wangu, tulishuka kuingia kwenye orofa ya chini, na—na kulikuweko na kundi la wavulana walioonekana kama dondoadume waliokuwa wamesokota nywele zao, mwajua, kama wanavyofanya wanawake, na—na kukatwa nywele mraba kwenye paji la uso, wamevalia hizi suruali ndefu walizopandisha juu sana, kwa namna fulani, nafikiri ni bitiniki, ama cho chote kile mnachoziita. Nao

walikuwa kule ndani, na kila mtu alikuwa anawaangalia, nazo nywele zao zikuwa kubwa *hivi*, kama wanawake wanaokata nywele zao mtindo wa "kichwamaji", mwajua. Nao walikuwa kule chini.

89 Ndipo kijana mwanamke akapita pale, naye akasema, "Unafikirije juu ya jambo hilo?"

90 Nikasema, "Basi unapaswa kujionea aibu, kama unaweza kuwazia jambo hilo." Nikasema, "Yeye ana haki ya kutosha kufanya jambo hilo kama ulivyo nayo wewe. Hakuna hata mmoja wenu aliye na haki."

91 Kwa hiyo nikaenda kwenye orofa ya juu, na nikaketi chini. Basi nilipofanya hivyo, kulikuwa na kipandio, ilikuwa ni duka kubwa la J.C. Penny, nacho hicho kipandio kikiwapandisha watu. Vema, kweli nilichefuka tumboni mwangu, kuona hao wanawake wakipanda kuja kule; vijana, wazee, na wasiojali, wenye makunyanzi, vijana, na kwa kila njia, wamevalia vikaptura vidogo; miili yao najisi, na hao wanawake waliovalia kizinifu, wakiwa na nywele hizo kubwa mno namna hiyo, basi hawa hapa wanakuja. Basi mmoja anakuja moja kwa moja kutoka kwenye kipandio hicho, akija tu moja kwa moja namna hiyo, mahali nilipokuwa nimeketi kule nyuma kitini, nimeketi kule huku nimeinamisha kichwa changu.

92 Ndipo nikageuka nikaangalia. Na mmoja wao alipokuwa anakuja kwenye vile vipandio alikuwa anasema, "Uui," akizungumza Kihispania, na mwanamke mwingine. Yeye alikuwa mwanamke mzungu akizungumza na mwanamke Mhispania. Basi nilipotazama, [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.], mara moja nilibadilishwa. Pale, nilikuwa nimeona jambo hilo hapo awali. Macho yake, mnajua vile ambavyo wanawake wanafanya siku hizi, kupodoa macho yao, hivi majuzi tu, kama paka, mnajua wanajipaka juu namna *hii*, huku wanavaa miwani ya paka na kila kitu, mnajua, huku macho yao yako *hivi*, na kitu kile cha kijani kibichi chini ya macho yao. Hicho hapo kile kitu nilichoona nilipokuwa mtoto. [Ndugu Branham anapiga mimbara mara kadha.] Huyo hapo yule mwanamke vile vile ilivyokuwa kabisa. Nami nikafa ganzi mwili mzima, kisha nikaanza kuangalia kila mahali, na palikuwepo na watu wale wakinong'oneza, mwajua, wakiongea juu ya bei na kadhalika katika lile jengo. Nami nikanini-hii tu. . .

93 Ilionekana kana kwamba nilibadilika tu kwa dakika moja. Ndipo nikaangalia, nikawaza, "Hayo ndiyo niliyoona kuzimu." Hao hapo, kuoza kule. Nilifikiri kilichowafanya wawe namna hiyo ni kwa kuwa walikuwa kuzimu, kitu fulani cha kijani kibichi na samawati chini ya macho yao. Basi hawa hapa wanawake hao wamejipodoa kwa rangi ya kijani kibichi na

samawati, jinsi ile ile ono lile lilivyosema mnamo miaka arobaini iliyopita.

94 Mnaona, yapata miaka arobaini iliyopita, ndivyo ilivyokuwa. Mimi nina umri wa miaka hamsini na minne; nilikuwa na kumi na minne. Kwa hiyo ni yapata miaka arobaini iliyopita, mimi . . . Na jambo hilo ndilo—ndilo . . . Hiyo ndiyo nambari, hata hivyo, ya hukumu, mnaona. Sasa kulikuwa . . .

95 Nilikuwa nimeona jambo hilo na hata sikuweza kuzungumza na mke wangu wakati alipokuja. Yeye alikuwa kule akijaribu kumnunulia Sara na hao watoto kitu fulani, namna fulani ya—ya nguo ama cho chote kile kwa ajili ya shule, nami—nami hata nisinge- . . . Hata nisingeweza kuzungumza naye. Akasema, "Bill, una nini?"

Nikasema, "Mpenzi, mimi ni kama . . . Mimi ni kama mtu aliyekufa."

Naye akasema, "Kuna nini? U mgonjwa?"

Nikasema, "La. Kitu fulani ndiyo kwanza kitendeke."

96 Sasa yeye hajui. Yeye anangojea kanda hii irudi. Sijapata kumwambia mtu ye yote jambo hilo. Nami nilifikiri afadhali ningojee, kama nilivyoahidi, kulileta kanisani kwanza. Mnaona? Kulileta kanisani. Hiyo ilikuwa ni ahadi yangu. Nanyi mtatambua, baada ya usiku wa leo, sababu ya mimi kujaribu kutimiza ahadi yangu. Mnaona?

97 Niliwaza wakati huo, nilipoyatazama hayo macho yanayoonekana yameoza ya wanawake hao. Kulikuweko na Wahispania, Wafaransa, na Wahindi, na watu weupe, na wote pamoja, lakini hizo nywele kubwa mno, mwajua, zilizochanuliwa, na vichanuo hivyo, jinsi wanavyozilaza kwa nyuma, kubwa mno, kisha zinatokeza nje. Mwajua, mnajua jinsi wanavyofanya jambo hilo, kuzitengeneza kama wanavyofanya. Halafu macho hayo yanayoonekana kana kwamba yameoza, na yale macho yaliyopodolewa, yanayorudi nyuma kama macho ya paka. Nao wakizungumza, nami huyo pale tena, nikisimama pale katika duka kubwa la J.C. Penney, nimerudi kuzimuni tena.

98 Ni—ni—niliogopa sana. Nikawaza, "Bwana, hakika sikufa, Nawe umeniacha kuja mahali hapa hata hivyo."

99 Basi hao hapo, wakifanya . . . wanazunguka namna hiyo, kama vile katika ono lile, ilikuwa tu ni vigumu kusikia kwa maskio yako, mwajua. Kunong'ona tu na kuendelea, kwa watu, na hao wanawake wakipanda kwa kipandio hicho na kwenda kila mahali pale, na ile "Uui, uui!" Hayo hapo macho ya kijani kibichi, ya ajabuajabu, na ya maombolezo.

100 Ndipo mke wangu alipokuja. Nami nikasema, "Niache tu peke yangu kidogo, mpenzi." Nikasema, "Kama ni sawa kwako, na—na—nataka kwenda nyumbani."

Naye akasema, “Unaumwa?”

101 Nikasema, “Hapana, endelea tu, mpenzi, kama unataka kununua bidhaa zo zote.”

Yeye akasema, “Hapana, nimemaliza.”

102 Basi nikasema, “Hebu nikushike mkono.” Mnaona? Ndipo nikatoka.

Yeye akasema, “Kuna nini?”

Nikasema, “Meda, Mi—mi—mimi . . . Jambo fulani lilitukia juu kule.”

103 Basi nilipokuwa kwenye jambo hilo, niliwaza jambo hili, “Tunaishi katika siku gani? Hivi huu ungeweza kuwa ndio ule Mvuto wa Tatu?” Sasa nina muhtasari mdogo hapa.

104 Yesu. Tunaona ya kwamba, Yesu, katika huduma Yake, baada ya Yeye kuwahubiri watu. Sasa tutakuwa wa Kimaandiko kabisa juu ya jambo hili. Baada ya Yesu kumaliza huduma Yake, na huduma Yake ikakataliwa na watu. Sasa mtasoma katikati ya mistari, pateni ufafanuzi wenu wenyewe. Kumbukeni nilichowaambia hapo kwanza. Baada ya Yeye kuhubiri . . .

105 Yeye alikuja kama Yule aliyeahidiwa kwa ajili ya siku hiyo. Sote tunajua jambo hilo. Maandiko yalimtambulisha Yesu kama Masihi. Hiyo ni kweli. Kinaganaga, kwa uthabiti, alithibitishwa na Mungu pamoja na Neno Lake, ya kwamba alikuwa Masihi. Hakuna swali. Kama mtu ye yote akihoji jambo hilo, kama ukifanya hivyo, basi inakubidi kuja madhabahuni, ya kwamba, “Yeye hakuwa Masihi.” Yeye alitambulishwa dhahiri kama Masihi. Lakini baada ya Yeye kabisa . . . Mungu alimthibitisha.

106 Kama Petro alivyosema Siku ya Pentekoste, alipozungumza na wale Wazee pale, kwenye nini-hii nne . . . yapata siku nnne baadaye. Yeye alisema, “Yesu wa Nazareti, Mtu aliyethibitishwa kwenu na Mungu kwa ishara na maajabu, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono Wake kati yenu, ambazo sisi sote tu mashahidi wake. Mnaona? Mmemchukua, kwa mikono ya watu wabaya, na kumsulubisha Mfalme wa Amani; ambaye Mungu amemfufua, na kuwaonyesha mambo haya ambayo mmeyaona.” Mnaona? Kristo aliendelea kuishi. Bila shaka, yungali anaishi leo.

107 Sasa baada ya Yesu kuja hasa, akajitambulisha Mwenyewe; Mungu alimtambulisha Yeye, Naye akatabiri. Na baada ya siku za unabii Wake, ingawa alitambulishwa Kimaandiko, watu walimkataa. Hiyo ni kweli. Ndipo akahubiri basi baada ya wao kumkataa hapa, wale waliokuwa na uwezekano wa kuokolewa. Kumbukeni, alipokuwa anahubiri, kulikuweko na uwezekano wa mtu ye yote kuokolewa. Hatujui hao ni nani. Wao wamechanguliwa tangu awali. Bali Yeye aliendelea kuhubiri.

108 Lakini baada ya siku za kuhubiri Kwake, huduma Yake iliendelea, maana kundi la mwisho alilolihubiri lilikuwa

nafsi ziliokuwa kuzimuni, ambazo zisingeweza kusamehewa. Nimesoma jambo hilo dhahiri kutoka kwenye Biblia hapa, kutoka Petro wa Pili. Mnaona? Yeye alienda akazihubiri nafsi zilizokuwa kifungoni, ambacho ni kuzimu, zimefungwa mle hata kwenye ile Siku ya Hukumu.

109 Maana, mnaona, Hukumu si sasa, wala hakuna kuzimu kunakowaka moto sasa. Mtu fulani akikwambia, "Jamaa huyo yuko katika kuzimu kunakowaka moto sasa," hilo ni kosa. Mnaona? Hakimu wa ulimwengu ana haki vya kutosha kutomhukumu mtu mpaka ameletwa hukumuni. Wala Mungu kamwe hatamtupa mtu katika ile—ile tanuru inayowaka moto mpaka kwanza amehukumiwa kwa sheria za Mungu Mwenyewe. Alikataa rehema, kwa hiyo, mnaona, kwanza hana budi kuhukumiwa, nayo mahakama ni ile Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi. Bali sasa yuko mahali panapoitwa gereza.

110 Kama nilivyoona ono la mahali pote pawili, na kwa neema ya Mungu. . . Nasema jambo hili sio kwa kukufuru, na, kama ni kosa, Mungu anisamehe. Ninaamini nimekuwa mahali pote pawili, mnaona, mahali hapo pawili. Nami nimewaona waliokombolewa, waliobarikiwa; na nimeona waliopotea, na mahali walipokuwa. Na hiyo ndiyo sababu ninasimama kama ndugu yenu, leo, kuwaonya kuikimbia njia hiyo ya mtelemko. Kamwe usiende kwenye barabara hiyo. Nawe una kila kitu cha kuishia, ile njia iliyobarikiwa ya kwenda juu, mahali ambapo waliokombolewa wako katika raha na amani, wala hawawezi kufanya dhambi. Hawawezi—hawawezi kupata majonzi. Hawawezi. Hakuna, hakuna kitu; wao ni wakamilifu. Nimekwisha kuona mahali pote pawili! Ninajua hilo ni tamshi zito sana kwa mtu kutamka, lakini, Mungu akiwa Hakimu wangu, ninaamini kwa uchaji nimeona mahali pote pawili. Ni—ninaamini jambo hilo.

111 Na, lo, na iwe mbali na mtu ye yote kuingia kwenye hiyo nchi ya waliopotea! Kama ulikuwa umesimama huku umechomwa waya zenye moto, ukiteswa kwa kila hali, isingekuwa kama mateso hayo ya ibilisi yaliyo mahali pale. Kusingekuwa na kitu . . . akili ya mwanadamu, akili ya mwanadamu isingefahamu jinsi nchi hiyo ya waliopotea ilivyo. Hakuna njia ya kulielezea jambo hilo. Wala hakuna njia ya kueleza jinsi nchi ya waliobarikiwa ilivyo, ni nzuri sana. Hiyo ni ya kutisha sana, nayo Hii ni—ni kuu sana, ni kutoka kwenye ya kuchukiza hadi yenye fahari sana. Kwa hiyo kama mtu ye yote ananisikia . . .

112 Nami ninakuwa mzee. Sijui nina muda gani zaidi. Hivi karibuni nitakuwa na umri wa miaka hamsini na mitano. Nami si—sijui, kulingana na maumbile, huenda nisiwe na miaka mingi sana. Sijui mahali hii kanda itakapokwenda. Lakini hebu kila mtu asikie, hapa na kwenye kanda, ama po pote inapoweza kwenda. Usielekee kamwe kwenye nchi hiyo ya waliopotea. Huwezi kuwazia kuzimu kukiwa kubaya namna hiyo. Na lo lote

ufanyalo, usithubutu kamwe kupata nini-hii. . .kusahau hili, ya kwamba nchi ya waliobarikiwa. . . Ningesema jambo hili, pamoja na Mtakatifu Paulo, "Jicho halijaona, sikio halijasikia, wala haingeweza kuingia moyo wa mwanadamu, kile Mungu amewawekea akiba hao wampendao Yeye." Kwa hiyo komea hapa, kama unasikiliza kanda, zima kinasasauti, kisha utubu kama wewe hujaokolewa, halafu jiweke sawa kwa Mungu.

113 Ninasema jambo hili kwa tukio la kibinafsi, kama ninavyoamini katika moyo wangu. Nami nasema, kama haya, kama maono haya yamenidanganya, Mungu na anirehemu kwa kufanya tamshi kama hilo. Bali kwa uaminifu moyoni mwangu, nikijua ya kwamba hakuna moja la hayo maono lililopata kushindwa, ninaamini ya kwamba nimekuwa mahali pote pawili. Na iwe mbali na mwanadamu ye yote kupitia barabara hiyo ya mtelemko!

114 Naam, Yesu, baada ya Yeye kumaliza huduma Yake, akazihubiri nafsi hizo zisizoweza kuokolewa, ambazo hazingeweza kamwe kuokolewa. Sasa Biblia inatwambia jambo hilo. "Yeye aliienda akazihubiri nafsi zilizokuwa kifungoni, ambazo hazikutubu." Wakati zilipopewa rehema, nazo ziliikataa neema, basi sasa hizo zinaingoja ile Hukumu. Loo, ulikuwa wakati wa namna gani! Loo, laiti kungalikuwa na njia ningeweza kuutikisa ulimwengu kwa jambo hilo, kuwafanya waone ukweli ulivyo.

115 Naye Yesu alisema, Mwenyewe, "Kama Baba alivyonipeleka Mimi, nami nawapeleka." Basi kama Baba alivyompeleka kuwahubiri wa—walio hai, kwa wale waliokuwa na matumaini, kisha apeleke Ujumbe ule ule kwa wale wasiokuwa na matumaini, inaonekana ni jambo jema, kwenye wakati huu, kwamba jambo hilo litapaswa kufanyika, maana Roho wa Kristo anayeishi ndani yetu habadilishi tabia Yake, ama habadilishi taratibu ya Mungu. Hana budi kuwa ni yeye yule katika kila kizazi. Hana budi kuwa ni yeye yule. Kasema, "Kama Baba alivyonipeleka Mimi, mimi nami nawapeleka."

116 Zile huduma hazina budi kuwa zile zile, kwa kuwa Yeye alisema. . .Ninaona wengine wenu wakiandika Maandiko. Yohana Mtakatifu 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Mnaona, "zile kazi," kuwahubiri waliopotea, kuponya wagonjwa, halafu kwa wasioweza kuokolewa. Mnaona? Kazi iliendelea vile vile. Kwa hiyo, jambo hili limekuwa, (limekuwa?) naomba niliweke namna hii, huduma ya Yesu Kristo ikifanyika mwili katika Kanisa Lake katika siku hizi za mwisho. Hivyo ndivyo wengi wetu wanavyoamini. Ninaamini pamoja nanyi. Ninaamini jambo hili. Kama nisingaliliamini, ningefanya jambo jingine kuhusu jambo hilo. Kwa sababu, hata hivyo, huyo ni mimi ninayehusi-. . . ninayehusika hapa. Na kama Roho ya Mungu ikiwa ndani yako, unahusika juu ya watu.

117 Kulikuwa na Andiko lililonitatiza daima, jinsi ambavyo Musa angemwambia Mungu wazo zuri zaidi kuliko alilokuwa nalo Mungu, mpaka nikapata kujua kwamba ilikuwa ni Roho wa Kristo ndani ya Musa. Mnaona?

118 Mungu alisema, "Musa, jitenge nao. Nitaangamiza kitu hicho chote, halafu nianze nawe."

119 Akasema, "Bwana!" Akajitupa mwenyewe katika pengo, kasema, "Nichukue mimi. Lifutilie mbali jina langu." Juu ya watu wawa hawa waliokuwa wameasi, moyo wake uliwahurumia. Mnaona?

120 Basi wakati mhudumu anayewahurumia watu... Ningewezaje kamwe kujisikia nimehesabiwa haki kwa nini-hii yangu...mbele za Mungu, na kwangu mimi mwenyewe, kuwaficha jambo lo lote watu unaowapenda kuliko unavyojipenda mwenyewe. Mtu angewezaje kumwingiza mtu kanisani kwa kujiunga kwa mkono, ama kunyunyizia fulani, ama ubatizo fulani wa uongo, ama cho chote kile, kisha awaache wakae chini ya—ya ushawishi wa uongo fulani na akijua ya kwamba Biblia iko pale, halafu aseme ati anampenda huyo mtu?

121 Ingawa inanibidi kuomba riziki yangu, cho chote kile, hebu niwe mwaminifu kwa Mungu na kwa watu, kuwaambia Kweli. Kamwe usiniruhusu niwe mdanganyifu. Ninawezaje kuwadanganya hao niwapendao? Ingawa inanibidi kuwaudhi, hata hivyo ninawapenda. Hiyo ndiyo sababu unampiga mtoto wako, ni kwa sababu unampenda. Si kwa sababu humpendi; kwa sababu unampenda. Kama amekosea, yeye atauawa kama hutamsahihisha.

122 Naam, vivyo hivyo ndivyo huduma imekuwa. Kama ilivyokuwa, ndivyo ilivyo leo. Imehubiriwa, na kuthibitishwa kwelikweli kwa Neno la Mungu, ya kwamba isingekuwa ni mwanadamu, haina budi kuwa ni Mungu. Haina budi kuwa. Angalia, ishara zile zile za kiroho alizozifanya Yesu, zimetukia tena duniani katika siku za mwisho. Ishara zile zile za kiroho ambazo alijitambulisha Mwenyewe kama Masihi, zimemtambulisha leo. Yeye yungali ni Masihi! Ishara zile zile za kuonekana dhahiri kimwili zimetukia duniani, ambazo zilitukia Kwake, kile alichokuwa Yeye. Nguzo ile ile ya Moto aliyoiona Mtakatifu Paulo, ile ile, yote hayo yametukia yakiwa na tabia ile ile ndani yake, yakifanya jambo lile lile.

123 Yesu alidai ya kwamba Yeye hajafanya kitu mpaka Baba alipomwonyesha. Naye Baba ni Roho Mtakatifu, tunatambua jambo hilo. Ni ofisi tu ya Mungu. Kama sivyo ilivyo, basi ni yupi kati yao aliye Baba ya Yesu Kristo? Yesu alisema Mungu alikuwa ndiye Baba Yake, nayo Biblia ilisema Roho Mtakatifu alikuwa Baba Yake. Naam, huwezi kumfanya awe mwana haramu, kwa hiyo Roho Mtakatifu ni Mungu, kwa hiyo Yesu alikuwa Mungu.

Kwa hiyo, Mungu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni...Ni nini hii...Hivyo ni ofisi tatu za Mungu mmoja. Ni sifa tatu, Mungu yule yule.

124 Wewe ni sehemu ya Mungu, nami ni sehemu ya Mungu, unaona; lakini mimi si Mungu mzima, wala wewe si Mungu mzima. Unaona? Unaona? Ni sifa za Mungu juu yetu, kama wana waliofanywa wana na Yesu Kristo. Ambapo, Mungu Mwenyewe alifanyika mwili, apate kufa kwa ajili yetu.

125 Naam, Roho Mtakatifu daima alimwonyesha mambo yajayo, naye hakukosea kamwe. Ilikuwa kamilifu daima. Sivyo? Yeye hakujisifu Mwenyewe. Alimsifu Mungu. Alisema, "Mwana hawezi kufanya neno kwa nafsi Yake bali lile analomwona Baba akifanya hilo." Naye Baba, Roho Mtakatifu, alikuwa Baba Yake. Hiyo ni kweli? "Yusufu, ewe mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mke wako, kwa maana mimba yake ni ya Roho Mtakatifu," ambaye alikuwa ndiye Baba Yake. Naye Roho Mtakatifu alimwonyesha Yesu mambo yajayo, akamwambia mambo yaliyokuweko.

126 Naye alikuwa ndiye yule Mungu-Nabii. Kwa sababu, Neno la Bwana daima huja tu kwa nabii; ikionyesha ya kwamba Maneno yalikuja, katika hali ya chini, manabii waliandika kile alichowaambia Bwana. Bali hakuandika kitu, kwa maana Yeye alikuwa Neno. Alikuwa Neno.

127 Angalia, Roho Mtakatifu yule yule aliyeishi ndani Yake, "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; lakini ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Nitakuja kwenu," Yeye alisema. "Mimi," alikuwa Baba aliyekuwa ndani Yake, "atakayekuja kwenu." Naye alisema, "Roho Mtakatifu akisha kuja juu yenu, atawafunulia mambo haya ambayo nimewafundisha, na mambo yajayo atawapasha habari zake." Haya basi.

128 Sasa tunaona, ya kwamba Roho Mtakatifu alipofanya kazi Kanisani wakati huo, vivyo hivyo Roho Mtakatifu amefanya mambo yale yale kabisa leo; akitangaza kwa ile Nguzo ya Moto, kama tu vile ilivyokuwa hapo mwanzo hasa, jambo lile lile. Basi alipoona kitu hiki kikimjilia Yesu, Yohana alitangaza jambo hilo kwenye mto Yordani. Na amethibitisha kila kitu, hata picha zake za kisayansi. Hakiwezi kukanushwa. Kilithibitishwa kisayansi. Kilikuwa kitu dhahiri. Halikuwa wazo la kubuniwa. Haikuwa saikolojia. Kama alivyosema George J. Lacy, "Jicho la kimitambo la kamera halitapiga picha saikolojia. Ile Nuru iligusa lenzi."

129 Vipi kuhusu ninyi, enyi kanisa, ambao yapata miezi sita ama minane iliyopita hapa, nikisimama hapa, nikisema, "Ni BWANA ASEMA HIVI, ya kwamba ninaenda Tucson, Arizona. Kutakuweko na mlipuko, Malaika saba watatokea." Mnakumbuka? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Wala

hata . . . Mungu akilifanya jambo hilo halisi sana hata gazeti la *Look* likalipiga picha. Kiroho, nililiona kabla, likaonekana vile vile kabisa, wale Malaika saba, ambao walileta kumaliziwa kwa Maandiko yote. Maana, siri zote za Biblia nzima zimo kwenye zile Muhuri Saba. Tunajua ya kwamba hicho ni Ki— Kitabu, Muhuri Yake, pamoja na Kitu hicho kimekamilishwa. Ni siri za Kitabu kizima, zimewekwa katika Mihuri hiyo Saba, ambayo Bwana alituruhusu kuileta.

130 Na kuna mtu anayeketi hapa, leo, aliyekuweko pale pamoja nami wakati jambo hilo lilipotukia. Gazeti la *Look* lilithibitisha jambo lile lile, ya kwamba li—lilitukia kweli. Kwa maana, Mungu ndiye aliyesema jambo hilo. Alikuwa ni Mungu ambaye husimama nyuma ya Neno Lake, kulitimiza anaposema atalitenda. Kwa hiyo, si mtu fulani, mtu wa kimwili kama mimi mwenyewe, ambaye yuko kati yenu enyi watu. Ni Mungu wa Milele.

131 Yeye humtumia mwanadamu. Hiyo ni kweli. Yeye hafanyi kitu nje ya jambo lile analofanya akimtumia mwanadamu. Tunatambua jambo hilo. Yeye, huyo ni—huyo ndiye mjumbe Wake. Huyo ndiye Yeye aliyemchagua. Sababu yake, sijui. Yeye angalilifanya jua kuhubiri Injili. Angeweza kufanya upepo uhubiri Injili. Angeufanya upepo ufanye mambo, lakini alimchagua mwanadamu.

132 Hilo lilikuwa ni wazo Lake, kwamba mwanadamu angezungumza na mwanadamu; si mwenyewe, bali, "Neno la Mungu liliwajia manabii," watabiri, wahubiri. Basi mtabiri anayelikana Neno la asili, anawezaje kuwa nabii wa kweli? Mnaona? Hawezi kuwa, kwa maana yeye anaikana Kweli ya Neno. Halafu kama sivyo, basi Neno hili, Lenyewe, kama likihubiriwa kwa kweli ya Neno na kwa kweli ya Roho Mtakatifu, litadhihirisha kila ahadi lililoahidi. Hivyo ndivyo tunavyojua kama ni kweli ama si kweli. Hivyo ndivyo alivyosema Yesu, "Kama sifanyi yale niliyoandikiwa kwamba Mimi nitafanya, basi msiniamini." Mnaona? Sasa tunaona mambo haya.

133 Kumbukeni, zile Muhuri Saba zilimalizwa, na wakati zile Kweli saba zilizofunuliwa . . .

134 Moja ya hizo, Yeye asingeturuhusu kujua. Sisi . . . Ni wangapi waliokuwa hapa kwenye zile Muhuri Saba, na kusikia? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Ninyi nyote, nafikiri. Mnaona, ile—ile Muhuri ya Saba, asingeiruhusu.

135 Yeye alisimama pale pale chumbani na kufunua kila moja ya hizo. Na kama nilipata kuhubiri jambo lo lote maishani mwangu, lililokuwa limevuviwa, lilikuwa hilo. Nalo halina budi kuwa ni kweli, kwenu. Kasimama hapa na kawaambia ya kwamba litatukia, kisha kwenda moja kwa moja kule, na hata sayansi na cho chote kile, utafiti wa sayansi na kila kitu, siri kwa watu,

ulithibitisha ya kwamba lilitukia pale pale. Kisha tunarudi moja kwa moja na kulisikia likifunuliwa, na kulifanya kila Neno kweli kabisa. Tunaishi katika siku gani? Tuko wapi?

136 Basi kumbukeni, katika hiyo Muhuri ya Sita, ambapo, Baragumu zote zinalia katika Muhuri ya Sita. Tutakapoufikia, mtaona jambo hilo. Kila (saba) Baragumu ilitukia katika Muhuri hiyo ya Sita.

137 Saba daima ni siri. Angalia hiyo saba, hiyo ni kumalizia. Hiyo ilikuwa ni kule Kuja kwa Bwana. Mbingu zilitulia, zilikuwa kimya, hakuna mtu aliyesogea. Kwa maana, Yesu alisema Mwenyewe, "Hata Malaika wa Mbinguni hajui wakati nitakaporudi. Wala Mimi hata sijui, Mimi Mwenyewe, ni wakati gani. Baba ameweka jambo hilo moyoni Mwake." Mungu peke Yake anajua, Roho. Kasema, "Mimi sikuijua." Halafu, haukufunuliwa. Wakati hiyo Baragumu ya Saba ilipotoa sauti . . . ama yule Malaika wa Saba, Mu—Muhuri ilifunguliwa, kisha ikawa kimya Mbinguni. Mnaona, haikuelezwa, kile kingetukia.

138 Lakini kwenye ile Muhuri ya Sita, mahali ambapo Baragumu hizi zilifunguliwa. Kumbukeni, kwenye huo, tunaona ya kwamba Mwana-Kondoo alikuja, akajitokeza hadharani. Yeye alikuwa ameondoka kwenye Kiti cha Rehema. Kazi Yake ya Ukombozi ilikuwa imekwisha. Ndipo akaja akakitwaa kile Kitabu kwenye mkono wa kuume wa Yeye aliyeketi kwenye Kiti cha Enzi, na "hakukuwa na wakati baada ya hayo." Ndipo mara moja malaika akatokea katika sura ya saba, ama sura ya 10 na aya ya 7, akisema . . . Malaika huyu alishuka akaapa, kwamba, "hapana wakati tena."

139 Lakini, mnaona, ndani ya Kitabu hiki mlikuwemo na kile kilichokombolewa. Kilikuwa ni Kitabu cha Ukombozi. Na kila kitu alichokuwa amekomboa kilikuwa kimeandikwa katika Kitabu hicho. Na yote aliyofia yalikuwa yameandikwa katika kile Kitabu, wala Yeye hangeweza kuondoka kwenye Kiti Chake cha maombezi mpaka Yeye amekomboa kabisa. Wala Yeye asingeweza kukikomboa pale msalabani, kwa maana wao walichaguliwa tangu awali katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, naye ilimbidi kukaa Mle kufanya maombezi hata mtu yule wa mwisho amekwisha. Utukufu!

140 Lakini siku moja akainuka kutoka Kule, akaja. Kile Kitabu kilikuwa wapi? Kilikuwa bado kiko kwa Mwenyewe asiyeonekana, Mwenyezi Mungu. Ndipo Yohana akaangalia kila mahali, kisha akalia, kwa maana hapakuwepo na mtu aliyekuwa anastahili hata kukiangalia kile Kitabu na, hasa sana, kuzifungua zile Muhuri, kufunua ile siri iliyofichwa ni nini.

141 Zile siri zilikuwa katika zile Muhuri Saba. Wakati hizi Muhuri Saba zilipofunguliwa, hilo lilifungua Biblia nzima. Zile Muhuri Saba; kilikuwa kimetiwa muhuri kwa Siri Saba, na

katika hizi Muhuri Saba kulikuwemo na siri Yake yote. Nacho kilikuwa Kitabu cha Ukombozi, Agano Jipya.

142 Si la Kale. Lilitangaza tu Agano Jipya. "Wao wamefanywa . . . hawawezi kukamilishwa pasipo sisi," Waebrania 11. Mnaona? Mnaona? Naam, ukombozi ulikuja tu wakati yule Mkombozi alipokufa. Nao walikuwa kwa uwezekano chini ya damu ya wana-kondoo, si Mkombozi; wao hawakuwa wamekombolewa bado, mpaka yule Mkombozi alipokuja.

143 Angalieni sasa wakati Mkombozi huyu . . . Yohana aliangalia kila mahali, naye huyu hapa Mungu ameketi kwenye Kiti cha Enzi, ameshika kile Kitabu katika mkono Wake, ambacho kilikuwa kimetiwa muhuri kwa Mihuri Saba, na mpango wote wa ukombozi ulikuwa ndani yake.

144 Nacho kilikuwa kimepotezwa na jamii ya binadamu, Adamu. Ndipo Mungu . . . Kilirudi wapi? Shetani asingeweza kukichukua; yeye alimsababisha tu akipoteze. Lakini hicho Kitabu kilienda wapi basi? Hakikuwa mali ya jamii ya binadamu. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha—Mh.] Zile baraka hazikuwa za pale; hapa jamii ya binadamu ilikuwa imekipoteza. Kwa hiyo kilirudi moja kwa moja kwa Mwenyewe wa asili, huyo alikuwa ni Mungu.

145 Huyu hapa ameketi Nacho, ndipo akaita mtu fulani, mtu mmoja, aje akidai Hicho.

146 Yohana akaangalia kila mahali, wala hapakuwepo na mtu Mbinguni, wala mtu duniani, hamna mtu, hakuna Malaika, hakuna kitu kingaliweza kukichukua kile Kitabu wala kuzifungua zile Muhuri, wala hata kukitazama. Hakuna mtu aliyestahili. Yohana alisema alilia kwa uchungu.

147 Ndipo Malaika akamjia, kasema, "Usilie, Yohana, kwa maana Simba wa kabila la Yuda ameshida, Naye anastahili. "

148 Ndipo Yohana akaangalia apate kumwona mwana-kondoo . . . ama kuona simba, naye aliona kitu gani? Mwana-Kondoo, naye alikuwa Mwana-Kondoo aliyejaa Damu, Mwana-Kondoo aliyekuwa amechinjwa. Kwa muda gani? Tangu kuwekwa misingi ya dunia.

149 Yule Mwana-Kondoo akaja, akaenda moja kwa moja kwa yule aliyekuwa na kile Kitabu katika mkono Wake wa kuume, akakipokea kile Kitabu; akapanda kwenye Kiti cha Enzi akaketi. Haya basi. Ilikuwa imekwisha (lini?) wakati zile Muhuri zilipofunuliwa. Wakati yule wa mwisho, hayo yalikuwa ndiyo kila kitu alichokuwa amekomboa, hapakuwepo na kitu . . .

Alikuja kukomboa.

150 Kasema, "Kwa nini Yeye hakuwakomboa miaka arobaini iliyokwisha? Miaka elfu mbili iliyokwisha?"

151 Mnaona, majina yao yako kwenye Kitabu cha Uzima, kwenye hicho Kitabu. Naye ilimbidi kusimama hapa, kwa maana ilikuwa ni kusudi la Mungu kuwakomboa. Majina yao yaliandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mwana-Kondoo aliwekwa kule pamoja nacho, apate kuuawa. Huyu hapa Mwana-Kondoo anakuja, alipochinjwa, akarudi kufanya maombezi.

152 Mwangalie! Kutakuwa na kuiga kwingi sana, wingi wa cho chote kile, bali kulikuwa hasa na mtu ambaye angeokolewa, kwa kuwa Yeye. . . Kanisa lilichaguliwa tangu awali kuwa lisilo na waa wala kunyanzi. Litakuwepo. Naye Mwana-Kondoo alikufa kwa ajili hiyo. Halafu tena wakati lile jina la mwisho katika kile Kitabu lilipokombolewa, Mwana-Kondoo alitokea akakichukua kile Kitabu, "Mimi Ndimi niliyefanya jambo hili!"

153 Wale Malaika, Makerubi, wale Wazee ishirini na wanne, wale Wenye Uhai, kila kitu, walijivua taji wenyewe, wakaanguka mbele ya Kiti cha Enzi, wakasema, "Umestahili!"

154 Yohana akasema, "Kila kitu Mbinguni na duniani kilinisikia mimi nikipiga makelele, 'Amina,' nikipaza sauti, 'Haleluya,' na sifa kwa Mungu. Makelele yakapigwa. Kwa nini? Majina yao yalikuwa kwenye Kitabu kile, kufunuliwa, naye Mwana-Kondoo alikuwa amefunua jambo hilo.

155 Mwana-Kondoo alikuwa amekikomboa, bali hangeweza kuja mpaka kila jina limefunuliwa, na jambo hilo lilikuwa likitendeka chini ya Muhuri ya Sita, kabla ile ya Saba haijavunjwa. Ndipo yule asiye na waa . . . Ndipo Mwana-Kondoo akaja kwa ajili ya kile alichokomboa. Alikuja kudai kile alichokuwa amekomboa. Tayari anacho, papa hapa katika kile Kitabu, akakichukua kutoka mkononi Mwake. Sasa Yeye anakuja kupokea kile Yeye alichokomboa. Hiyo ni kazi Yake. Amemaliza. Amekuja kukipokea. Loo, ni—ni wakati wa namna gani! Amehakikisha jambo hilo, Muhuri ya Saba imehakikisha jambo hilo. Akarudi akaja akachukua Kitabu cha Ukombozi!

156 Angalia, ilikuwa ni Ujumbe wa malaika wa saba ambao ulikuwa ufunue ile ya saba, zile Muhuri Saba. Ufunuo 10:7, sasa, mtaona jambo hilo. Mnaona?

157 "Naye akaona Malaika huyu akishuka, akaweka mguu Wake juu ya nchi na juu ya bahari," huyo alikuwa ni Kristo, "alikuwa na upinde wa mvua juu ya kichwa Chake." Mwangalie Yeye, utamwona katika Ufunuo 1, tena, "akiwa na upinde wa mvua juu ya kichwa Chake; alionekana mithili yake kama yaspi na yakiki," na kadhalika. Huyu hapa anakuja, akaweka mkono mmoja . . . "Mguu mmoja juu ya nchi, mmoja juu ya maji; akainua mkono Wake. Yeye alikuwa na upinde wa mvua juu ya kichwa Chake," bado. Huo ni agano. Yeye alikuwa Malaika wa Agano, ambaye alikuwa ni Kristo; aliyefanywa punde mdogo kuliko Malaika,

apate kuteswa. Huyo pale anakuja, "Naye ameinua mikono Yake hata Mbinguni, akaapa kwa Yeye aliye hai milele na milele," Yule wa Milele, Baba, Mungu, "ya kwamba hapatakuwa na wakati baada ya haya," wakati jambo hili linapotukia. Umekwisha. Umetimia. Umemalizika.

158 Halafu Maandiko yanasema, "Na kwenye—kwenye Ujumbe wa malaika wa saba wa duniani," yule mjumbe wa duniani, wakati wa saba na wa Mwisho wa Kanisa, "katika mwanzo wa huduma yake," itakapoanza duniani, kwenye wakati huo, "siri ya Mungu, ya hizi Muhuri Saba, inapaswa kujulikana kwenye wakati huo." Sasa tunaona mahali tulipo. Je! ingeweza kuwa, enyi marafiki, ingeweza kuwa? Angalia, yote yawezekana.

159 Wote wale waliokuwa wamekombolewa kwenye kile Kitabu, Yeye alikuja kwa ajili ya ukombozi. Wote waliokuwa wakombolewe walikuwa kwenye kile Kitabu, waliochaguliwa tangu awali kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye alikuja kuwakomboa. Wote aliokuwa amewakomboa walikuwa wameandikwa mle.

160 Ninataka kuwaulizeni swali sasa. Na ninyi watu kwenye kanda, sikilizeni kwa makini. Hayo macho ya kuchukiza, kichwa hicho cha kuchukiza sana, hivi hiyo ingekuwa ndiyo sababu Ujumbe huu umekuwa ukiwapinga sana wanawake wa wakati huu wa kisasa? Je! huu waweza kuwa ndio Ujumbe wa malaika yule wa mwisho? Yeye alisema nini kule chini mtoni, yapata miaka thelathini na mitatu iliyopita? "Kama vile Yohana alivyotumwa," mnaona, "kutangaza kule kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utakutangaza kule Kuja kwa pili." Kila mahali ulimwenguni, na hivyo ndivyo umefanya, basi kule Kuja hakuna budi kuwe karibu. Angalia kinachotukia sasa.

161 Kwa nini? Nimekuna kichwa changu. Nimegaagaa kwenye mto wangu. Nimetangatanga chumbani. "Una nini?"

162 Siku chache zilizopita, niliwauliza watu wawili niliokuwa nimepanda kwenye gari nao. Nilimuuliza Jack Moore wakati mmoja. Nanyi nyote mnamjua Jack Moore. Ninaenda kwake Shreveport. Nikasema, "Ndugu Jack, umekuwa rafiki msiri wangu kama niliyepata kuwa naye duniani." Na kabla sijamuuliza, nilimuuliza mke wangu.

163 Kama mtu ye yote anajua lo lote juu yangu, ubaya wangu na—na kila kitu, ni mke wangu, mnaona, mtu mpendwa. Nami nikamwambia siku moja, nikasema, "Mpenzi, mimi kama mume wako, ni mhudumu wa Injili. Sitaki kuleta shutuma lo lote juu Yake yule ninayempenda. La. Sitaki kukuudhi. Nisingeleta shutuma lo lote kwako. Mungu anizuie nisifanye jambo lo lote ambalo lingekudhuru. Basi ni zaidi sana namna gani unafikiri lingemdhuru Mungu, jinsi ninavyompenda! Wewe ni mke wangu; Yeye ni Mwokozi na Mungu wangu. Ninataka

kukuuliza swali. Usisitesite. Niambie kweli." Nikasema, "Hivi nimesoma sana . . . "

164 Nami nimeshangaa. Mimi, mi—mimi ni wa kujifanya, wa kuchekesha, wa kipekee. Najua jambo hilo. Kila mtu alisema, "Ni mtu wa namna gani!" Vema, mnaona, huwezi kujifanya mwenyewe. Wewe u kile ulicho, kwa neema ya Mungu.

165 Nami ni—ni—nikasema, "Hivi nimerukwa na akili kidogo tu, mwajua, na—na kwa namna fulani kuingia kichaa?" Nikasema, "Kwa nini ninawahukumu hao wanawake, daima, wakati ninawapenda?"

166 Wao hupiga simu, wanasema mimi nilikuwa "mchukia wanawake," mimi wala sichukii tu kamwe . . . Ati mimi "nawachukia tu wanawake." Mnaona? Hilo ni kosa. Ninawapenda wanawake, ninamaanisha, kama dada zangu.

167 Mimi sitawapapasa mgongoni, kwa kuwa mmekosea. Ninaweza kuwaambia jambo hilo. Ninawapenda mno kiasi kwamba siwezi kufanya jambo hilo. Mwanamume fulani ambaye angefanya hivyo, ni upendo wa namna nyingine. Mnaona? Ninakupenda wewe kwa sababu ninapenda ulicho wewe; wewe ni msaidizi wa mwana fulani wa Mungu, nawe u sehemu yake. Mnaona? Nami na—nakupenda kwa kuwa—kuwa ulifanywa katika mfano wa mwanamume, naye mwanamume alifanywa katika mfano wa Mungu, kwa hiyo basi, nyote pamoja, ninyi ni mmoja katika Kristo. Hiyo ndiyo sababu nawapenda. Jambo jingine lo lote, hamna kitu kwake. Mungu anajua jambo hilo, maishani mwangu mwote. Mnaona? Hiyo ni kweli. Ninawapenda. Kwa nini nisimame na daima . . .

168 Wakati wao wanaposema, "Waambieni wanawake wote, wanaposema watakuja kumsikiliza Ndugu Branham akihubiri, wachanue nywele zao vinginevyo. Wavae kofia ama cho chote kile, maana yeye ataanza kuwakemea juu ya nywele fupi, na nini-hii yenu . . . Msijipodoe hata kidogo," na kadhalika namna hiyo. Hivyo ndivyo walivyofanya. "Loo, yeye amesema watu . . . "

169 Kasema, "Kwa nini wewe usinini hii . . . " Kasema, "Watu wanakuamini wewe kuwa nabii. Kwa nini usiwafundishe wanawake jinsi ya kupokea vipawa vikubwa vya kiroho, na vitu kama hivyo, badala ya kujaribu kuwafundisha upuzi kama huo?"

170 Nikasema, "Kama hawatajifunza ABC zao, watajuaje aljebra?" Mnaona? Jiweke sawa, kwanza.

171 Na nilivyozidi kuhubiri, ndivyo wanavyozidi kuwa wabaya. Halafu mnasema, "Mbona usiache?" La, bwana. Hapana budi kuweko na sauti, shahidi dhidi yake.

172 Mmoja wa watu mashuhuri sana katika huduma leo, aliweka mikono yake juu yangu si muda mrefu uliopita, kasema, "Nitakuombea, Ndugu Branham, kama utaniruhusu kufanya

jambo hilo, kwamba Mungu ataliondoa jambo hilo moyoni mwako." Kasema, "Waache hao wanawake peke yao, katika mambo hayo."

173 Nikasema, nikasema, "Unaamini katika jambo hilo, bwana? Wewe ni mhubiri wa utakatifu."

174 Akasema, "Bila shaka. Siliamini, lakini," kasema, "hiyo—hiyo ni juu ya . . . "

Nikasema, "La."

Akasema, "Hilo ni shauri lao wachungaji."

Nikasema, "Wao hawafanyi jambo hilo."

175 Mtu fulani hana budi kufanya jambo hilo. Ule mto hauna budi kuvukwa. Ngozi haina budi kuchunwa. Mimi sitaki kufanya jambo hilo. Mungu anajua sitaki kufanya jambo hilo. Wengi wa hao wanawake huwalisha watoto wangu, nao wangeyatoa maisha yao kwa ajili yangu mimi, karibu wangeyatoa. Mnafikri, na neema ya Mungu imekwisha kumiminwa na Roho Mtakatifu, mnafikiri ningeweza kusimama kimya na kuona maskini mtu huyo akitumbukia kule ng'ambo katika Umilele bila tumaini, kama sitapaza sauti dhidi yake?

176 Sio kuwa mjuvi; bali roho ya taifa hili, roho wa kanisa, si Roho wa Kristo, sasa; roho ya kanisa, madhehebu, imewatupilia wanawake hawa kwenye uchafu ule huko ng'ambo. Nami ni sauti tu, inayolia, "Tokeni kwake. Ukimbieni uchafu huo." Msimwache ibilisi awafanyie jambo kama hilo. Ni kosa!

177 Na ninyi Waasemblies of God, mnawaacha hao wanawake, mnawaacha wakate nywele zao, lakini mnawakataza kujipodoa. Kweli hakuna Andiko dhidi ya kujipodoa, lakini lipo linalokukataza kukata nywele zako. Yeye hata hafai kuomba mbele za Mungu, Biblia inasema. Mumewe ana haki ya kumpa talaka na kumwacha. Sawa. Yeye anajitoa kwa ulimwengu kama mwanamke mchafu. Biblia ilisema hivyo. Anamwaibisha mumewe anapofanya jambo hilo. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema hasa. Mnaona?

178 Vema, lakini mwanamke anayejipodoa, tunaona mwanamke mmoja aliyefanya jambo hilo katika Biblia, mmoja tu. Ilikuwa ni Yezebeli. Huyo ndiye aliyejipodoa. Mtu pekee katika Biblia aliyewahi kujipodoa, alikuwa ni Yezebeli, Mungu mara moja akamlisha kwa m—mbwa wakali. Yeye amekuwa fedheha, na hata nini-hii yake . . . Kila kitu, kila kitu kilicho kichoyo kinaitwa Yezebeli.

179 Si lazima ufanye jambo hilo. Si lazima ulifanye. Ni nini kinachokufanya utende jambo hilo basi? Roho wa ibilisi.

180 Hutambui jambo hilo. Ninajua hutambui. Ninyi ni watu wazuri sana. Ninyi ni wazuri. Mnanipa mkono, mnazungumza nami.

181 Nami nawapenda. Hiyo ni kweli. Lakini nikiona jambo hilo, hivi nisingekuwa mnafiki...Paulo alisema, "Mimi sijajiepusha katika kuwatangazia Shauri lote la Mungu." Damu ya mwanamke ye yote isiwe juu yangu kwenye Siku hiyo, wala ya mwanamume ye yote. Nimewaambia Kweli. Nami nimechukia kufanya jambo hilo; si kuchukia kwa sababu sitaki kufanya yale Mungu aniambiayo nifanye, lakini ninawapenda. Sitaki kuwaumiza, kwa hiyo nitafanya nini? Lakini Upendo wa Kiungu usioghoshiwa utakusukuma ufanye jambo hilo.

182 Yesu hata aliomba kuuepa msalaba. "Inawezekana kwamba kikombe hiki kipite?" Kasema, "Hata hivyo, si mapenzi Yangu, Yako."

183 Hivi itanilazimu kuwa jamaa yule anayesema jambo hili? Je! itanilazimu kuwachukua hao wanawake wa thamani ambao ni wazuri sana na kila kitu, na kuwararua vipande-vipande tu? Itanilazimu kufanya jambo hilo? Itanilazimu kuwachukua ndugu zangu wahudumu, na kusimama pale na kuwaambia ya kwamba wao wanapenda pesa na ma—madhehebu zaidi ya wanavyompenda Mungu? Mimi, kwa ndugu zangu wa thamani wanaoweka mkono wao...Loo, hivi inanibidi kufanya jambo hilo? Ee Mungu, usiniache nifanye jambo hilo.

184 Bali mimi sijajiepusha na kuwatangazia ninyi Shauri lote. Ni Upendo halisi ulionisukuma kwenye jambo hilo.

185 Je! hiyo ndiyo sababu Ujumbe huu umekuwa namna hii? Hauko mahali pengine po pote ulimwenguni. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Uko wapi? Vema. Wao wanaogopa. Mnaona? Lakini umekuwa mjasiri. Kweli kabisa. Mungu daima yuko namna hiyo, mnaona. Vema. Je! hii ndiyo sababu wanawake wamekemewa sana na Ujumbe huu? Bila kujua, halikufunuliwa. Nilionyeshwa hilo, bali halikuja kwangu mpaka tu hivi juzijuzi. Mnaona? Angalieni pale. Vema. Hakika linafaa huduma hii.

186 Sasa ngojeni kidogo. Kumewahi kuwa na wakati ambapo umekuwa ni ulimwengu wa wanawake huko nyuma? Naam. Kulingana na historia, katika siku za Eliya, kulikuweko na mwanamke jina lake Yezebeli. Basi alipata utawala juu ya kanisa la Mungu, jambo ambalo Biblia inasema atafanya tena katika siku za mwisho; roho yake, kupitia kwa kanisa, madhehebu. Naye atakuwa kahaba, na makanisa mengine yote pamoja naye watakuwa makahaba, kama tu yeye alivyo. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

187 Ufunuo 17, lilisema, "Yeye ni kahaba, naye ni MAMA WA MAKAHABA." Hiyo haiwezi kuwa ni mwanamume. Hao ni wanawake. Mnaona? Na wote walitupwa, wakiwa hai, katika Ziwa la Moto, wakaangamizwa. Hiyo ni kweli? Haya basi.

188 Angalia, wakati huyo Yezebeli alipojitokeza, kulikuweko na mwanamume aliyeinuka dhidi yake. Mungu alileta mwanamume. Hata hatujui alikotoka. Hakuwa na msingi wa

huduma. Yeye hakuwa kamwe kuhani wala cho chote kile. Alitokea, mtu mkali wa mwituni jina lake Eliya, naye akaweka shoka kwenye shina la mti, nao walimchukia. Si hivyo tu, bali kusanyiko lake zima lilimchukia.

189 Basi wakati mmoja alifikiri amesimama peke yake. Akasema, "La, nina elfu saba bado walio pamoja nawe kabisa." Mnaona? Hilo lilikuwa ni kundi lile lililoteuliwa, mnaona. Daima kuna kundi hilo. Kasema, "Usiogope, Eliya. Ninajua unafikiri umefukuzwa, kwa maana madhehebu yalikufukuza mpaka kwenye kilele cha kile kilima. Lakini," kasema, "nina elfu saba ambao wanaamini jambo lile lile unalohubiri. Mnaona, ninao."

190 Halafu baada ya zamani zake, Rumi ikatawala, kisha ukafikia wakati ikawa ni ulimwengu wa mwanamke tena, mitindo yote ya—ya wanawake, jinsi walivyotoka wamevalia kofia zao na kadhalika, mnaona. Ndipo Mungu akamwinua mwingine akiwa na Roho yule yule juu yake, Roho wa Elisha. Hiyo ni kweli? Naye akasema, "Shoka limewekwa kwenye shina la mti."

191 Basi kulikuwa na maskini mwanamke mchokozi mle ndani, aliyekuwa ameolewa na nini-hii yake . . . akamwacha mumewe, akaolewa na ndugu yake, Herode. Herodia, naye alikuwa mcheshi aliye—aliyejipodoa wa zamani hizo, akacheza dansi. Yeye alimfundisha msichana wake jinsi ya kucheza dansi. Alikuwa na binti, kwa baba yake wa kambo, ba—baba wa kambo; kwa baba, ndugu yake. Herodia! Huyo alikuwa binti ya—ya—ya huyo mwanamke. Basi akamfundisha kucheza dansi, naye akawa mcheza dansi halisi wa kuvua nguo, kama mama yake. Naye alifikiri angeweza kuolewa mara nne ama tano, afanye lo lote alilotaka.

192 Basi huyu hapa Herode anatoka nje. Wote walikuwa Wayahudi, sasa kumbukeni. Walikuwa ni wafuasi wa kanisa. Huyu hapa Herode anatoka nje, na kanisa lake, kumsikiliza nabii huyu, ambaye watu waliamini alikuwa ni nabii.

193 Akaenda moja kwa moja mbele ya uso wa hao wawili, akasema, "Si halali kwako kumchukua." Basi hivi hilo lilimfanya ashikwe na hasira kali! Unaona?

194 Naam, mtu wa kawaida angalisema, "U hali gani, Herodia? Tunafurahi kweli kuwa pamoja nawe katika kusanyiko letu leo." Lakini si Yohana.

195 Yesu alisema, "Mlienda kumwona nani, mlipotoka kwenda kumwona Yohana? Mlienda kumwona mmoja aliyevaa kama kuhani?" "La, huyo anaweza, wa namna hiyo hubusu mtoto mchanga na kuzika wafu." Mnaona? Akasema, "Mlitoka kwenda kuona nini? Upepo, mwanzi unaotikiswa na upepo wo wote? Wanasema, 'Njoo huku, Yohana. Tutakulipa zaidi kama

ukituhubiria. Na, sisi, sisi ndio kusanyiko lililo kubwa kabisa'?" Si Yohana. La, yeye hakuenda hata kidogo kuona jambo hilo.

196 Kasema, "Mlienda kuona nini, basi, wakati mlipoenda kumsikia na kumwona Yohana, nabii?" Yeye akasema, "Nami nasema, kwenu, zaidi ya nabii! . . . mnaweza kulipokea, huyu ndiye nabii alinena habari zake kwamba anakuja, 'Nitampeleka mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, naye ataitengeneza njia ya Bwana.'" Yeye alikuwa mjumbe wa Agano. Akasema, "Hapajakuwa na mtu, aliyezaliwa na mwanamke, aliye mkuu kama yeye alivyo." Mnaona?

197 Mtu wa namna hiyo ndiye Mungu aliinua kwa ajili ya siku hiyo, Eliya, mtu wa mwituni. Yohana, jambo lile lile. Mnaona? Roho wa Eliya alikuwa juu ya Yohana. Naye anasema, itakapofikia siku ya mwanamke tena, Roho huyo atainuka tena, "Kabla ya kuja kwa Bwana, wakati dunia itakapochomwa moto, nao wenye haki watatoka watembee juu ya—ya majivu ya wasio haki, kama majivu chini ya miguu yao." Yeye aliahidi jambo hilo, tena, katika siku hizi. Angalia, Roho Mtakatifu aliahidi jambo hilo. Linafaa kwa siku tunayoishi.

198 Hapana budi kuwe na mtu fulani atakayeinuka. Ambaye hana budi kuja, kwa maana ni BWANA ASEMA HIVI, Malaki sura ya 4. Hiyo ndiyo hasa Yeye aliyosema ingekuwa ishara, "Kabla tu haijaja ile Siku iliyo kuu na ya kuogofya ya Bwana, nitawapelekea Eliya." Naye atafanya nini? "Kuigeuza mioyo ya watoto ielekee Fundisho la baba zao, kurudi kwenye Biblia," kutoka kwenye tofauti hizi za madhehebu, "na kurudi kwenye Biblia, kumrudia Mungu." Hilo ndilo Yeye angefanya. Angalia ni wakati mkuu namna gani tunamoishi.

199 Hao manabii waliwakemea hao wanawake wa kisasa wa siku zao, na wote wawili wakalipia jambo hilo kwa maisha yao. Historia inathibitisha ya kwamba kila moja ya nyakati hizo zilikuwa ni ulimwengu wa mwanamke, wakati wanawake walipotawala.

200 Angalia habari za siku hizi. Tutakuwa na Rais mmoja moja ya siku hizi, inaonekana kana kwamba ingeweza kutendeka sasa hivi. Kwa kweli, huyo mwanamke ndiye Rais. Mnaona? Huyo mwanamume ni kibaraka tu. Hapa si muda mrefu uliopita, katika moja ya mataifa yale mengine, mwanamke huyo alikuwa akisifiwa sana na kadhalika toka kwa watu wote, hata Rais, mwenyewe, akasema, "Mimi ni mumewe." Rais wa Marekani, mnaona. Yeye ndiye anayeongoza kwa mitindo, wanawake wakimfuata, kama tu alivyofanya Yezebeli. Mlisikia mahubiri yangu juu ya *Dini ya Yezebeli*. Mwajua. Mnajua habari zake. Mnaona tulipo sasa?

201 Mnaona kilichotukia hapa, juma moja ama mawili yaliyopita, hapa mjini? Mhudumu wa Imani ya Kiluteri alimwalika kasisi wa Kikatoliki wa Moyo Mtakatifu kuja apate

kuhubiri badala yake, naye akahubiri, halafu huyo mhudumu wa Imani ya Kiluteri akashuka akaenda kwa yule kasisi wa Kikatoliki akahubiri badala yake.

202 Baraza la Makanisa kule sasa, linalokutana huko Rumi. Barua hii ya kueneza habari ambayo rafiki yangu mzuri, David du Plessis; nilipoketi pale na kumlilia juu yake, Kwenye Fourteen-Mile Creek, si muda mrefu uliopita; bila kutambua alilitupilia kanisa moja kwa moja Babeli, wakati kila mtu anasema, "Loo, makanisa yote yatakuwa moja sasa." Naam, ninajua jambo hilo, mnaona, ni vile vile hasa ilivyoandikwa katika kitabu changu cha unabii katika mwaka wa 1933, kwamba jambo hilo lingetukia. Mbona, hivi hamtambui huyo ni Shetani akiunganisha pamoja? Biblia inasema hivyo. Na baada tu ya muda kidogo, baada tu ya muda kidogo, mara tu watakapokuwa mmoja, ndipo wasio wa kimadhehebu wamekwisha, mnaona. Hiyo ndiyo itakayokuwa alama yako ya mnyama, sawa. Mnaona?

203 Ni vile sina wakati wa kuendelea na jambo hili, lakini, karibu saa sita kasorobo. Mnaona, ninataka kumalizia jambo hili, kupata jambo hili. Ninaweka tu Maandiko haya humu ndani ambapo mnaweza kuona uwezekano wa mahali tulipo, kisha tutafunga katika dakika chache tu.

204 Sasa angalieni kile tu kilichotukia. Ma—manabii waliwakemea hao wanawake katika siku hizo nao waliitwa "wachukia wanawake." Hiyo ni kweli. Historia inathibitisha jambo hilo lilikuwa ni kweli.

205 Sasa ngoja kidogo tu. Mnaandika Maandiko, mnataka kuandika Timotheo wa Kwanza 5:6. Biblia ilisema, "Mwanamke anayeishi maisha ya a—anasa za dunia." Haiwezi kuwa ni anasa za mapenzi ya Mungu; kwa hiyo haina budi kuwa hivyo, mnaona. "Mwanamke anayeishi maisha ya anasa za dunia huyo amekufa ingawa yu hai." Hivyo ndivyo alivyosema nabii, Mtakatifu Paulo, "Mwanamke anayeishi katika hali hii ya dunia huyo amekufa ingawa yu hai." Basi kama akiikataa rehema, anaweza kuvuka mstari unaogawanya ambapo hakuna nafasi kwa ajili yake tena. Ndipo basi yuko wapi, akiwa na macho yake yaliyopodolewa, nywele zake zilizokatwa? Naye amevuka mstari, bila ya njia ya kurudi, na hapana budi kuwe na huduma itakayomhubiria. Lakini kumbukeni, katika wakati huo, yote imekwisha. Imemalizika. Ni kuzuriwa tu na pepo.

206 Kutakuwako na huduma itakayoonyesha ishara za ajabu sana, Yoeli alisema hivyo, bali hakutakuwa na wakati wa ukombozi. Yote yamekwisha. Mwana-Kondoo tayari amekichukua Kitabu Chake, na kukomboa Kwake kumekwisha. Kama vile Yesu alivyohubiri kwanza kisha akakataliwa, kisha akawaendea wale waliokuwa mle, akawahubiri hao waliokuwa kifungoni, hawakuweza kutubu, hamna wakati wa wokovu,

huduma iyo hiyo itapaswa kurudi tena. Vipi kama jambo hilo lingekuwa ndio ule Mvuto wa Tatu, kwa waliopotea Milele. Vipi kama umekwisha kuwepo? Natumaini sivyo ilivyo. Vipi kama ndivyo ilivyo? Wazia jambo hilo kwa dakika moja tu sasa. Vipi kama ndivyo ilivyo? Hasha! Nina watoto. Mnaona? Lakini hakika inaonekana upo karibu mno hapa.

207 Kwa nini ono hilo lije nilipokuwa mtoto? Kwa nini mimi sijapata kuliwazia hapo kabla? Kwa nini hiyo njozi ikaja mle chumbani hivi juzijuzi, kasema, "Hili hapa"? Iko moja kwa moja katikati ya nini-hii . . . zile—zile nafsi zilizopotea. Naye Yesu aliwahubiri, akawashuhudia, lakini wao—wao hawakutubu kamwe. Na nilivyozidi kuhubiri, ndivyo wanavyozidi kuwa wabaya. Hakuna toba. Hakuna nafasi kwake.

208 Mwana-Kondoo alichukua Kitabu wakati ambapo, zile Muhuri Saba zilikuwa tu tayari kufunguliwa, ile Muhuri ya Sita. Kumbukeni, Yeye alitufícha ile Muhuri ya Saba. Asingefanya jambo hilo. Wakati yule Malaika aliposimama, siku baada ya siku, akisimulia habari hiyo, lakini basi asingefanya hivyo kwa ajili ya hiyo moja. Kasema, "Kukawa kimya Mbinguni." Hakuna mtu aliyejua. Ilikuwa ni kule Kuja kwa Bwana.

"Loo," mnasema, "haiwezekani." Natumaini sivyo ilivyo.

209 Hebu tuendelee mbele kidogo hapa. Nina kitu kilichoandikwa, mnaona. Vema.

210 Kumbukeni, "Yeye anayeishi katika anaza za dunia," kuhusu mambo ya ulimwengu, akitenda kama walimwengu. Angeweza kwenda kanisani na kutenda kama mtakatifu, hilo halina uhusiano wo wote na jambo hilo, mnaona, lakini, "huyo amekufa ingawa yu hai."

211 Angalia yale ambayo madhehebu yamemfanyia. Yalimfanya mhudumu wa Neno Takatifu, ambalo ni kinyume cha Biblia. Wao walimfanya mhubiri. Hilo limekatazwa katika Maandiko. Hata yanamfanya sasa kuwa mtawala, meya, maliwali, kila kitu nchini, na mtumishi katika nyumba ya Mungu.

212 Wakati, yeye ana hatia ya kila dhambi ambayo ilipata kutendwa, yeye ndiye mwenye kuisababisha. Hiyo ni kweli. Sasa, mimi, mimi sizungumzii juu ya haki. Yeye ana hatia. Yeye ndiye alisababisha kila mtoto mchanga kuzaliwa kipofu. Ndiye aliyesababisha kuchimbwa kwa kila kaburi. Ndiye aliyesababisha dhambi, maradhi, huzuni. Gari la kuwabeba wagonjwa haliwezi kupiga honi isipokuwa mwanamke alisababisha jambo hilo. Hakuna kulia kunakoweza kutukia, hakuna dhambi, hakuna mauti, hakuna huzuni, hakuna maumivu, ila mwanamke alitenda jambo hilo. Basi Mungu amemkataza kwenda mimbarani kuhubiri, hata hivyo wao wanafanya jambo hilo. Madhehebu, mnaona yalipo?

213 Yeye ni mungu wa kike. Jinsi ibilisi anavyotenda kazi! Mbona, Wakatoliki wanawafanya, wanawake, miungu,

wanaomba kwao; hiyo ni kweli, mungu wa kike Mariamu, na kadhalika. Ninaona ambapo katika Baraza la Ekumeni wao walisema ya kwamba ingetukia kwamba wao wangeomba zaidi kidogo kwa Yesu kama jambo hilo lingewasaidia Waprotestanti kuingia. Mnaona? Mnaona? Loo, hilo limefunikwa na sukari! "Halibadiliki," wao walisema. Mnaona? Ingali ni ibilisi yule yule wa kale. Biblia ilisema, ya kwamba, "aliwafanya wote kupokea alama kwenye vipaji vya nyuso zao, ambao hawakuandikwa majina yao kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo."

214 Ni Kanisa lililochaguliwa tangu awali ninalozungumzia, si hao kule nje. La, bwana. Kutoka kwenye kila kundi, Yeye aliwatoa aliowachagua tangu awali. Hao ndio Yeye anaowajia, katika kila wakati.

215 Lakini huyo hapo anasimama. Yuko pale. Ndiye huyo; kuhubiri Neno, kuhudumu Neno, kuwa mungu wa kike, na chanzo cha kila dhambi. Biblia ilisema, "Simruhusu mwanamke kumfundisha, wala kuchukua mamlaka yo yote, bali awe mtiifu kama inavyosema—inavyosema torati." Mnaona? Wala yeye hawezi kufanya jambo hilo. Bali wao wanamfanya mtawala wa nchi, meya, liwali; hivi karibuni atakuwa Rais. Hakika. Haya basi. Hivyo ndivyo, hivyo ndivyo inavyoendelea, mnaona. Na watu wanafanya jambo hilo kwa sababu hawajali kuhusu Neno hili. Wao hawataliona kamwe.

216 Waangalie hao Wayahudi wakisimama pale, wanachuoni, watu wazuri. Naye Yesu alisema, "Ninyi ni wa Baba yenu, ibilisi."

217 Vipi kama nilimleta Yeye mahakamani sasa hivi mbele zenu? Hebu tujaribu tu jambo hilo kwa dakika moja, na Mungu anisamehe kwa kuchukua msimamo dhidi Yake; lakini kwa dakika moja tu, kuwaonyesha jambo fulani.

218 Vipi kama ukisema, "Vema, Mimi, Mungu atukuzwe, nilinena kwa lugha! Haleluya! Ninajua. Mimi, naam, ni—nimempata. Mungu abarikiwe. Naam!" A-ha, ulinena?

219 Wakumbukeni Waisraeli hao. Biblia ilisema, baada ya kuwaita hao watu watoke, kisha akawaokoa kutoka Misri, Yeye aliwaangamiza kwa sababu hawakuufuata ule Ujumbe. Mnaona? Walikula mana kutoka Mbinguni. Wao walikula mana ambayo Mungu alishusha duniani wapate kula, nao wakasimama mbele ya mjumbe, na kuona ile Nguzo ya Moto, na kuisikia Sauti ya Mungu, na kuiona ikithibitishwa. Halafu basi, kwa sababu wao walitaka kumwamini Kora, "Kunaweza kuwapo na watu wengi watakatifu. Kunaweza kuwa na *hiki*, *kile*, au *kinginecho*. Hatuna budi kuwa watakatifu, pia. Hatuna budi kufanya yote *haya*. Watu wote ni watakatifu."

Mungu akasema, "Jitenge nao. Ondoka hapo."

220 Musa akasema, "Wote walio upande wa Bwana, nifuateni." Hiyo ni kweli. Mnaona? Naye akaifungua tu nchi akawameza. Mnaona?

221 Wao walikuwa watu wazuri, pia. Hakika, walikuwa wazuri. Walikuwa watu wazuri. Naam, bwana, bali jambo hilo halikufaa. "Si wote wasemao, 'Bwana, Bwana,' bali yeye atendaye mapenzi ya Baba Yangu." "Si yeye aanzaye; ni yeye amalizaye." Kwamba, hakuna njia za mikato; wewe unakataliwa kwenye mwisho wa mbio. Hakuna njia za mikato. Huna budi kuja jinsi tu Maandiko yalivyosema.

222 Kama Yakisema, "Tubuni, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu," hakuna njia ya mkato, kupeana mkono, kujiunga na kanisa wala madhehebu. Unakuja njia hiyo! Isipokuwa ufe kwa nafsi yako, na kuzaliwa na Roho wa Mungu, u—u—umepotea. Ni hayo tu. Hakuna njia za mkato.

223 Mnasema, "Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa." Ninajua. Hilo ni jambo zuri. "Vema, mama yangu. . . " Sishuku jambo hilo, bali huyu ni wewe ninayezungumza naye. Mnaona? Huna budi kupitia Njia hiyo, kwa sababu hakuna njia za mkato; wewe umekataliwa ifikapo kwenye ile Hukumu. Unapitia Njia moja.

224 Kuna Njia moja tu, naye Kristo ndiye Njia hiyo. Naye Kristo ndiye Neno linaloishi ndani yako, ambalo huthibitisha kila kitu alichoahidi katika wakati wake. Mnaona? Mlilipata jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. Angalieni sasa.

225 Watu wengine wanasema, "Watu hawa ni wazuri." Hakika. Sisemi kwamba si watu wazuri. Sisemi Mtakatifu Cecilia na hao wengine hawakuwa wanawake wazuri; vivyo hivyo mama yangu pia, lakini hakika mimi simwombi yeye. La hasha. Bila shaka, nimewaona watu wengi sana wazuri, bali wao si miungu wa kike. Wao ni wanawake, wanaume. "Kuna Mpatanishi mmoja tu kati ya Mungu na mwanadamu."

226 Basi kwa nini, kwa nini mtu, Mpentekoste, mtu wa ulimwengu. . .ile barua ya kupashana habari ambayo Ndugu duPlessis, ndugu yetu mpendwa, amesambaza. Labda wengine wenu mnayo. Aliketi. . .Naam, mnayo. Katika Baraza la Ekumeni, karibu na papa, naye akasema, "Lilikuwa ni jambo la kiroho sana." Huo ni upambanuzi wa roho, sivyo? "Loo, Roho wa Bwana alikuwa pale, la kiroho sana." Naam. Haya basi.

227 Kwa nini? Kwa sababu ni nafasi ya kuwaunganisha Waprotestanti pamoja nalo, jambo ambalo tumepiga vita kwa miaka kadha wa kadha, nayo Biblia imelitetea na kutwambia kwamba jambo hilo lingekuja. Ndipo nini hii yetu. . .mmoja wa viongozi wetu walio wakuu sana anaingia moja kwa moja, kasema, "Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo tunafanya," na kanisa lote la Kiprotestanti linadanganywa na jambo hilo.

228 Na barabara kabisa, kama ukitazama pale juu, BWANA ASEMA HIVI. Kwanza, Neno lilisema jambo hilo. Kisha Roho wa Bwana akasema, katika mwaka wa 1933, ambaye alisema mambo haya mengine yote kuhusu mataifa yakiingia vitani, na jinsi ambavyo mitambo ingekuwa, na kadhalika namna hiyo, kasema hivyo ndivyo hasa ingetukia mwishoni. Na ndilo hili hapa. Halijashindwa kamwe. Basi hapa tunaliona likijiandaa.

229 Mnakumbuka mahubiri yangu juu ya *Dini ya Yezebeli* si muda mrefu uliopita? Mnamkumbuka Elisha akishuka kuja barabarani asubuhi ile, kuwaambia? Hilo, nilihubiri juu ya jambo hilo. Mnaona? Na jinsi nilivyobashiri wakati huo ya kwamba wakati ungekuja ambapo hii Halmashauri ya Ekumeni hatimaye ingefanyika alama ya mnyama, kwa maana ingeungana na yule mnyama. Inafanya jambo hilo. Katika wakati wangu, nimeishi kuona jambo hilo. Na hapa Waprotestanti, kwa mamilioni, wanadanganywa na jambo hilo. Kwa nini? Hilo ndilo wanalotafuta.

230 Wao ni vipofu! Yesu aliwaambia Mafarisayo hao, "Enyi viongozi vipofu wa vipofu. Kipofu akimwongoza kipofu," Yeye alisema, "si wote wataanguka shimoni?" Na huko ndiko wanakoangukia. Ningewezaje kuamini ya kwamba mtu aliyesimama pamoja nami na kuzungumza nami, angeweza kuketi na kutoa tamshi kama hilo! Mnaona, "Limefichwa, macho, kutoka kwa wenye hekima na wenye akili, na kufunuliwa watoto wachanga wanaoweza kujifunza."

231 Ninajua siku moja jambo hilo litanigharimu maisha yangu. Hiyo ni kweli. Litanigharimu, lakini hapa Ukweli unajulikana. A-ha.

Wa kwanza kufa kwa ajili ya mpango huu wa Roho Mtakatifu,
Alikuwa Yohana Mbatizaji, bali yeye hakutoroka; alikufa kiume;
Kisha, akaja Bwana Yesu, wao wakamsulubisha,
Yeye alihubiri kwamba Roho angemwokoa
mwanadamu kutoka dhambini. (Hiyo ni kweli?)

Kisha wakampiga Stefano kwa mawe, alihubiri dhidi ya dhambi,
Aliwakasirisha sana, wakakipondaponda kichwa chake;
Lakini alikufa katika Roho, akakata roho,
Ndipo akaenda kuungana na wengine, lile jeshi litoalo uhai.

Kuna Petro na Paulo, na Yohana mtawa,
Waliyatoa maisha yao kusudi Injili ipate kung'aa;

(Walifanya nini?) Waliichanganya damu yao, pamoja na manabii wa kale,
Ili Neno la kweli la Mungu lipate kusimuliwa kwa uaminifu.

Nafsi zilizo chini ya madhabahu, zilikuwa zikilia, “Hata lini?”
Bwana awaadhibu wote waliofanya makosa;
Lakini kutakuweko na wengi watakaotoa
damu ya maisha yao (naam, hiyo ni kweli)
Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu na mafuriko yake mekundu.

232 Inaendelea kudondoka damu! Naam, itafanya jambo hilo siku moja, bali ninangojea saa hiyo wakati itakapomalizika.

233 Dada fulani hivi karibuni alipata ndoto. Akaituma kwangu, kasema, “Niliwaona, kanisa hilo likijiandaa jinsi litakavyoua” mimi, kisiri, siku moja wakati nitakapokuwa nikitoka kwenye motokaa yangu, nikiingia, nipigwe risasi kutoka . . . Lakini kasema, “Ndipo Roho akasema, ‘Si kwenye wakati huu, lakini litatukia baadaye.’” A-ha.

234 Mungu anizuie nisipatane juu ya cho chote. Sijui kitu ila Yesu Kristo naye amesulubiwa. Tunaishi katika siku ya kutisha. Dhambi imesababisha jambo hili. Naam. Wao—wao walimpiga Stefano kwa mawe. Walikikata kichwa cha Yohana, mwanamke alimkata. Sijui jinsi tutakavyoyatoa yetu, bali yatatatolewa, siku moja. Vema, angalia.

235 Katika Yohana Mtakatifu, kama ulitaka Andiko hilo juu ya jambo hilo. Yohana Mtakatifu 6:49, ndipo walipokula mana, naye Yesu alisema, “Nao, kila mmoja wao, amekufa.”

236 Unasema, “Vema, da—dada yangu, nilimwona mwanamke huyu akicheza katika Roho.” Loo, naam. A-ha. “Ninawaona wakitenda jambo hilo. Nimewaona wakinena kwa lugha. Nimemwona . . . ” Naam.

237 Yesu alisema, “Wengi watakuja Kwangu katika siku ile, na kusema, ‘Nimefanya mambo haya yote.’” Mnaona? “Walikula mana jangwani,” Yesu alisema, “nao, kila mmoja, ametengwa Milele. Wamekufa.” Hiyo ni kufa Milele. Walikufa papo hapo jangwani.

238 Mnakumbuka Waebrania sura ya 6, “Hao waliopata ujuzi wa ile Kweli, kisha wakakataa kutembea katika Hiyo, hakuna tena toba kwa ajili yao.” Mnaona, mwamini wa mpaka- . . . Wakati mtu ameonyeshwa ile Kweli kwa wakati wa mwisho, nao wanakataa kuipokea; wkulingana na Kitabu cha Waebrania, mnaona, wao watanini hii . . . hakuna hata kitu cho chote ulimwenguni kinachoweza kuwokoa.

239 Wao wamekwisha. Hamna toba, hamna ukombozi, hamna kilichosalia kwa ajili yao. Wao wametengwa Milele. Biblia

ilisema jambo hilo, "Wakiutazamia ukali wa moto na hasira itakayowaangamiza hao wapingao." Basi wakati Kweli ya Injili imehakikishwa, imethibitishwa kwelikweli, kisha wanageuka na kuondoka Kwake, wao wamekwisha. Hivyo tu. Ni jambo la kuchukiza sana, bali sina budi kulisimulia.

240 Kumbukeni wale Malaika ambao hawakukaa mahali pao, bali waliachwa pale katika nyumba hiyo ya jela katika giza, ambamo ulimwengu unatembea leo katika kifungo hicho hicho, hapana toba.

241 Kumbukeni miaka michache iliyopita, nilisema, niliposhuka kutoka Chicago, "Aidha Marekani itaupokea mwaka huu, au haitaupokea kamwe." Mnaona mahali limekwenda? Naam.

242 Sasa sijui kama ule Mvuto wa Tatu ungeweza kuwa namna hiyo? Ee Mungu, na liwe mbali na jambo hilo! Je! hiyo ndiyo sababu ya ule Mvuto wa Tatu? Ingewezekana kuwa ni huo? Loo, jamani! Wazieni jambo hilo, marafiki. Wazieni jambo hilo; sitaki kufanya hivyo.

243 Yesu alisema, "Unafiki wa namna hii . . ." Kama mkitaka kuliandika hilo, Mathayo 23, -saba. Ni—nimeliandika hapa, "soma hilo," lakini mnaweza kuona. "Enyi Mafarisayo vipofu!" Hebu . . .

244 Mna dakika zingine chache? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh] Hebu tuone. Hebu tufungue tu hapo, maana nilisema "soma hilo." Kuna jambo fulani hapo ninataka kusoma kabla tu . . . Sasa labda nitaondoa jambo lingine, lakini hebu—hebu tu tupate tu jambo hili kwa dakika moja. Mathayo 23, kwa dakika moja tu, vema, nasi tutaanzia kwenye aya ya 27. Sikilizeni tu sasa. Someni hayo yote mtakapoenda nyumbani, mkitaka. Dakika chache tu zaidi.

245 Sasa angalieni hapa. Mathayo 23, na kuanzia aya ya 27, "Ole wenu, waandishi!" Naam, kumbukeni, hawa anaozungumza nao ni watu watakatifu.

> *Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! kwa kuwa mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa*, (hiyo ni watu waliokufa, mnaona), *makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya* mtu aliyekufa, *na uchafu wote*.

246 Unafiki na wivu na ugomvi, ndani yao; nje, "Mimi ni Daktari *Fulani*."

> *Vivyo hivyo ninyi nanyi, kwa nje mwaonekana kwa watu kuwa wenye haki,* (angalia lile Baraza la Ekumeni na hao Wapentekoste wameketi pale), *bali ndani mmejaa unafiki na maasi*.

247 Maasi ni nini? Jambo unalojua kwa kweli ni kweli wala hutalifanya. Yesu, sasa angalieni kile Yeye . . . ni kizazi gani anamoliweka jambo hili sasa.

> *Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! kwa kuwa mnayajenga makaburi ya manabii, na kuyapamba maziara ya wenye haki*, mnaona, "Loo, hao manabii!"
>
> *Na kusema, Kama sisi tungalikuwako zamani za baba zetu, hatungalishirikiana nao katika damu ya manabii.*

248 "Tungaliliamini Neno la Bwana kama tungaliishi kule nyuma." Hebu angalieni.

> *Hivi* mnashuhudia *wenyewe, ya kwamba ninyi ni wana wao* waliooua *manabii.*
>
> *Kijazeni basi kipimo cha baba zenu.*

249 Hilo ndilo tu linalotendeka. Sasa angalieni analosema hapa.

> *Enyi nyoka,* na *wana wa majoka, mtaikimbiaje hukumu ya jehanum*?

250 Mnawezaje kufanya jambo hilo? Sasa yeye anazungumza na wahudumu, mnaona, hiyo ni kweli, watu watakatifu. Unawezaje kusimama na kujua Biblia inabashiri na kuwaambia watu wasifanye jambo hilo, nawe unaweza kusimama na kupatana kwa ajili ya dolla chache chafu na zinazonuka, kwa ajili ya kupendwa na watu fulani, na mtu fulani kukupigapiga mabegani na kukuita "Daktari"? Unawezaje kusema unawapenda hao watu?

Mimi ninahubiri kwenye kanda, pia. Mnaona?

251 Unawezaje, unawezaje kusema unawapenda hao watu, na kuacha kitu kama hicho kutukia? Mnaona? Enyi—enyi Mafarisayo, enyi vipofu, enyi nyoka, enyi kizazi cha majoka, mtaikimbiaje hukumu ya jehanum? Wakati ninyi . . . Mtu anawezaje leo, anayejua ya kwamba mambo haya ni makosa, na kusimama pale kushikilia kusanyiko lake, kuyaendeleza madhehebu yake, kisha ashindwe kuwaambia wanawake na wanaume? Mtaepukaje ile hasira ya jehanum, na huku ilifanywa kwa ajili yenu? Mtafanyaje jambo hilo? Mnaona?

252 Sikilizeni, sikilizeni hapa. Itakuwaje? "Kwa hiyo . . . " Aya ya 34.

> . . . *angalieni, Mimi* nitatuma *kwenu manabii* . . .

253 "Mimi nitatuma," siku za usoni. Hao hapo Mafarisayo wako wakirudi tena. Mnaona?

> . . . wenye *hekima na waandishi; na wengine wao ninyi mtawaua na kuwasulibisha, na wengine wao mtawapiga katika masinagogi yenu, na kuwasaka katika kila mji*;

254 Yeye alibashiri angewapelekea manabii, wakiwa na Neno la Bwana. Nao wangefanya nini? Jambo lile lile baba zao

walilofanya, maana hivyo ndivyo mlivyo. Mnaona, roho hazifi. Watu waliopagawa nazo hufa, bali hizo roho hazifi. Yeye alisema, “Ninyi ni wana. Ninyi ndio.” Basi angalieni tu jinsi mambo haya yalivyo.

255 Jinsi ambavyo Mtakatifu Paulo alisimama pale (mnaamini yeye alikuwa ni nabii?) na kuwahukumu hao wanawake, kukata nywele zao; akayahukumu madhehebu yao; akatangaza ya kwamba kila mtu ambaye hakubatizwa katika Jina Lake Yesu Kristo hana budi kuja na kubatizwa tena. Hiyo ni kweli.

256 Na siku hizi wao wanapatana na kulitia sukari kila mahali. Hawajui tofauti, hata hivyo. Ni jambo la huzuni. Kama ile saa imekwisha, huenda nikasema jambo hili, mnaona: wao walikuwa vipofu, walichaguliwa tangu awali kuwa vipofu. Mungu na aturehemu. Wasingeona jambo hilo.

257 Yesu alisema, “Ninyi ni vipofu. Enyi waandishi na Mafarisayo vipofu, enyi wanafiki! Wakati mnaposoma Neno lile lile ambalo hao wote wamesoma, na hapa mnakuja na kunihukumu Mimi. Nami ni vile vile kabisa Neno lilivyosema kwamba ingekuwa katika zamani hizi. Ilikuwa niwe Mjumbe wa siku hii. Mimi ni Masihi,” Yeye alisema, katika maneno machache. “Mimi ni Masihi. Hivi nimeshindwa kuthibitisha jambo hilo? Kama sijafanya yale yaliyoandikwa juu Yangu, basi nihukumuni Mimi. Nanyi Mafarisayo vipofu mnawaongoza watu wenu kuwaingiza moja kwa moja katika kitu kama hicho, na kutuma kundi hilo lote.” Kasema, “Vema, vipofu wanawaongoza vipofu.” Kasema, “Ninyi ni . . . ”

258 Mlisema, “Loo, kama tungaliishi kule nyuma katika siku za Mtakatifu Paulo, naam, ningalisimama pamoja na Mtakatifu Paulo.”

259 Enyi wanafiki! Mnaona? Mbona msisimame na Mafundisho yake? Mngelifanya jambo lile lile wakati huo basi ambalo mmefanya sasa, kwa maana ninyi ni watoto wa baba zenu, baba zenu wa kimadhehebu: Mafarisayo, Masadukayo, na wenye kujiona wana haki. Hivyo—hivyo ndivyo ilivyo. A-ha. Nitawaambia, na—na kwa majira tunayoishi, sijui kama hii ingeweza kuwa ndiyo ule Mvuto wa Tatu? Hebu kidogo sasa, mnaona, Yesu alisema, “Watu wa namna hii wanapata hukumu iliyo kubwa zaidi.” Mnaona? Je! hilo si ni jambo baya sana?

260 Kama Mmarekani mkuu, wakati mmoja, wakati adui alikuwa karibu kuiteka nchi hii, kuna mtu katika usiku wa manane, aliyeruka juu ya farasi akaenda shoti barabarani, akilia kwa sauti kuu, “Adui yuaja!” Ilikuwa ni Paul Revere.

261 Mimi ni Mmarekani, pia. Nami nimepanda farasi, usiku huu wa manane, si nikisema adui yuaja, lakini yuko hapa! Yeye haji; tayari yuko hapa! Tayari ameshinda. Ninasikitika imekwisha; akishinda, usiku huu wa manane.

262 Kumbukeni, kule Tucson, wale Malaika saba, kile Ujumbe ulichokuwa, “Kumalizia kwa ile siri ya Mungu.” Mara baada ya jambo hilo, akishuka kilimani . . .

263 Nyote mlisikia juu ya ile milima. Angalieni. Ndugu Fred ana picha zake, na Ndugu Tom. Nami nina baadhi ya hizo picha, sinema fulani, kila kitu. Tutazionyesha hapa siku moja, na kuwaonyesha ni mahali gani lilipokuwa. Nyote mnajua hadithi hiyo.

264 Angalieni, vile vilele vitatu. Akasema, “Huo hapo ule wako wa Kwanza, wa Pili, na wa Tatu.”

265 Naye Ndugu Fred ana picha yake nzuri sana, wakati yeye na Dada Martha walipopita. Mawingu yalikuwa yametoka kwenye ukungu wa nchi, na yalikuwa yameficha hiyo mingine, na ilionyesha tu ile Mivuto Mitatu; mmoja *hapa*, mmoja *hapa*, na mmoja *pale*. Mnaona? Zile saba!

266 Angalieni, ule wa Kwanza, mitatu. Tatu ni ukamilifu. Hapo ndipo hii huduma ilipoanza.

267 Ule Mvuto wa Pili ulikuwa upambanuzi wa roho, ule unabii. (Kwanza ilikuwa ni kuwaponya wagonjwa.) Wa Pili ulikuwa ni unabii uliotoka, nao ulijua siri za mawazo, wakati Neno Lenyewe lilipodhihirishwa. Ambalo, hiyo ni neema.

268 Lakini, kumbukeni, ya saba ni kule kumalizia. Hivi huu ungeweza kuwa ndio ule Mvuto wa kumalizia, yote imekwisha? Ingewezekana? Wazieni jambo hilo sasa. Wazieni tu. Mko wapi? Mnaona? Saba daima ni kumalizia. Mivuto Mitatu!

269 Huduma ya Yesu ilikuwa na Mivuto Mitatu. Mlijua jambo hilo? Angalieni! Nanyi mwe waaminifu, kama mliwahi kuwa maishani mwenu, sasa kwa dakika moja, dakika chache.

270 Mvuto Wake wa Kwanza ulikuwa ni kuponya wagonjwa. Akawa mtu anayependwa sana na watu. Kila mtu alimwamini, ilionekana namna hiyo. Hiyo ni kweli? Alipotoka akaenda akiwaponya wagonjwa, kila mtu alimtaka Yeye aje kanisani mwao.

271 Lakini siku moja Yeye aligeuka akaanza kutabiri, kwa maana Yeye alikuwa ni Neno, Naye alikuwa Ndiye yule Nabii ambaye Musa alinena habari Zake. Basi alipoanza kuwaambia, na kuwaambia jinsi walivyokuwa wanaishi, na mambo waliyokuwa wanafanya, alichukiwa sana. Huo ulikuwa Mvuto Wake wa Pili.

272 Sijui kama imerudia huo mfano tena? Wazieni tu kwa dakika moja. Ingewezekana? Ule wa Kwanza, kuponya, kila mtu. Wa Pili: “Loo, huenda ikawa ni Yesu Pekee. Huenda ikawa ni Beelzebuli, huenda ikawa ni nini hii . . . ” Hilo ni jambo lile lile walilofanya pale. Mnaona? Roho zile zile zikiishi katika watu wa aina ile ile, hao waliohukumiwa wasioweza kuokolewa kamwe,

kwa maana wao walihukumiwa hapo awali; wao, kama Yuda Iskariote, aliyezaliwa mwana wa upotevu.

Mnasema, "Yuda?" Hakika.

273 Kumbukeni, yeye alikuwa mtu wa dini sana, bali hangeweza kwenda umbali wote na Ujumbe. Aliweza kuukubali kwa sehemu, bali uliosalia asingeweza kuuvumilia. Wao wanaweza kuchukua kuponya na mambo kama hayo, lakini inapofikia Mungu kuwanena kindi waweko, basi hilo lina kilindi sana kwao. "Haiwezekani!" Huyo alikuwa ni Yuda. Roho yake inaweza kuishi moja kwa moja kufikia kwenye sehemu hiyo. Hawezi kuendelea baada ya jambo hilo. Mnaona?

274 Wao waliweza kumkubali Musa vema wakati alipoifungua ile Bahari ya Shamu, na kadhalika namna hiyo. Bali ilipofikia kuwaambia, hawakuwa, hao wengine wote hawakuwa wafanye jambo *hili* wala *lile*, wala *jinginelo*: "Yeye anajifanya Mungu, juu yetu." Mnaona, hawakuweza kustahimili hilo, Kora na wengineo. Kwa hiyo, iliwabidi kuwa na madhehebu, kwa hiyo Mungu akawameza tu.

275 Huduma ya Yesu, wakati alipokuwa anawaponya wagonjwa, "Yeye alikuwa mtu mzuri sana, Nabii huyo kijana wa Galilaya! Naam, anawafanya vipofu kuona. Hata amewafufua wafu. Tuna visa vitatu vya jambo hilo. Yeye kweli aliwafufua wafu."

276 Lakini siku moja akageuka, akasema, "Enyi uzao wa majoka. Mnasafisha nje ya chano. Mnaonekana kuwa ni watakatifu, bali ndani yenu, ninyi si kitu ila kundi la majoka." Loo, wakati unabii huo ulipotolewa, ukiyahukumu madhehebu hayo, basi mambo yalibadilika. Wao walimgeuka. Hiyo ni kweli. Na hatimaye, kwa kumkataa Yeye, wakamsulibisha.

277 Lakini huwezi kuiua Huduma. Inaendelea kuishi. Unaweza kumfanya mjumbe alale mauti, bali huwezi kuufanya Ujumbe ulale mauti. A-ha. Sawa. Yeye aliendelea kuishi. Halafu angalia wakati ule Mvuto wa Tatu wa huduma yake ulipokuja. Wa kwanza ulikuwa ni kuwaponya wagonjwa.

278 Wa Pili ulikuwa ni kuyakaripia madhehebu, na kutabiri; yale waliyokuwa wamefanya, kile walichokuwa, na yale yaliyokuwa yanakuja. Kilichopo, kilichopo, kitakachokuja; na kile kilichokuweko, kile kilichopo, na kitakachokuja. Hivyo ndivyo alivyofanya. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."]

279 Bali Mvuto Wake wa Tatu ulikuwa wakati alipowahubiri wale waliopotea ambao wasingeweza kuokolewa tena. Walikuwa kule chini ambako hayo macho makubwa na yaliyopodolewa yalikokuwa, "Uui, Uui!" Akawahubiri nafsi zilizokuwa jehanum, ambazo hazikukubali rehema, lakini zilikuwa zimetenganishwa milele na Uwepo wa Mungu. Lakini hata hivyo hizo ilizibidi kutambua jambo hilo, alichokuwa Yeye, kwa maana Mungu alimfanya Yeye pale.

280 Sijui kama huduma yake inapanda namna ile ile katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa? “Kama Baba Yangu alivyonituma Mimi, Mimi Nami nawapeleka ninyi. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.”

281 Wamepotea, wasingeweza kuokolewa. Walikuwa wamekataa rehema. Huo ulikuwa Mvuto Wake wa Tatu.

282 Sasa kuna swali lo lote? Mvuto Wake wa Kwanza, Yeye aliwaponya wagonjwa. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Huduma Yake ya Pili, Yeye alikuwa anatabiri. Huduma Yake ya Tatu ilikuwa ni kuwahubiri waliopotea Milele. Ile Milima mitatu, na kadhalika; waliopotea, Milele!

283 Huduma ya Nuhu, huduma zote, zilifanya jambo lile lile. Nuhu alihubiri. Hiyo ni kweli kabisa. Akaingia safinani. Basi wakati alipoingia safinani, kulikuweko na siku saba ambapo hamna kitu kilichotukia. Ushuhuda wake uliwahubiri waliohukumiwa.

284 Sodoma na Gomara! Yesu alirejea kwa hiyo miwili kwamba inakuja. “Kabla ya kuja kwake Mwana wa Adamu, ndivyo itakavyokuwa kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.” Yeye alirejea kwa Nuhu.

285 Nuhu alikuwa na Mivuto Mitatu, na ule wake wa Tatu ulikuwa kwa waliopotea baada ya mlango kufungwa. Kwa kuwa, Mungu aliiacha ikae pale, ambapo hakuna mtu angaliweza kuingia wala kutoka. Wao walikuwa ndani. Kwa kuwa, (kama ilivyo kwenye ule mlima wa saba) mlima ulio mrefu kuliko yote, hapo ndipo Yeye aliiweka ile safina, mlima. Mnaona? Hiyo ni kweli?

286 Katika siku za Sodoma, Mvuto wa Kwanza ulikuwa mwenye haki Lutu. Nayo Biblia ilisema, “Dhambi za Sodoma ziliihuzunisha sana nafsi yake yenye haki kila siku,” jinsi hao wanawake walivyotenda na kufanya.

287 Mnakumbuka, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu.” Wao walikuwa wanafanya nini? “Wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa.” Wanawake, mnaona, wanawake. Ilikuwa nini katika siku za—za Sodoma? Wanawake.

288 Na ujumbe wa Kwanza ulikuwa ni Lutu. Wakamcheka kwa dharau.

289 Ndipo wakawatuma wajumbe wengine, wawili wao, nao wakashuka wakaenda. Huo ulikuwa Mvuto Wake wa Pili kwa ajili ya Lutu . . . kwa ajili ya Sodoma.

290 Lakini mwangalie yule Mmoja aliyeenda mwisho, kuna rehema zaidi na zaidi. Ilikuwa imekwisha wakati huo, imekwisha wakati huo. Huyo Mjumbe wa tatu aliyeshuka akaenda kule chini, ule Mvuto wa Tatu, Yeye alikuwa ni nini? Alikuwa na huduma ya namna gani? Yeye aliketi pamoja na

wateule, ndipo akawaambia kilichokuwa kinatukia nyuma Yake. Hiyo ni kweli? Lakini alipoingia Babiloni, ama Sodoma, Yeye alitaka kupata . . .

291 Hata Ibrahimu, akilia, "Kama ningalipata wenye haki hamsini?" Mpaka akafikia "wenye haki kumi."

Mungu akasema, "Haya, tafuta kumi wenye haki."

292 Hebu nikwambie jambo fulani, dada, dakika moja tu. Huenda ukawa wa mtindo wa kale, bali una jambo fulani ambalo hawa malkia wa zinaa hawana. Una kitu ambacho asingeweza kupata kamwe. Kweli. Huenda ukawa wa mtindo wa kale katika mavazi yako, unavalia kama bibi. Huenda wao wakasema, "Mwangalie yule maskini mtakatifu anayejifingirisha." Usijali. Yeye ana kitu fulani ambacho maskini malkia huyo wa kale wa zinaa, anayeufanya ulimwengu wote umwangalie huko nje, hana kitu hicho. Hawezi kuwa nacho kamwe. Amepotea, Milele. Amehukumiwa. Mnaona? Yeye kamwe haja-. . . Una uadilifu; una wema. Yeye hana kitu. Yeye ana chambo kinachonasa nafsi zilizopotea kuziingiza jehanum. Vipofu wanaingia ndani yake. Sasa, una kitu fulani.

293 Unajua, huenda hata usiwe kwenye kitabu cha kanisa, bali huenda ikawa ni maisha yako yenye haki yanayoishikilia hasira ya Mungu kutoka ulimwenguni leo. Ulimwengu hautaamini jambo hilo. Wewe mwanamke unayeitwa mtakatifu anayejifingirisha, ewe maskini mwanamume mdogo ambaye karibu hujui kitu, bali unamlilia Mungu, usiku na mchana, kwa ajili ya dhambi za nchi, huenda ikawa wewe ndiwe unayeshikilia ile hasira isianguke. "Kama ninaweza kupata kumi, nitauacha. Kama ninaweza kupata kumi!" "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa." Mnaona ninalomaanisha?

294 Si, "Kama ninaweza kupata Wamethodisti kumi, kama ninaweza kupata Wabatisti kumi, kama ninaweza kupata Wapentekoste kumi, kama ninaweza kupata wana riadha kumi, kama ninaweza kupata wabunge kumi, kama ninaweza kupata wahudumu kumi."

295 Bali ni, "Kama ninaweza kupata wenye haki kumi!" Kuna Mmoja aliye mwenye haki, huyo ni Kristo. Kristo akiishi ndani, Mmoja katika hao—hao kumi, mnaona, "Nitauacha."

296 Lakini yule mjumbe wa mwisho aliwahubiri waliohukumiwa. Mnasema . . . Yeye alishuka kwenda kule. Maandiko hayasemi kilichotukia, bali moto ulishuka asubuhi yake, hiyo ni kweli, baada ya kufanya ishara hizo, mara baada ya kutimiza huduma yake ya kinabii. "Mbona Sara amecheka?"

Akasema, "Sikucheka."

Kasema, "Naam, ulicheka." Mnaona?

297 Naam, mara baada ya jambo hilo, Yeye aliingia Babiloni, ama akashuka kwenda Sodoma. Hakuwapata, kwa hiyo moto

ukashuka. Alimpata Lutu na binti zake wawili, kasema, "Ondokeni humu sasa hivi." Mnaona? Ikatoka. Alishuka akaenda kule. Kumbukeni, Yeye alikuwa akishuka kwenda Zake. Alikuwa amewatuma wajumbe mbele Zake, bali Yeye alishuka akaenda Mwenyewe, kweli, kuona kama jambo hili lote lilikuwa hivyo. Naye aliukuta huo umejaa nini? Wanawake waliojipodoa. Ujumbe kwa waliohukumiwa. Walifanya nini? Waliucheka.

298 Wao wanafanya nini leo? Jambo lile lile. "Mimi ni mfuasi wa Assemblies. Mimi ni mfuasi wa Oneness. Mimi—Mimi . . . Nimecheza katika Roho. Mungu atukuzwe, ninanena katika . . . " Vema, endelea. "Nitakata nywele zangu nikitaka. Nitafanya jambo *hili*. Nita—nitasema tu *hivi*. Si lazima nibatizwe katika Jina la Yesu. Si—sijali nini kilisema. Paulo ni maskini mchukia wanawake, hata hivyo. Hiyo ni . . . " Vema, endelea.

299 Moja ya siku hizi, kama bado hujavuka, utavuka mstari huo. Hutatamani tena kufanya lililo sahihi. Umesikia nililosema? Ni jambo la . . . Ndugu, dada, unatambua lililosemwa? Utavuka mstari huo, nawe kamwe hutataka kufanya jambo hilo. Ungali utaisikia Injili, hakika, bali hutaikubali kamwe. Huwezi kuikubali. Lakini Injili itahubiriwa kwa waliohukumiwa, hao ambao wamepotea Milele, hawawezi kuokolewa, tena. Wewe tayari uko kwenye sehemu hiyo, nawe hujui. Unafikiri unaishi katika anasa, nawe umekufa ingawa unaishi.

300 Loo, sikilizeni. Wote wale ambao waliukataa Ujumbe wa zamani hizo, kabla ya hukumu, Injili ilihubiriwa kwa waliohukumiwa, kwanza, kabla wao hawajaondoka; bila rehema. Nuhu, alipofungiwa, alikuwa ni ushuhuda. Mungu aliufunga mlango, baada ya Mvuto wake wa Tatu. Baada ya ule Mvuto wa Tatu huko Sodoma, milango ilifungwa. Hapakuwepo na rehema tena. Wale kumi hawakuweza kupatikana. Nao waliopotea walihubiriwa Injili, ambao hawakuweza kuokolewa, kwa maana ilikuwa tu . . . Imekuwa namna hiyo katika kila wakati, kila wakati unakataa Ujumbe kabla ya hukumu.

301 Wao wamefanya jambo hilo tena? Jambo hilo linatukia katika Nguzo ya Moto hapa chini mtoni? Jambo hilo linatukia katika Ujumbe la kuwakemea wanawake, na kutupa mahali linapopaswa kuwa, na kuwakemea wahudumu wale wanaojiunga na madhehebu badala ya kukaa kwenye Neno? Ambapo, Mungu amethibitisha kwelikweli kwamba ni Yeye, wala si maskini mtu asiye na maarifa wala elimu kama mwanadamu. Ni Mungu! Basi hivi tumefikia mahali ambapo ule Mvuto wa Tatu ungerudi tena kwa waliopotea, Milele?

302 Hiyo ndiyo sababu nilipewa lile ono, kama mvulana mdogo sana kule ng'ambo? Nami nimekwenda Magharibi, na kuna ule Msalaba wa thamani wa Injili ukiangaza chini, umeitangaza ishara kutoka Mbinguni, barabara. Kumbukeni,

ule Msalaba ulikuwa kwenye mandhari, kama—kama piramidi, pia, iliyojengwa. Mnaona? Ingeweza kuwa kwamba ni sehemu ya kichwa ambapo imeishia, na kuanza kutoka *hapa* na kufikia kifuniko?

303 Kama vile Piramidi, ilikuja kupitia Luther, Wesley, Pentekoste, kisha kule kufunikwa kwa lile jiwe. Ingeweza kuwa hiyo? Kama hiyo ndiyo, tuko wapi? [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha—Mh.] Huenda, huenda ikawa ndiyo hii. Natumaini siyo, bali haina budi kuwa. [Ndugu Branham anapigapiga mara tatu mimbarani.] Itakuwa. Kumbukeni tu, hizo huduma hazina budi, wakati wote huingiliana vivyo hivyo tu, moja kwa nyingine. Haina budi kuja. Mungu habadiliki. Wazia jambo hilo!

304 Uma dhamiri yako kwa meno yako ya kiroho, kisha utafute kujua mahali tulipo. Vipi kama ndivyo ilivyo, nawe ungali jinsi ulivyo? Basi afadhali utembee. . . Umekwisha, hao walio upande wa nje. Baada ya kile Kitabu kuchukuliwa na Mwana-Kondoo, Muhuri ya Sita inafunuliwa pamoja na Mihuri yote, imekwisha. Ingeweza kuwa. Ninatumaini sivyo ilivyo. Ingeweza kuwa. Vema.

Naam, hiyo ndiyo sababu Mvuto huu wa Tatu umekawia muda mrefu hivi?

305 Mnaona, ule Mvuto wa Kwanza na Mvuto wa Pili ulitoka kwa mmoja ukaenda kwa mwingine. Nilibashiri, mnakumbuka, nilipoanza mara ya kwanza, juu ya wa Kwanza. Nami nilisema, "Utafika wakati ambapo Huo utajua hata siri za moyo." Mnakumbuka? Ni wangapi? Mbona, nyote mnakumbuka jambo hilo, katika mikutano yangu kila mahali. Basi usiku mmoja nilienda nikaingia tu Regina, kule juu, nikaenda jukwaani; naye Ndugu Baxter pale, watu elfu kadha. Ndipo mtu fulani akapanda jukwaani, [Ndugu Branham anadata kindole chake mara moja—Mh.] na hapo ukatukia. Na tangu wakati huo imekuwa ni vile vile.

306 Bali imekuwa ni miaka mingi [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha—Mh.] tangu nisimamishe kazi ya nje, minne, yapata miaka mitano tangu nilipoisimamisha. Ni kitu gani? Nini kilisababisha jambo hili? Hivi hiyo imekuwa ndiyo sababu ilikuwa kama ilivyokuwa hapo mwanzo, katika Mwanzo, "Uvumilivu wa Mungu"?

307 Kumbukeni, wakati alipoufanya ulimwengu, siku ya saba hakuumba kitu. Alipumzika. Mnaona? Mungu alikuwa anavumilia katika huo mwaka wa sita, hataki mtu ye yote apotee, bali wote wafikie toba. Mungu alikuwa anavumilia.

308 Tena, pia, katika Mwanzo 15:16, kama ukitaka kuliandika, 16, 15. Yeye alimwambia Ibrahimu, "Huko katika nchi ya Waamori, uovu wao," wao walikuwa Mataifa sasa. "Siwezi kuwapeleka kule ndani sasa hivi, maana uovu wa Waamori,

Mataifa, haujatimia bado. Bali Mimi nitawahukumu. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha—Mh.] Nitakuja katika kizazi hicho cha nne, kisha nitalihukumu taifa hilo kwa fimbo ya chuma." Hiyo ni kweli?

309 Imekuwa muda mrefu sana, hata uvumilivu wa Mungu, ile huduma daima, kupitia kwenye kanda na cho chote kile, umeenea kila mahali ulimwenguni, kuona kama kuna mmoja zaidi? Lakini labda huyo wa mwisho ameingia juzijuzi tu. Imekuwa uovu ambao ume—umekuwa kwa muda mrefu sana? Kama Yesu ni yeye yule, ambapo ndivyo alivyo, Waebrania 13:8, Ujumbe Wake hauna budi kuwa vile vile. (Ninakaribia kufunga.) Kutenda Kwake hakuna budi kuwa ni kule kule.

310 Kama ule Mvuto wa Kwanza na wa Pili hauna swali! Je! kuna swali moyoni mwako juu ya Mvuto wa Kwanza na wa Pili? Je! ulitimia kama tu alivyosema? [Kusanyiko, "Amina."] Basi kwa nini kutilia shaka wa Tatu? Mnaona? Kwa nini kuutilia shaka Huo? Ile miwili ya kwanza ilitambulishwa na Maandiko. Nimewathibitishia asubuhi ya leo ya kwamba ule wa Tatu umetambulishwa na Maandiko, pia.

311 Uangalieni ulimwengu, muone mahali ulipo. Angalieni jinsi walivyoikataa ile Kweli, na jinsi ulivyothibitishwa barabara, ile sehemu ya unabii. Sasa tuko wapi? Ee Mungu, turehemu! Jambo hilo linaufanya moyo wangu kuhuzunika sana kwa ndani. Vipi juu ya jambo hilo? Tuko wapi?

312 Kumbukeni, hivi vilele saba kule juu, wao wangekwambia. Ni. . .Hakuna kilele kingine mbele ya hicho. Kiko kwenye milima ya Continental Divide. Inaendelea moja kwa moja hata jangwani, kutoka mahali pale na kuendelea. Umilele unaingia. Vilele saba, moja kwa moja kwenye Continental Divide. Hiyo ni moja kwa moja kati ya kweli na uongo. Na kwenye mwisho wake, ule Mvuto wa Tatu ulikuwa ndio Mvuto wa mwisho wa ile safu ya milima. Hiyo ni kweli? Mnaona? Vema.

313 Nuhu aliingia, halafu baada ya siku saba, hakuna kitu kilichotukia, mnaona. Katika siku saba ile hukumu ilikuja. Laiti . . . Sikilizeni sasa, katika kufunga. Laiti, katika zamani za Nuhu, wangaliijua ishara hiyo! Laiti wangaliijua tu! Sasa nitafunga. Laiti wangaliijua ishara ile, ulimwengu katika siku hiyo! Ambayo, Mungu alithibitisha hapa, kwa kusoma Maandiko, muda kidogo uliopita, Yeye aliwaangamiza hao watu.

314 Si bila rehema; rehema ilitumwa kwao na nabii. Wasingeiamini. Mungu ni mwenye rehema, lakini, Yeye alituma neema bali wao wasingeipokea. Yeye daima hutuma rehema, kwanza.

315 Vipi kama wangaliijua ishara hiyo ilikuwa ishara ya wakati wa mwisho? Basi walipoona, mara moja, wokovu umeachilia na hapana mtu. . .Mnaona? Nini-hii tu, muda si muda, mlango

ulifungwa. Kama wao. . .Kulikuwa na mtu mmoja tu aliyeijua ishara hiyo, huyo alikuwa ni Nuhu na kundi lake. Huyo ndiye tu aliyeijua. Wakati mlango huo ulipofungwa, Nuhu alijua jambo hilo. Nuhu alijua huo ulikuwa ni mwisho. Alijua jambo hilo. Hiyo ni kweli. Laiti mngaliijua ile ishara!

316 Loo, laiti wangalijua tu ile ishara, wakati walipomwona Huyu akiingia mle, alikuwa kule juu pamoja na Ibrahimu!

317 Laiti wangalijua ya kwamba Billy Graham huyo wa kisasa wa siku hizo, alishuka akaenda kule, yeye na Oral Roberts, na kuhubiri ujumbe ule kwa hao watu waliopofushwa! Laiti wangalijua, hao Wamethodisti wa kale wenye haki na Wabatisti kule nyuma walikuwa ishara kwao ya siku hiyo, Lutu, wakati dhambi zilizichukiza nafsi zao. Basi Wamethodisti na Wabatisti waligeuka wakawa nini? Kama alivyofanya Lutu, jambo lile lile. Lakini wale wenye haki, kutoka pale, wakatoka. Hakika.

318 Vipi kama ingalikuwa wakati Billy Graham aliyeshuka akaenda, wakienda kule wakakate kauli, huku wanatafuna peremende, wakipigana makonde wao kwa wao, na kucheka, wamekata nywele, wamejipodoa nyuso, na hata wasipige hatua yo yote juu ya jambo hilo. Wanarudi kesho yake, naye Billy akasema, "Nina elfu thelathini; ninarudi katika mwaka mmoja, wala hata sina wanaotimia thelathini."

319 "Loo, nilikata kauli. Si—si—sitaenda jehanaum; ninaenda Mbinguni," wakigaagaa moja kwa moja katika dhambi. Laiti wangalinini-hii tu. . .

320 Halafu basi Injili ikihubiriwa katika Nguvu, na ishara na maajabu, pamoja na Nguzo ya Moto juu yake, na kila kitu kikiendelea vizuri kabisa, na kubashiriwa na kuwekwa wazi. Laiti wangali-. . . Wao walisema, "Kundi la watakatifu wanaojifingirisha. Ni uwezo wa kushirikishana mawazo. Namna fulani ya roho wa kichawi. Ibilisi, hivyo ndivyo tu lilivyo Hilo. Msiliamini. Haliko katika madhehebu yetu. Hatuna uhusiano wo wote na jambo Hilo." Laiti wangaliijua ile ishara! Laiti wangalijua!

321 Yesu alisema, kasema, "Laiti ungaliijua siku yako, ewe Yerusalemu. Laiti ungaliweza tu kuitambua! Lakini," kasema, "sasa umeachwa peke yako." Mnaona? "Laiti ungalijua tu. Ee Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi ningewakusanya pamoja, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake, kutokana na hukumu zitakazokuja! Bali hukuijua siku yako." "Ninyi mliowapiga mawe manabii, na kuwaua wenye haki, laiti mngaliijua siku yenu! Laiti mngalijua, na mngalikuwa mnajua Maandiko yenu, na kujua ya kwamba kuja Kwangu kulikuwa ishara ya mwisho wenu. Sasa ninyi ni vipofu. Sasa mmekwisha kemewa. Wakati wenu umekwisha." Na ulikuwa umekwisha. Hiyo ni kweli. "Laiti mngaliujua ule wakati!"

322 Angalieni, Yesu alipotangaza jambo hilo, ulimwengu uliendelea moja kwa moja. Mnaona? Ulimwengu uliendelea moja kwa moja, kama kawaida. Kwa nini? Kwa kuwa wao hawakujua majira yao.

323 Ulimwengu uliendelea moja kwa moja, wakati Nuhu alipoingia katika safina. Ulimwengu uliendelea moja kwa moja. Wenye kudhihaki, katika siku ile, wangali walikuwa na karamu za zinaa. Wangali walikula, wakanywa, wakafunga ndoa, wakafanya mambo wanayofanya leo. Vile vile kabisa, kama kawaida. "Ha-ha! Maskini mtakatifu yule anayejifingirisha alifunga mlango. Naam, mlipata kusikia jambo kama hilo? Ha-ha! Mnajua analosema? Ati sote 'tutazamishwa.' Upuzi huo! Hayo maji yako wapi?"

324 Wenye kudhihaki, katika siku za Nuhu. "Ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Vema. Nuhu alijua ile ishara. Jambo lile lile katika siku za Lutu. Mambo yale yale katika siku za Yesu. Ndivyo ilivyo leo. Wao wanadhihaki kwa mara yao ya mwisho . . .? . . .

325 Vile vile kule Sodoma, wao hawakujua. Wakati Mjumbe yule alipokuwa anasimama pale, Ujumbe kutoka kwa Mungu, wao waliwacheka tu na kujaribu kuwapotosha kwenye matendo yao wenyewe. Hiyo ni kweli? "Njoni mkajiunge nasi. Mwe mmoja wetu." Hiyo ni kweli? "Karibuni mkajiunge nasi, mwe mmoja wetu. Mtakuwa mmoja wa hao wavulana. Karibuni, jiungeni nasi." Mnaona? Wao hawakujua ishara yao kamwe.

326 Wao hawakujua ya kwamba wakati Ujumbe huo ulipokuwa ukiendelea, ya kwamba jambo lile hasa . . . Hawakuweza kuona jambo hilo, kwamba moto na ghadhabu ya hukumu, kama Mungu, miali ya moto wa kiberiti ilikuwa inawashwa angani. Hawakuweza kuona jambo hilo. Wale wajumbe waliweza kuuona. A-ha. Lutu alijua jambo hilo, pia. Alijua ulikuweko. Bila shaka.

327 Ndivyo ilivyo leo, jambo lile lile tu. Ghadhabu inawaka, mabomu ya atomiki yananing'inia, kila kitu kiko katika mwisho. Ni jambo lile lile leo.

328 Angalieni, enyi watu, sikilizeni. Je! mlijua . . . Mnasema, "Ndugu Branham, loo, vipi kuhusu jambo hilo lote?" Mwajua, watu wanaweza kuendelea kuhubiri Injili moja kwa moja kama walivyofanya daima, wanachoita Injili, ingeweza kuwa imekwisha. Walifanya jambo hilo katika siku za Nuhu. Walifanya jambo hilo katika siku za Lutu. Walifanya jambo hilo katika siku za Yesu. Hiyo ni kweli?

329 Hata Wayahudi, baada ya Yesu kuwaambia ya kwamba ghadhabu . . . "Mmekwisha. Mmeangamia. Hakuna la zaidi. Mmekwisha."

330 "Loo," yeye alisema, "mtakatifu huyo anayejifingirisha. Alitoka kwenye shule gani? Alitoka wapi, huyo?"

331 Kumbukeni, Yeye alikuwa tayari wakati huo kwa ajili ya Mvuto Wake wa Tatu. A-ha. Hiyo ni kweli. Yeye alisema, "Ni mara ngapi ningetaka kuwakusanya pamoja!"

332 Lutu alifanya mwito wake wa mwisho. . . ama, ninamaanisha, yule malaika alifanya, yule mjumbe, ye yote yule. Mungu akiwakilishwa kwa ajili ya siku hii, Mungu akiwakilishwa katika mwili wa binadamu, alifanya ishara ya mwisho, akafanya kazi yake ya mwisho. Yote yalikuwa sasa yamekwisha.

333 Nuhu alihubiri ujumbe wake wa mwisho; mlango ukafungwa nyuma yake. Basi. Wao walilicheka jambo hilo, na kulifanyia mzaha.

334 Fikirini, watu wanaweza kuendelea kuhubiri moja kwa moja! Baraza la Ekumeni linaweza kujiunga na kanisa Katoliki, kama tu walivyoahidi kufanya. Madhehebu yote yanaweza kuja, lakini ile alama ya mnyama iko pale tayari. Wao wanaichukua, katika jambo hilo. Mnaona? Nao wanasema, "Loo, haleluya, Mungu abarikiwe, kulikuwa na wengi sana waliookolewa jana usiku." Ati waliokolewa? "Walicheza katika Roho. Walinena kwa lugha." Hilo halimaanishi kitu. Mnaona? "Loo, wao ni wapole na watulivu na wanyenyekevu. Naam, bwana. Wao wana tunda la Roho." Hiyo si ishara kamwe. Hata kidogo.

335 Hebu niwapeni tunda la Roho, kati ya Yesu na Mafarisayo, muone ni yupi aliyekuwa na tunda la Roho. Vipi kama ningesimama, kama vile nilivyoanza kusema hivi punde, dhidi ya Kristo sasa kwa dakika moja? Mungu anisamehe hata kwa kusema jambo hilo, mnaona, bali ili niwaonyeshe tu jambo fulani.

336 Vipi kama nikija kwenu na kusema, "Aisee, enyi kusanyiko, ni yupi rafiki yenu? Ni yupi anayeonyesha tunda la Roho? Maskini kasisi wenu mwema. Ni nani anayewatembelea hospitalini mnapokuwa wagonjwa? Maskini kasisi wenu mnyenyekevu. Hiyo ni kweli. Ni nani huyo anayewakopesha pesa daima wakati mmefilisika, mna shida sana? Enyi wafuasi wa kusanyiko lake, si mnaenda kwa maskini kasisi wenu mwema naye anawakopesha pesa? Mnaona? Ni nani ambaye daima ana upendo na ni mwema, na anaonyesha tunda la Roho? Maskini kasisi wenu mwema.

337 "Ni nani huyo aliyesoma kwa miaka kadha wa kadha, katika masinagogi kule chini, mahali ambapo babu wa babu wa babu wa babu wa babu wa babu yake alikotoka, tokea huko nyuma? Ni nani aliyesoma na kupata. . . aliyejitahidi sana akapata digrii ya daktari na ma-PhD na ma-LLD, apate kulijua Neno hili, na kusimama hapa na kuwahubiri kila Jumapili asubuhi katika kusanyiko lake? Maskini kasisi wenu mwema.

338 "Basi haini huyu ni nani, anayeitwa, 'Yesu'? Alitokea shule gani? Ametoka shule gani? Iko wapi kadi yake ya ushirika? Yeye ni wa madhehebu gani?

339 "Yeye hufanya nini wakati ninyi nyote mnapokuwa na ugomvi wa kifamilia? Ni nani anayewatembelea? Maskini kasisi wenu mwema, kujariu ku-. . . Nawe una mabishano na jirani huyu hapa, ndipo maskini kasisi wenu mwema anakuja na kuwapatanisha. Kasema, 'Ninyi nyote ni watoto wa Mungu. Hampaswi kufanya jambo hilo.' Hivyo ndivyo yeye . . .

340 "Huyu Yesu wa Nazareti anafanya nini? Anakirarua kitu hicho. Yeye hufanya nini? Anayakemea madhehebu yenu. Anafanya nini? Alimwita kasisi wenu 'kiongozi kipofu wa vipofu.' Alimwita 'nyoka nyasini.' Alichukua dhabihu ambayo Mungu aliagiza, na kuzipindua meza, kisha akutupa pesa nje, na kuwaangalia kwa hasira. Mlipata kumwona kasisi wenu akionekana namna hiyo?" Sasa tunda la Roho liko wapi? A-ha. A-ha.

341 Si kwa kunena kwa lugha. Si kwa kucheza katika Roho. Si kwa kujiunga na kanisa. Si kwa tunda la Roho; Christian Science linaweza kuwazidi wo wote wenu katika jambo hilo, unaona, hata na wakane kwamba Yesu Kristo alikuwa Mungu. Si jambo hilo.

342 Lakini ni Neno, likiishi! Hilo hapo. Kama wao wangaliangalia tu, Yeye alikuwa ni Masihi. Alikuwa Neno lililo hai, likidhihirishwa.

343 Basi mwanamume aliye na Roho wa Mungu ndani yake, ama mwanamke, anayeishi Neno hilo, anaishi moja kwa moja katika hayo. Hao ndio walio muhimu sana, hao waliochaguliwa tangu awali, kwa kuwa Neno la Bwana huwajilia wao, nao ni Neno kwa watu. "Nyaraka zilizoandikwa zinazosomwa na watu wote." Hiyo ni kweli? Hivi ule Mvuto wa Tatu unaweza kuwa unaendelea?

344 Watu wa kanda, hao ni ninyi mnaosikiliza kanda hii, laiti mngaliliangalia kusanyiko hili wakati huu. A-ha. Natumaini mnasikia namna ile ile.

345 Vipi kama ndivyo ilivyo? Angalieni Maandiko yaliyolundikwa hapa. Je! ingewezekana kuwa ndio? Je! Mvuto wa Tatu ni wa kuwahubiri waliohukumiwa Milele ambao wameukataa Ujumbe wa wokovu?

346 "Vema," mnasema, "kanisa litaenda . . ." Naam, wao watafanya hivyo. Wataendelea moja kwa moja, vivyo hivyo.

347 Lakini, kumbukeni, wakati wote huu, Nuhu alikuwa katika safina. Bibi-arusi ametiwa muhuri pamoja na Kristo, yule mshiriki wa mwisho amekwisha kombolewa. Ile Muhuri ya Sita imejidhihirisha yenyewe. Ile ya Saba inamrudisha duniani. Mwana-Kondoo alikuja akakichukua kile Kitabu kutoka mkono

Wake wa kuume, kisha akaketi chini na kudai yaliyo mali yake, ile aliyokwisha kukomboa. Hiyo ni kweli? Daima imekuwa ni Mvuto ule wa Tatu.

348 Tatu ni ukamilifu. Huduma ilifikia ukamilifu wake wakati ilipomdhihirisha Kristo tena katika maumbile ya asili, miongoni mwa wanadamu, kama ilivyotabiriwa, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu."

349 Loo, wazeni, watu wangeendelea kuhubiri moja kwa moja, wakififikiri wanaokolewa, wakiamini wanafanya sawa, wakiamini madhehebu yao yanapanuka, hakika, wala hawana matumaini hata kidogo. Basi kama hilo ono lilikuwa ndio jambo hilo, na umekuwa mkali sana dhidi ya wanawake, tumefika kwenye saa hiyo. Mlango umefungwa, imekwisha, tayari kile Kitabu kimo mkononi Mwake. Wazia jambo hilo.

350 Hebu niwaambie jambo hili kabla tu hatujafunga sasa. Ninamaliza. Ilisemwa, juu ya Ireland, kuelekea majini. Kulikuwa na miamba mikuu inayoelekea kando kando ya ukingo wa bahari, mpaka juu huku kwenye kilima hiki kikuu. Basi kulikuwa na mtu aliyekuwa anaenda, akitembea hapo siku moja, kwenye—kwenye wakati tu ambapo bahari hujaa. Basi kulikuwa na muungwana mmoja aliyeishi kwenye kile kilima, aliyejua kupwa na kujaa huku kwa maji. Yeye alijua ni wakati gani mchana maji yalipaswa kujaa. Alijua ni wakati gani maji yaliporudi. Jamaa huyu hakujali ni wakati gani. Alikuwa mmoja wa hawa wajuri. Yeye alikuwa na wazo lake mwenyewe. Alikuwa mwana riadha, jamaa mwerevu, mwenye akili, bali yeye hakujua tu wakati wa maji kujaa. Yeye hakuijua hiyo nchi. Hakujua wakati gani ile ishara ilikuwa imewadia, wakati mwezi ulipokuwa umeshusha mgongo wake kutoka duniani.

351 Basi wakati Mungu anapoishusha Roho Yake kutoka duniani, ndugu, ulimwengu umekwisha, yote yamekwisha.

352 Kama mwezi huo ungalipata kuondoka mahali pake, maji yangeifunika nchi kama ilivyokuwa wakati Mungu alipoliazisha jambo hilo, katika Mwanzo 1. Lakini mwezi unakaa pale, na wakati hata unapogeuza kichwa chake, maji yanaanza kujaa mbio.

353 Mzee huyu mwenye hekima aliyeishi kule katika uwepo wake, alijua jambo hilo lilikuwa ni wakati gani. Jamaa huyu hakujua. Yeye kamwe hakusoma jambo hilo. Hakujali hilo. Ndipo mzee huyu mwenye hekima akatoka mbio, akasema, "Mtu wangu mwema, usithubutu kwenda mbali zaidi. Geuka, upesi. Kuna ukuta. Huwezi kupanda huo ukuta. Utaangamia. Zile . . . Ishara zinaonyesha, ule wakati. Maji—maji yatabubujika kwa nguvu mara moja, nawe huwezi kurudi. Usiendelee mbele zaidi."

354 Ndipo yule mtu akageuka, akamcheka, kasema, "Nenda zako ukashike lako. Ninajua ninaloweza kufanya na lile nisiloweza." Nayo mawimbi yakampata. Mnaona?

355 Huenda muda umeenda sana kuliko tunavyodhani. Mnaona? Mtashikwa. Msiende mbele zaidi. Msifanye hivyo, enyi watu. Kama daima mmeniamini mimi kama mtumishi wa Mungu, lishikeni neno langu asubuhi ya leo, kama mlipata kufanya jambo hilo. Huenda ikawa tayari muda umeenda sana. Maandiko mengi sana yanaonyesha jambo hilo namna hiyo. Naam, kumbukeni, sisemi kwamba ndivyo ilivyo. Sijui. Lakini angalieni tu.

356 Basi nimepunguza yapata kurasa kumi hapa, ambazo niliogopa kuwaambieni. Mnaona? Mnaona? Bibi Woods ni shahidi wa jambo hilo, na Bw. Woods. Niliposhuka kwenda kuwaona asubuhi ya leo, nilisema, "Si—siwezi kuwaambia hao jambo hilo, siwezi kwenda umbali huo. Nitaweka tu kiasi hiki cha Maandiko, na kuwaachia, maana utanaswa." Utasambazwa.

357 Basi watu watauchekea Ujumbe huu. Ni sawa, itakuwa haiwezekani kurudi nyuma, moja ya siku hizi. Endelea, wewe kuwa tu mfuasi wa kanisa. Kata nywele zako, ukazifupishe, ujipodoe uso. Endelea, haya chukua "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," ukitaka kufanya hivyo, jambo hilo, lifanye tu Miungu watatu nawe uwe mpagani. Endelea, shikilia madhehebu yako. Fanya hivyo, ukitaka.

358 Sema, "Nilicheza katika Roho, nilinena kwa lugha; nimempokea."

359 Nimeona pepo wakifanya jambo lile lile. Nimeona wachawi wakinena kwa lugha na kufasiri; na kuandika katika lugha zisizojulikana, wanazifasiri; waliokunywa damu kutoka kwenye fuvu la kicha chwa mwanadamu, na kumwita ibilisi, wakacheza katika roho.

360 Waislamu hucheza katika roho, namna hiyo, mpaka wanaweza kuchukua vibanzi na kuvichomeka chini ya vidole vyao; kisha wanachukua mkuki na kuuchomeka usoni mwao, namna hiyo, na kuutoa, wala hakuna hata tone la damu litakalotoka kwake.

361 Wahindi watatembea motoni, miguu mitupu, wenye kina cha futi tatu; na nne, tatu ama wenye upana wa futi nne; wanauchochea, wanayachochea makaa hata yanakuwa mekundu sana kwa joto; wala wasiungue miguu yao, kisha wanakana kwamba kuna kitu kama Yesu Kristo.

362 La, la, rafiki. Neno ndilo linalofafanua jambo hilo. Watu pamoja na Neno hawana budi kuwa kitu kimoja. Mnaona? Yesu na Neno walikuwa kitu kimoja; Yeye alikuwa Neno. Na wakati Yesu anapoishi katika mwanadamu, hiyo inamfanya mtu huyo na Neno kitu kile kile. Msi. . .Maisha yako yanaonyesha wewe ni nani.

363 Sasa jiangalie tu kwenye kioo cha Mungu cha kuangalia, useme, "Ninaonekanaje asubuhi ya leo?" Tunapoomba.

364 [Ndugu fulani ananena kwa lugha. Mwingine anafasiri.—Mh.]

> Nimetembelea mbali,
> Sasa narudi;

Ombeni, kama mliwahi kuomba!

> Fungua kabisa mikono Yako ya upendo,
> Bwana, naja nyumbani.
> Narudi . . .

365 Huku mkiendelea kuimba, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Kuna mahali moyoni mwako ambapo panaonekana pametiwa giza na dhambi? Kama pako, wakati umewadia sasa kupaondoa, sasa hivi, kama kuna rehema iliyosalia.

366 Jambo hili, natumaini, sivyo lilivyo. Natumaini halipo. Lakini je! linaonekana kana kwamba ingeweza kuwa namna hiyo? Sikilizeni yale ambayo Roho Mtakatifu amenena kati ya watu, baada ya mimi kumaliza, "Ni Sauti kwenu."

367 Basi iwapo pako, una giza lo lote katika maisha yako, mbona usije moja kwa moja hapa karibu na madhabahu sasa, tunapoendelea kuimba. Hivi sasa, kama kuna mahali penye uchovu, kama kuna mahali, usiahirishe jambo hilo zaidi.

368 Nikitumaini na kuamini ya kwamba jambo hili sivyo lilivyo; lakini litakuwa, moja ya siku hizi, na huenda ikawa ni leo.

> Sasa, Bwana, naru- . . .

369 Kwa pumzi ya pua yako karibu tu nawe! Laiti watu wa kanda wangaliona kinachoendelea nje hapa sasa hivi; wanasongamana tu wao kwa wao, wakilia, wakija kutoka kila mahali.

370 Hivi ono lile lingeweza, nilipokuwa mvulana mchanga, hivi saa imewadia? Huu ndio ule wakati ambapo hao wanaoonekana wachovu, wenye huzuni; jehanum ikiumbwa papa hapa duniani?

371 Madhabahu na marefu ya kanisa, na kila kitu, vimejaa sasa. Kama huwezi kufikia kwenye madhabahu na marefu ya kanisa, po pote miongoni mwa hawa mamia hapa; simama tu, kama ukisema, "Ninataka kusimama na kuomba, ili kwamba tu watu wajue," ama kupiga magoti, lo lote unalotaka. Loo, jamani! Sasa ni vigumu kwako kuona mtu ye yote ameketi chini. Ni watu wanaosimama kila mahali.

372 Hebu niseme jambo hili. Mungu na azuie, Mungu na azuie! niliyosema isiwe ni sasa. Naomba nifahamu jambo hilo, kila mtu; Mungu na azuie. Kuna . . . Nina watoto ambao hawajaingia. Nina binti wawili na mwana wa kiume. Nina ndugu. Nina watu wangu ambao hawajaingia. Mungu na azuie! neema isiwe imetuacha; kwamba haya yote yatakuwa ni kujifanya tu.

373 Hivi kuna neema iliyosalia, Bwana? Hebu nikosee kwenye jambo hili, Bwana. Hebu iwe sivyo kwa wakati huu. Kwamba mimi, sivyo ilivyo, kwamba watu wangali wanaweza kuokolewa.

Tujalie, Bwana. Ninaomba, na kulikabidhi kusanyiko hili Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo.

374 Kila mtu aombe sasa, kama tu. . . Vipi kama jambo hilo lilikuwa hivyo? Sasa, sijui kwamba ndivyo lilivyo, bali vipi kama ndivyo lilivyokuwa? Omba kwa namna utakavyo. Omba tu jinsi unavyotaka kuomba. Vipi kama jambo hili lingekuwa ni kweli, tungefanya nini, enyi marafiki? Tungefanya nini? Nini, itakuwaje? Sasa ombeni, kila mtu. Lieni—lieni tu, ombeni tu mnavyotaka. Mlilieni tu Mungu, mtakavyo. Ee Mungu!"

> . . . Mikono Yako ya upendo,
> Ee Bwana, narudi.

375 "Bwana, nilitaka kufanya jambo hilo muda mrefu uliopita. Hivi nimengojea muda mrefu zaidi, Bwana? Hivi, hivi imekwisha? Ee Mungu, ifungue mikono Yako ya upendo na unipokee. Jambo fulani, moyo wangu unaomba sana hilo, Bwana. Ifungue mara nyingine. Kama jina langu lilikuwa katika Kitabu cha Mwana-Kondoo, sema nami, Bwana. Hebu nilipokee sasa hivi. Tafadhali sema nami, Mungu."

> Naja nyumbani, naja nyumbani,
> Lo, kamwe, sitanini hii tena, Bwana, sitatangatanga tena;
> Ifungue sana mikono Yako ya upendo,
> Ee Bwana, naja nyumbani . . .

376 Biblia ilisema, wakati watakapomtambua Yesu, kwamba, "Kila mmoja atalia kama kwamba mwana wao wa pekee anauawa."

> . . . -ja nyumbani,

377 Ninyi mlio nje, ninyi mlio kwenye magari yenu, kwa masafa mafupi, ninyi mnaosimama kila mahali jengoni, wengi wenu, egemeza tu kichwa chako kwenye jengo, useme, "Bwana Mungu, nirehemu. Fungu- . . . " Iweni wanyenyekevu sana, enyi marafiki! Fikirini ni wakati gani tunaoishi! Tuko wapi? [Ndugu Branham anagongagonga mara kadha mimbarani—Mh.]

> . . . upendo
> Bwana, sasa naja nyumbani.
> Naja nyumbani, . . .

378 Bwana Yesu, nimefanya vizuri jinsi nijuavyo. Nimefanya yote nijuayo. Nijalie, Bwana, kwamba milango ya rehema ingali imefunguliwa. Kwa kweli mamia, mamia kweli wakikutafuta Wewe wakati huu, ondoa kila doa la dhambi, Bwana, kisha uwaingize ndani leo.

379 Na—nakusihi, kwa moyo wangu wote, tunapoona si mtu fulani tu akizungumza, lakini, Maandiko Yenyewe yakituleta kwenye saa hii. Na ono lile, la mvulana mdogo, nikiwaona watu hao katika hali hiyo; na sasa, wazieni, ya kwamba jehanum yenyewe, rehema imeondolewa duniani, na sasa jehanum

yenyewe iko hapa, nao watu, Bwana, wako katika hali hii ya kuchukiza.

380 Ee Mwenyezi Mungu, katika Kanisa hili Teule, naomba, Mungu, ya kwamba utamwaga baraka Zako, ili kwamba wapate kupokea hu—huduma ya ushuhuda, kama aliyokuwa nayo Lutu, kama aliyokuwa nayo Nuhu, kama aliyokuwa nayo Yesu, kwa waliopotea Milele, endapo ipo; ili kwamba wao wenyewe wametiwa muhuri kuwa katika Ufalme wa Mungu, lakini wakitoa ushuhuda kwa Yesu Kristo kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tujalie, Bwana. Naomba upokee maombi yetu, kwa kuwa tunakusihi katika Jina la Yesu.

381 Ombeni tu jinsi mnavyotaka kuomba sasa. Msiwe katika haraka yo yote. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara—Mh.] Msiwe katika haraka yo yote. Vipi kama wewe ndilo jina la mwisho kuingia katika kile Kitabu?

> Narudi.
> Narudi, narudi,

382 Ndugu Neville, nende kule, ukawaom bee muda kidogo. Mchungaji ataomba pamoja nanyi sasa mnapoomba. Nitaimba.

> Sasa unikaribishe,
> Bwana narudi.
>
> Narudi, narudi
> Kutoka mbali; (Naam, Bwana.)
> Sasa unikaribishe,
> Bwana, narudi.
>
> Narudi, narudi.
> Kutoka mbali;
> Sasa unikaribishe,
> Bwana, narudi.

383 [Ndugu Branham pamoja na kusanyiko waliimba wimbo ulio hapo juu huku Ndugu Neville akiomba, "Mwenyezi Mungu, Baba yetu wa Mbinguni, kweli, leo, tunafurahi sana kwamba Wewe umetukabidhi, kweli, wakati huu mdogo tupate kutafakari njia zetu mbele Yako. Mungu wangu, leo, kutoka kwenye kilindi cha nafsi yetu, tunakulilia Wewe, Bwana, kwa niaba, si yetu tu, bali mmoja kwa mwingine. Naomba kwamba saa hii, Mungu, iwe ndiyo wakati, asubuhi ya leo, Baba, wakati Wewe, kama umeongeza muda wa rehema, Baba, na iwe, ya kwamba hawa ambao siku ya leo wameacha kiburi chao chote, mawazo, na mambo mengine yote. Bwana Yesu, leo, tunaomba ya kwamba utawajaliahiyo wale wanaopiga magoti, loo, na kuinamisha vichwa vyao kila mahali humu jengoni. Ee Mungu, jalia Sauti hiyo, kutoka watu hawa, ambao ni wanaume na wanawake wanaokufa, Yesu, naomba tupate, siku ya leo, faraja ya Shahidi yule akishuka kutoka Mbinguni asubuhi hii. Katika Jina la Yesu Krisho, tunasihi, Bwana, kama bado kuna kuongezwa muda wa rehema kwa njia ya ile Damu, jalia ije

juu ya kila mmoja, leo, kulingana na kuja kwao. Na iwe hivyo, leo."—Mh.]

[Ndugu Neville anaendelea kuomba. "Pia naomba kila mmoja, Bwana, aridhike, leo hii, kwamba Wewe ni Mwenyezi Mungu. Kama huku kukiwa ni kuongezwa kwa muda wa rehema, na iwe kwa kila mmoja, kibinafsi."] Tujalie, Bwana. ["Na iwe sasa, Baba. Pia jalia amani ya Mungu, ambayo daima imepita ufahamu, na ije tena kwa mioyo inayongojea."] Naam, Bwana. ["Jalia hii iwe ndiyo ile saa."] Naam. ["Tunaamini ya kwamba kwamba umesikia kutoka Mbinguni."] Mungu, tujalie. ["Cho chote kilichowekwa akiba kwa ajili yetu, kama imekwisha, basi, Bwana, tunajua mwisho wake ni nini."] Naam, Bwana. ["Lakini, kama sivyo, naomba yule Shahidi aje."] Naam, Bwana. ["Naomba kwamba hawa ambao wamekuja, wapate amani leo hii,"] Tujalie, Bwana. ["Katika Yesu Kristo. Ni katika Jina Lake tunaomba. Amina."—Mh.]

384 Bwana Yesu ninaomba ya kwamba utamwokoa Becky na Sarah na Joseph, na hao wengine, pia, Bwana. Usiache jambo hili litukie kwa watoto wangu, Bwana. Usiliache litukie kwa ndugu zangu na marafiki zangu. Tujalie, Bwana.

385 Hatujui, hatujui, bali tunaona jambo fulani, Bwana. Je! ni ishara ya kututikisa sasa hivi mbele zetu? Tujalie, Bwana. Tuvute karibu Nawe, upesi, Bwana. Tunakupenda na tunakuhitaji. Na iwe hivyo, Baba, Roho Mtakatifu na atupe faraja katika mioyo yetu sasa.

386 Tunaomba kwamba tuweze kuwa mashahidi Kwako katika saa hii, kwa maana tunajua jambo hili halina budi kutukia kwetu. Limebashiriwa katika nyakati zote, nasi hatuna budi kulikabili, kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho tunapoona ishara hizi zikitokea. Tunajua, na tumeambiwa kwa miaka mingi sasa, ya kwamba jambo hili litatukia. Sasa tunaliona moja kwa moja mlangoni mwetu, ghadhabu kubwa mno ya Mungu ikipitia kote mitaani, ikiwaondoa wasiotahiriwa. Mahali ambapo hapana Damu mlangoni, malaika wa mauti anazuru; nao wanaendelea moja kwa moja kuishi, bali wamekufa ingawa wanaishi, bila rehema, bila Mungu, wala hawawezi kamwe kuokolewa.

387 Mungu, jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya hawa waliookolewa! Jinsi sisi...Ni baraka kuu namna gani kwa mioyo yetu, kuwa ndani sasa, chini ya Damu, wakati huyo malaika wa mwisho anapopitia nchini, akiwachukua wale . . .

388 Wale wasio chini ya damu, walikufa bila rehema. Huo ulikuwa ndio mvuto wa mwisho wa Musa. Wa kwanza, ki—kijana mwanamume akizungumza na Israeli; wa pili, akashuka akaenda kuwakomboa; wa tatu, ulikuwa ndio ujumbe wa mwisho. Miujiza ilikwisha fanyika, Musa alikuwa akienda zake kwenye ile nchi ya ahadi, pamoja na waliokombolewa.

Ee Mungu, turehemu, naomba, katika Jina la Yesu.

389 Sasa ningetaka kuuliza jambo hili. Ninyi mnaoomba, ninyi mnaojisikia ya kwamba mna rehema, na kwamba (Mungu) mnajisikia ya kwamba mmo katika Ufalme wa Mungu, mnajisikia ya kwamba—kwamba mmetiwa nanga kwa njia moja ama nyingine, ya kwamba katika Kristo mna imani ya kuamini ya kwamba ninyi ni Wakristo, mmezaliwa mara ya pili nanyi mnajua ya kwamba ninyi ni Wakristo na hamna shaka. Natamani mngesimama nyote ninyi mnaotaka jambo hilo, mnaoamini hilo, kwamba hiyo rehema imewafikia sasa, nanyi ni Wakristo, nanyi mna-—nanyi mnaamini ya kwamba— ya kwamba ile Damu imetiwa moyoni mwenu, na—na—na kwamba mmesamehewa kila dhambi.

390 Jambo hili lilikuwa gumu sana kuzungumza kwenu ninyi. Ninashukuru sana, nami nawaona watu kutoka kila mahali. Nanyi, ni—nina nini hii sana . . .

391 Sijui kwamba jambo hili ni kweli, lakini halina budi kuwa namna hiyo, wakati fulani. Mnaona, haina budi kufikia hapo, na ingeweza kuwa ni sasa hivi. Mnaona? Kwa kila hali, ulimwengu utaendelea moja kwa moja. Watu wangali watakuja madhabahuni, wangali watalia, bali halitawafaa kitu. Mnaona? Watakuwa wamekwisha, mnaona, itakuwa imekwisha. Hakutakuwako na rehema yo yote. Kumbukeni jambo hilo. “Nayo madhabahu yakafuka moshi.” “Yeye aliye mchafu, ni mchafu bado; yeye aliye mwenye haki, ni mwenye haki bado; naye aliye mtakatifu, azidi kujitakasa.” Hakuna rehema tena, wakati Mwana-Kondoo anapokichukua kile Kitabu; haya basi, ni hayo tu. Na inaonekana sana kana kwamba ingeweza kuwa ni sasa.

392 Labda tuna siku nyingine; labda leo ndiyo siku ile. Labda kesho ndiyo ya mwi- . . . Labda usiku huu ndio usiku wa mwisho. Labda huu ndio mwaka wa mwisho. Sijui, marafiki. Ninawaambia, sijui. Sitaambiwa jambo hilo kamwe.

393 Lakini wakati Mungu atakapolichukua hilo jina la mwisho na kulikomboa kutoka kwenye hicho Kitabu cha Uzima, yote yamekwisha. Mnaona, hawawezi kuweko tena, hata hivyo. Hapawezi kuwa na mwingine, hata hivyo. Hivyo tu. Imekwisha.

394 Ni wangapi wanaojua jambo hilo ni Kweli? [Kusanyiko, “Amina.”] Vema. Ni—ni Kweli. Sasa kwa kuwa tunaona . . .

395 Nami ninaona kusanyiko hili ambalo nimelihubiria na kulionya, miaka hii yote, na kuona Ujumbe kama huu ambao mimi . . . ambao ni—nimeuleta katika hali hii isiyo kamili. Basi kumbukeni tu, ninasema jambo hilo kusudi mpate kufahamu, hali *isiyo kamili*; mambo mengine zaidi karibu yangewashtua kabisa, mnaona. Bali niliyaacha tu, nikasikia kufanya jambo hilo, maana sina hakika. Kama sina hakika

mahali ninapokanyaga, nitakanyanga polepole, mnaona, lakini ninawaambia tu.

396 Sikilizeni. Hivi hamana furaha? Kungeweza kuwa na jambo jingine kuu zaidi, ambalo mngeweza kuwazia, mlilofanya maishani mwenu?

397 Vipi kama sasa wakati umekwisha? Vipi kama yote yamekwisha? "Loo," mnasema, "Ndugu Branham, labda . . . " Naam, najua. Wangeweza kuendelea moja kwa moja. Walifanya hivyo, kila wakati. Nimeeleza jambo hilo na kulithibitisha kwa Maandiko, mnaona, ulimwengu uliendelea kusonga mbele moja kwa moja, lakini ilikuwa imekwisha. Mnaona? Mnaona?

398 "Upumbavu wa kuhubiri huwaokoa waliopotea. Ni upumbavu, kwa mwanadamu. Ni hekima ya Mungu." Mnaona? Mungu ni Roho. Yeye hutenda kazi katika njia za kiroho, mnaona, kutenda maajabu Yake; njia za ajabu. Lakini, sisi ni wanadamu, sisi tuna kikomo. Hatujui; tunaangalia tu yale tunayoweza kuona. Lakini Jambo Fulani ndani yetu . . .

399 Wakati unapotoka kwenye chumba kile hapa, kama hujaona maishani mwako, hujaona kamwe nuru ya mchana, ungejua ya kwamba ulipitia kwenye chumba hiki hapa, ukaingia kwenye nuru ya mchana ama cho chote kile. Ilikuwa na joto. Ungeweza kulihisi. Kama hakuna hisi ya mwili wako kuitangaza, ungejua, loo, hakuna hisi ya uwezo wa kuona upate kuona. Hapana njia ya kuona miti ya kijani kibichi, kuona maumbile; hukuwa na uwezo wa kuona, hakuna mtu aliyepata kuwa nao. Ungejua ungekuwa karibu na kitu fulani; kuhisi kwako kungekwambia jambo hilo. Ungejua jambo hilo. Kama ningejaribu kukwambia, "Ni jua. Linarudisha nuru. Linaonyesha mambo." Mnaona, mngejua kwamba lilikuweko kwa maana mngeweza kuhisi kwa hisi zenu. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

400 Naam, tunajua ya kwamba Kristo yuko hapa. Mnaona? Labda hammwoni kwa macho yenu. Mnaona? Labda hammwoni. Bali kwa ono, ninawaambieni, Yeye yuko hapa. Tunamsikia. Tunajua kuna Kitu Fulani hapa ambacho hisi zetu hazikitangazi. Roho ndiye anayetangaza, kwamba Kristo yuko hapa.

401 Ninajisikia kwamba Yeye ametukomboa. Ninajisikia ya kwamba majina yetu yamo kwenye Kitabu Chake. Ninaamini ya kwamba tumekombolewa kwa Damu ya Mwana-Kondoo.

Ninawapenda, nami ninajua mnapendana ninyi kwa ninyi.

Loo, kibarikiwe kifungo kiifungacho
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Ni kama wa kule Juu.

402 Daima inatupasa kujisikia namna hiyo mmoja kwa mwingine. Mnaona, hatuna budi, hatuna budi kujisikia namna

hiyo mmoja kwa mwingine. Mnaona? Maana, tunapopendana mmoja kwa mwingine, tunampenda Mungu. “Unaweza kumchukia ndugu yako ambaye umemwona, na kusema unampenda Mungu Ambaye hujamwona?” Hatuna budi kupendana sisi kwa sisi. “Hakuna aliye na upendo mkubwa kuliko mtu aliyeutoa uhai wake kwa ajili ya adui Wake, wapate kuwa rafiki Zake.” Lo!

403 Je! mnajua ule wimbo, *Kibarikiwe Kifungo Kiifungacho*? Si ni wa ajabu? Kibarikiwe kifungo! Waweza tafadhali kutupa sauti ya huo, dada, pale? Hebu tu uupige kwa dakika moja.

404 Vipi kama imekwisha? Vipi kama ule Mvuto wa Tatu, unaokuja sasa, ni kuwahubiri waliopotea? Vipi kama mifano yote itaonyesha wazi sasa? Nasi tumeingia, nasi tumeingia, je! jambo hilo halitakuwa ni zuri sana? Ni ushirika wa namna gani!

Loo, kibarikiwe kifungo kiifungiacho

(hii ndiyo inayosababisha jambo hilo)
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Ni kama wa . . . (Endelea moja kwa moja.)

405 Hiyo ilikuwa ni nini? Ushirika wa watu wenye nia moja. “Ufalme Wako na uje. Mapenzi yako yatendeke.” Mnaona?

406 Tunajaribu kumfanya Mungu mvulana wa kutumwa-tumwa, tarishi, ama cho chote kile, “Mungu, fanya jambo *hili*, fanya *lile*.”

407 Yesu alisema, “Ombeni, ‘Ufalme Wako na uje. Mapenzi Yako yatimizwe duniani, kama ilivyo Mbinguni.’” Basi, Mbingu imeshushwa kwetu, nasi tume—tumechukuliwa Mbinguni, na tunaketi katika Ulimwengu wa Roho sasa katika Kristo Yesu. Sote tunaamini Ujumbe huo kuwa ni Kweli, ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, anatukomboa.

408 Hebu tufunge macho yetu sasa kisha tuinue mikono yetu, tunapouimba.

Kibarikiwe kifungo kitufungacho
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Ni kama . . . (Endelea kuucheza.)

409 Naam, kusiwe na hata tabasamu moja. Huu si wakati wa kutabasamu. Kwa unyofu sana, wakati wimbo huo unapochezwa, hebu tupeane mikono na mtu fulani aliye karibu nawe, useme, “Mungu akubariki, Mkristo,” kwa unyofu.

410 Mungu akubariki, Ndugu Neville. [Ndugu Neville anasema, “Akubariki, Ndugu Branham!”—Mh.] Umri wa miaka hamsini na tisa. [Hiyo ni kweli.”] Umekula chumvi nyingi!

Mungu akubariki, Ndugu . . .?. . .

Sasa hebu na tumwinulie Yeye mikono yetu juu.

Tunapoachana,
Inatuumiza kindani;
Bali tungali tutakuwa tumeunganishwa moyoni,
Na kutumaini kukutana tena.

411 Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu, na, kwa pamoja, bila kujua ya kesho, kwa wakati huu, bila kujua ila kwamba imekwisha. Sijui. Siwezi kusema. Siwezi kusema. Sijui. Bali kwa sababu ya kweli ambazo tumezifunua asubuhi ya leo, hebu tuombe ombi ambalo Bwana alitwambia tuombe. Hata kama ni, "Ufalme Wako na uje. Mapenzi Yako yatendeke." Mnaona? Na tufanye jambo hilo pamoja.

412 [Ndugu Branham na kusanyiko wanakariri pamoja ombi lifuatalo, kutoka Mathayo 6:9-13.—Mh.]

. . .*Baba yetu aliye mbinguni,*

Jina lako litukuzwe,

Ufalme wako uje,

Mapenzi yako yatimizwe,

Hapa duniani kama huko mbinguni.

Utupe leo riziki yetu,

Utusamehe makosa yetu,

Kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.

Na usitutie majaribuni,

Lakini utuokoe na yule mwovu.

[kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.]

413 Sasa huku mioyo yetu imeinamishwa. Biblia ilisema, "Wakaimba wimbo, wakatoka." Kumbukeni, wakati walipofanya jambo hilo katika Maandiko, ilikuwa ni kwa sababu wao walikuwa wameisulubisha huduma ya Mvuto wa Pili wa Bwana wetu, nao Mvuto wa Tatu ulikuwa tayari kuingia. Masaa machache baada ya jambo hilo, Yeye alishuka akaenda jehanum na kuwahubiri waliopotea ambao walikuwa wameikataa rehema yao.

414 Sauti ya: *Yesu Kwa Imani.*

Ye—Yesu kwa imani,
Na kutumaini,
Peke Yako;
Nisikie sasa,
Na Kunitakasa,
Ni Wako kabisa
Tangu leo!

Hapa nazunguka,
Katika mashaka,
Na matata;
Palipo na giza
Utaniongoza,
Hivi nitaweza
Kufuata!

415 Bwana awabariki, amfanye Mwanawe pamoja na neema iwaangazie. Na Bwana awape Uzima wa Milele, na awe pamoja nanyi hapa katika ulimwengu huu, na ulimwengu ujao baadaye. Na, Uzima wa Milele, naomba mumtumikie katika wakati usiopimika utakaokuja.

416 Kama huu ndio wakati, nasi tumewasili mahali pale, mimi sioni haya kwa yale niliyohubiri. Na iwapo kila mhudumu hana budi kusimama na kusanyiko lake na kuhukumiwa, kama nilivyoona kwenye lile ono, ninashukuru kwa ajili ya Injili ambayo nimehubiri, kwa kuwa ni Injili ile ile aliyohubiri Paulo na hao wengine.

417 Ninafurahi kwa ajili yenu. Ninafurahi kwa sababu mmempokea Kristo kama Mwokozi wenu. Mpendeni, na muombe.

418 Nami nitawaona alasiri ya leo, Bwana akipenda, saa moja, hapa kanisani. Mungu awabariki. Mnaweza kufumukana.

NAFSI ZILIZO KIFUNGONI SASA SWA63-1110M
(Souls That Are In Prison Now)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, 10 Novemba, 1963, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2004 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1994 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org